# MASHAIRI-HURU: UCHAMBUZI WA DHAMIRA NA MTINDO

NA: MASINDE EDWIN

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya 'Master of Arts' katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

1992.

Masinde, Edwin
*Mashairi huru; uchambuzi wa dhamira*
94/207741

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote".

MASINDE EDWIN
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi wa kazi hii ya Chuo Kikuu".

BW. PETER M. MUGAMBI

# YALIYOMO

UKURASA

YALIYOMO ______ i

TABARUKU ______ iii

SHUKRANI ______ iv

MUHTASARI ______ vi

SURA YA KWANZA

1.1. Utangulizi ______ 1

1.2. Somo la Utafiti ______ 2

1.3. Madhumuni ya Utafiti ______ 3

1.4. Sababu za Kulichagua somo hili ______ 5

1.5. Upeo wa Tasnifu ______ 6

1.6. Yaliyoandikwa Kuhusu Somo Hili ______ 9

1.7. Msingi wa Nadharia ______ 14

1.8. Njia za Utafiti ______ 17

SURA YA PILI

2.1. Mazingira ya Msanii ______ 19

2.2. Wakati wa Ukoloni ______ 20

2.3. Kabla ya Azimio ______ 27

2.4. Azimio la Arusha na Baadaye ______ 29

2.5. Euphrase Kezilahabi ______ 31

2.6. Kulikoyela K. Kahigi ______ 36

2.7. Mugyabuso M. Mulokozi ______ 38

2.8. Kiishilio ______ 41

UKURASA

SURA YA TATU

3.1. Shairi "Mafahali Wapigana" 42
3.2. Shairi "Kuchambua Mchele" 46
3.3. Shairi "Hatumwoni" 50
3.4. Shairi "Kifo cha Mende Wekundu" 55
3.5. Shairi "Jua la Dhahabu" 58
3.6. Shairi "Damu Mpya Yatiririka" 61

SURA YA NNE

4.1. Shairi "Azimio" 65
4.2. Shairi "Ngoma ya Kimya" 69
4.3. Shairi "Afrika na Watu Wake" 73
4.4. Shairi "Uliza Wanaojua" 76
4.5. Shairi "Maombolezo ya Mtu Maskini" 79
4.6. Shairi "Enzi za Mapambano" 84
4.7. Shairi "Kiishilio" 90

SURA YA TANO

5.1. Shairi "Kisu Mkononi" 91
5.2. Shairi "Hadija" 93
5.3. Shairi "Hatima ya Kila Mwali" 95
5.4. Shairi "Wimbo Uliosahaulika" 98
5.5. Shairi "Habari Mpya" 102
5.6. Shairi "Karibu Ndani" 105
5.7. Shairi "Kiishilio" 113

SURA YA SITA

Hitimisho 115
Pendekezo kwa Utafiti Zaidi 123
Marejeleo 125
Faharasa 132

# TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa Babangu **Timona Masinde Wangila** na Mamangu **Esther Naliaka Amdavi** pamoja na wanangu wapenzi: **Austin, Jafred, Joy na Byrene** ambao ndio tegemeo langu la baadaye.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniongoza katika safari hii ngumu. Kuna mambo mengi mno ambayo nimeyashuhudia yakiwezekana hata wakati ambapo nilikuwa nimekwisha kata tamaa. Nimekinai kusema kwamba ufanisi wangu unatokana na nguvu pamoja na uwezo wake Jalia pekee kupitia kwa maombi yangu na ya aila yangu yenye mapenzi, na ambayo inamtambua Mola.

Sina budi vilevile kumtolea shukrani zisizo na kifani msimamizi wangu katika kazi hii, Bwana Peter Mugambi, ambaye bila mwongozo wake wenye busara pamoja na ushauri, nisingeweza kudhibiti bahari hii. Pia namshukuru Bwana Richard Wafula Makhanu kwa kujitolea kuchangia ufanisi wa kazi hii tokea mwanzo hadi mwisho wake. Msaada wake ulinipa moyo na hamasa kwa njia mbali mbali. Ushauri wake ni wa hekima

Shukrani nyingine za dhati ziwaendee ndugu Kahigi na Mulokozi kwa kunipa habari niliyohitaji kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana pamoja na kunitumia makala. Usaidizi wao umechangia ufanisi wa utafiti huu.

Ningependa pia kuwashukuru Profesa Ireri Mbaabu, Profesa Chacha Nyaigotti Chacha, Mwalimu Mutegi Mukobwa, Bwana Gwachi Mayaka na Bi. Catherine Ndungo ambao pia ushauri wao ulinifaa mno.

Ningependa vile vile kumshukuru mke wangu mpenzi, Bi. Alice Katila Wanyonyi ambaye alinisaidia kwa hali na mali pamoja na kunipa hima ya kuikamilisha kazi hii iliyo na vishindo vingi.

Nawashukuru ndugu zangu wapenzi kwa kunipa msukumo na hamasa licha ya kujitoa mhanga kugharamia masomo yangu ili nipate kupiga hatua. Nawashukuru mno kwa ukarimu wao. Bila msaada wao, nisingeweza kuikamilisha kazi hii.

Aidha, nawashukuru wanafunzi wenzangu ambao ni Bi. Judith Anne Mahero na Bi. Margaret Kamau kwa kuwa karibu nami. Mijadala yetu ilitupa nguvu ya kujisukuma na kutekeleza wajibu wetu kama ilivyopasa.

Mwisho kabisa, ningependa shukrani zangu ziwaendee Bi. Mary Makungu, Bi. Melody Nabutilu na Mary Khaemba kwa misaada yao ya vifaa pamoja na kukubali kunipigia chapa kazi hii. Bila msaada wao wa kujitolea kufanya kazi ya ziada, kazi hii isingefanikiwa na kufikia kiwango hiki.

Na kwa wengine wote ambao sikuweza kuwataja majina, isionekane kama ni mtovu wa shukrani. Nimefurahia michango yenu ya aina mbalimbali na kwenu nyote nawapa shukrani zangu za jumla. AHSANTENI.

## MUHTASARI

Tasnifu hii inashughulikia baadhi ya mashairi-huru ya watunzi watatu wa Tanzania. Inajadili dhamira na mtindo katika mashairi-huru ya Kiswahili, hususa jinsi dhamira zinavyoathiri uteuzi wa lugha katika kazi ya fasihi, na hasa ushairi.

Tumejaribu kuonyesha kwamba dhamira ya mtunzi na mtindo anaoutumia katika kutoa ujumbe wake ni vipengele vinavyotegemeana. Mtunzi atunga kutokana na tajriba aliyopata katika mazingira yake na lugha ndiyo njia aitumiayo kuyaeleza mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya kubuni.

Mazingira ya mwandishi katika ujumla wake huathiri uteuzi wake wa lugha na mitindo anayoitumia. Katika tasnifu hii, tumejaribu kuonyesha uwiano huu na kudhihirisha kwamba ijapokuwa ushairi-huru unatofautiana katika muundo wa nje na ushairi wa jadi, sifa za aina hizi mbili za ushairi ni sawa hasa tukizingatia umbo la ndani.

Aidha tumejaribu kuonyesha kuwa mtindo wa mwandishi huathiri uibushaji wa ujumbe wake.

Sura ya kwanza ni utangulizi ambao ni muhtasari wa mwongozo uliotusaidia katika utafiti na uchambuzi wa mashairi-huru tuliyochagua. Kati ya mambo ambayo yamejadiliwa katika sehemu hii ni somo la utafiti, madhumuni ya utafiti na msingi wa nadharia. Pia tumeeleza upeo wa tasnifu na kujadili kazi mbalimbali ambazo zimeshughulikia somo hili.

Sura ya pili inajadili mazingira walimotungia washairi tuliowachagua. Tunaafiki maoni ya Senkoro (1987:1) kwamba misingi na mikondo ya historia ya jamii huipa fasihi umbo kimaudhui na kifani pamoja na mwelekeo. Rene Wellek na Austin Warren (1949:94-95) wanasisitiza kauli hii kwa kusema:-

> Fasihi ni asasi ya kijamii inayotumia lugha; ni ubunifu wa kijamii. Vipengele vya fasihi kama taswira na mdundo vinatokana na jamii.

Wahakiki hawa wanachosisitiza ni kwamba fasihi haiibuki katika ombwe tupu. Hivyo, mhakiki wa fasihi hana budi kuzingatia mazingira ya kijamii ili kugundua vipengele vinavyoihuisha kazi fulani. Ni katika muktadha huu ambapo tunasisitiza kwamba mazingira ya kihistoria ya Tanzania, yawe ya kijamii, kiuchumi au kisiasa, yameathiri kazi za washairi hawa kidhamira na kimtindo.

Ushairi kama kazi ya sanaa utaeleweka na kutathminiwa vyema zaidi katika mazingira ya wakati maalum wa kihistoria. Pia fasihi hupata uhai wake kutokana na hali halisi za jamii. Hivyo basi katika sura hii, tumejadili mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya Watanzania katika vipindi viwili muhimu; wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni.

Tumejadili kipindi cha uhuru katika viwango viwili: Kabla na baada ya Azimio la Arusha la mwaka 1967. Lengo letu hapa ni kuonyesha jinsi matukio muhimu katika vipindi hivi yalivyoathiri mifumo ya kijamii ya Watanzania na kuathiri fasihi yao katika vipengele vyote.

Katika sura ya tatu, tumechambua mashairi yenye maudhui ya kisiasa. Tumeonyesha jinsi maudhui ya mtunzi yalivyosababisha uteuzi maalum wa lugha katika kuyaibusha.

Sura ya nne imejadili uchambuzi wa mashairi yenye maudhui ya uchumi. Katika sehemu hii, tumeonyesha jinsi uteuzi wa mtindo maalum wa mwandishi unavyosaidia kuibusha dhamira na jinsi dhamira pia inavyoathiri uteuzi huu.

Katika sura ya tano, tumechambua mashairi yenye maudhui ya maswala mengine ya kijamii kama vile ndoa, mapenzi, dini, utamaduni na falsafa kuhusu maisha. Tumeonyesha namna maudhui hayo yalivyojengwa kifani. Imedhihirika kwamba umbo la ndani la shairi ni muhimu katika kueleza maana yake.

Sura ya sita ni hitimisho. Sura hii ni muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu ambamo licha ya kueleza ugunduzi wa uchambuzi wetu, tumetoa kauli yetu juu ya ushairi-huru na mashairi-huru, na maeneo ambayo yanastahili kufanyiwa utafiti zaidi hapo baadaye.

# 1.0. SURA YA KWANZA

## 1.1. UTANGULIZI

Kwa zaidi ya miongo miwili sasa kumekuwepo na mgogoro katika Ushairi wa Kiswahili. Mgogoro huu una misingi yake katika kueleza maana ya Ushairi wa Kiswahili na umbo lake, na una pande kuu mbili. Upande mmoja wapo wanajadi ambao wanasisitiza kwamba vina na urari wa mizani ni uti na roho ya Ushairi wa Kiswahili milele. Baadhi yao ni kama vile K.A. Abeidi, S. Chiraghdin, J.M. Mayoka, S.A. Kandoro, S. Robert, A. Nabhany, A. Baruwa, A. Gibbe na D. Massamba.

Upande wa pili wapo wanamabadiliko wanaoeleza kwamba si lazima shairi liwe na vina au urari wa mizani ndipo liitwe shairi, na kwamba shairi halipaswi kuwa na umbo maalum lisilobadilika milele. Wao ni kama vile F. Topan, E. Kezilahabi, K.K. Kahigi, M.M. Mulokozi, E. Hussein, Kithaka wa Mberia miongoni mwa wengine.

Pande zote mbili zimetoa sababu mbalimbali kuunga mkono kauli zao. Kwa wanajadi, shairi la Kiswahili sharti lizingatie kanuni kama vina, mizani, idadi maalum ya mishororo katika kila ubeti na utoshelezi.

Wanamapinduzi kwa upande wao hawapingi kuwepo kwa ushairi unaofuata arudhi, bali wanasema kuwa shairi la Kiswahili halina budi kupanuka kimuundo. Chambilecho F.M. topan katika utangulizi wa E. Kezilahabi (1974:x):

> ... kitu kiitwacho shairi si lazima kiwe na muundo huo huo tu ndipo kistahili kuitwa hivyo... hadhi ya ushairi haitegemei muundo au umbo fulani bali yategemea yale yasemwayo na maneno ya shairi na vile yasemwavyo.

Tukizingatia mitazamo hii miwili inayopingana, ni muhimu kuchambua mashairi-huru tukitumia mojawapo ya nadharia za uhakiki wa fasihi ili tuweze kudhihirisha sifa zake. Ni kwa kufanya hivi ambapo tunaweza kutoa kauli iwapo kutozingatia arudhi za utunzi wa mashairi ya kimapokeo kunapunja au kukuza ushairi wa Kiswahili. Lengo hasa ni kusaidia kuamua iwapo sifa kuu za shairi ni umbo la nje au la ndani.

## 1.2. SOMO LA UTAFITI

Tasnifu hii imejishughulisha na uchambuzi wa dhamira na mtindo katika mashairi-huru. Mtindo ni jinsi msanii hutunga kazi na kuipa sura fulani kifani na kimaudhui, kwa lugha ambayo inaibusha kwa uzuri zaidi ujumbe anaotaka kuutoa.

Dhamira ya mwandishi hutokana na mazingira yake ambayo humpa msukumo wa kutunga shairi ili apate kutoa falsafa yake na hisia. Kwa hivyo, ni tokeo la mwingiliano kati ya mtu na mazingira yake na huonyesha namna anavyoyapa fasiri yake. Pia dhamira ya mwandishi huathiri mtindo wake kama vile mtindo anaoutumia husaidia kuibusha maudhui, dhamira na ujumbe anaounuia. Katika tasnifu hii tumechambua dhamira na mtindo kwa sababu kinacho-tofautisha mashairi ya wanajadi na yale ya wanamabadiliko

ni mtindo. Tumetumia mkabala huu kubainisha kuwa shairi hupata maana na umuhimu wake sio kutokana na umbo lake la nje tu bali pia matumizi ya lugha katika kujenga dhamira ya mwandishi.

Uchambuzi wa lugha ndio unaodhihirisha sifa za ndani za shairi na kuonyesha kwamba upekee wa shairi umo katika kunga za lugha zilizotumiwa. Katika kuchambua mtindo wa mashairi-huru, tumezingatia vipengele kama vile maana za ndani za maneno, taswira, sitiari, tanakali za sauti na takriri. Ingawa kunao watunzi wengi wa mashairi-huru, tumechagua baadhi tu ya mashairi ya Kezilahabi, Kahigi na Mulokozi kama kiwakilisho cha ushairi-huru. Tumechambua mashairi yenye maudhui yanayowakilisha vipengele mbalimbali vya maisha ya binadamu ili kutusaidia kutoa kauli jinsi uwiano wa dhamira na mtindo unaweza kutusaidia kuamua kwamba vipengele hivi viwili ndivyo vifanyavyo shairi kuitwa shairi.

## 1.3. MADHUMUNI YA UTAFITI

Tunachambua dhamira na mtindo katika mashairi-huru ili kudhihirisha mambo manne muhimu. Kwanza, kuonyesha kwamba kwa kuchambua mtindo katika mashairi tuliyochagua, tunabainisha kuwa ushairi-huru una sifa muhimu za ushairi, na kwamba dhamira na mtindo hasa ni

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

uti wa mgongo wa shairi na hudhihirika katika kazi moja.

Pili, kwamba mgogoro kuhusu maana ya shairi la Kiswahili haupaswi kuwepo iwapo wanaohusika, hasa wanajadi, wangetumia vigezo vinavyohusisha sifa zote za ushairi wala sio kipengele kimoja tu.

Tatu, kwamba shairi lina sifa za kimtindo za kipekee, na kuwa umbo la ndani la shairi ndilo muhimu katika kuainisha utanzu huu wa fasihi.

Mwisho, kwamba kauli ya wanajadi kuwa shairi la Kiswahili sharti lifuate arudhi za kimapokeo ni dufu na ni matokeo ya mtazamo finyu wa ushairi na fasihi kwa jumla. Tunapendekeza kwamba kaida za utunzi na za uchambuzi wa mashairi sharti zizingatie umbo la ndani na la nje. Pia mawazo haya ya kirasimi hayapaswi kumfunga mtunzi na mhakiki wa ushairi. Kama E. Kezilahabi anavyosema katika Topan (1977:59-60):

> ... Wataaalamu wetu wa mashairi wamesisitiza sana mambo madogo madogo ya mashairi. Mambo kama mizani, vina, kituo na kutosheleza si kiini cha shairi au maana ya shairi.

Tunakubaliana na madai yake kwamba kutilia mkazo arudhi katika ushairi kwa muda mrefu kumezuia uchambuzi wa kindani wenye kuzama katika mashairi yenyewe.

Hali kadhalika, kwa kuchambua mashairi-huru tunatarajia kuchangia mjadala kuhusu ushairi wa Kiswahili na kukuza uhakiki wake.

## 1.4. SABABU ZA KULICHAGUA SOMO HILI

Kama tulivyotangulia kusema, kumekuwepo na mgogoro katika ushairi wa Kiswahili kwa zaidi ya miongo miwili sasa. Mashairi-huru katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili yamerejelewa kwa sifa mbalimbali na wanajadi. Kwa mujibu wa msimamo wao, shairi halina budi kuwa na umbo maalum na ni lazima litimize masharti ya urari wa vina, ulinganifu wa mizani, kujitosheleza kwa kila ubeti, muwala au mtiririko mzuri wa habari na kuweza kuimbika. Mathalan, Mayoka (1986:X) asema:

> ... Tungo kama za Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi na wengineo watungao tungo tutumbi zisizokuwa na sanaa yoyote nimezitupa pembeni...

Wanajadi wanashikilia kwamba tungo zisizofuata au kutimiza arudhi hazina budi kupingwa kwa dhati kama dondoo hili linavyodhihirisha. Kwa upande mwingine, wanamabadiliko nao wanasema kuwa ushairi wa Kiswahili si lazima uwe na umbo maalum. Katika kutetea msimamo wao, kundi hili linasisitiza kwamba umbo la shairi halina budi kubadilika. Kwa mfano Kahigi na Mulokozi (1973) wameeleza kuwa utunzi wa mashairi hauna budi kuwa

na uhai kama ilivyo lugha yenyewe ya Kiswahili. Wanasisitiza kwamba utunzi wa mashairi hauna budi kubadilikabadilika na njia nyingine mpya za utunzi kuvumbuliwa.

Tumeamua kuchambua mashairi-huru kuonyesha kuwa haya mashairi pia hutungwa kwa sanaa na hutumia lugha yenye kuvuta masikio na fikra kama mashairi ya wanajadi, hata ingawa hayazingatii arudhi za ushairi wa mapokeo.

Vile vile tumeshughulikia dhamira na mtindo katika mashairi-huru kwa sababu hatuwezi kutenganisha lugha na ujumbe wa mwandishi katika kazi ya fasihi. Aidha, mtindo ndio hutofautisha utanzu wa ushairi na tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili.

Hali kadhalika, kauli, maoni na madai mengi ambayo yametolewa kuhusu nafasi ya ushairi-huru, hasa na wanajadi hayajikiti katika nadharia yoyote na hayaonyeshi vigezo maalum vinavyohusisha sifa zote za ushairi ili kutusaidia kuamua ni mashairi gani yanapaswa kuitwa mashairi halisi.

## 1.5. UPEO WA TASNIFU

Tasnifu hii inashughulikia mashairi-huru kumi na nane kutoka diwani nne za washairi watatu kutoka

Tanzania. Diwani hizo ni Kichomi (1974) na Karibu Ndani (1988) za Kezilahabi, na Malenga Wa Bara (1976) na Kunga Za Ushairi na Diwani Yetu (1982) za Kahigi na Mulokozi. Kazi hii imejikita katika uchambuzi wa dhamira na mtindo katika baadhi ya mashairi yaliyotungwa na Kezilahabi, Kahigi na Mulokozi katika diwani zao.

Tumejifunga katika uchambuzi wa mashairi kumi na nane ambayo tumechagua kulingana na maudhui kwa njia nasibu ili yawe viwakilishi vya mashairi mengine yanayobeba maudhui na fani sawa. Ingetubidi tuandike vitabu vingi ikiwa tungehakiki dhamira na mtindo katika mashairi-huru yote. Mashairi ambayo tumechagua yanaeleza vizuri maudhui na yana vipengele vingi vyenye kudhihirisha mtindo wa utunzi wa mashairi-huru.

Tumechagua mashairi ya watunzi hasa kutoka Tanzania kwa sababu ni huko ambako utanzu wa ushairi-huru umechapishwa zaidi. Pia tulijifunga kwenye mashairi-huru kwa kuwa mtindo wake mpya ndio uliosababisha mgogoro katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili. Aidha, si utafiti mwingi uliofanywa awali kuyahusu mashairi-huru.

Katika tasnifu, tumejadili kila shairi kwa kuangalia dhamira na mtindo kwa jinsi ambavyo mtindo husaidia kuibusha dhamira. Mtindo una vipengele vingi na tulizingatia maana za ndani za maneno, taswira, sitiari, tanakali za sauti na takriri. Istilahi kama zilivyotumiwa zimeelezwa katika faharasa.

Tumeyagawa mashairi hayo katika maudhui ya kisiasa, kiuchumi na maswala mengine ya kijamii kama vile ndoa, mapenzi, utamaduni, kifo na dini. Tumezingatia dhamira kuu zinazotokana na maudhui makuu ya shairi. Hii ndiyo orodha ya mashairi tutakayochambua:-


Siasa

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mafahali wapigana..... | Kichomi | uk. 5 |
| 2. | Kuchambua mchele...... | " | " 63 |
| 3. | Hatumwoni ........... | " | " 31 |
| 4. | Kifo cha Mende Wekundu | " | " 33 |
| 5. | Jua la Dhahabu........ | Malenga Wa Bara | uk. 17 |
| 6. | Damu Mpya Yatiririka.. | Kunga Za Ushairi | uk. 77 |

Uchumi

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Azimio ............... | Karibu Ndani | uk. 27 |
| 8. | Ngoma ya Kimya........ | " " | " 43 |
| 9. | Afrika na Watu Wake... | Kichomi | " 19 |
| 10. | Uliza Wanaojua........ | " | " 60 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Maombolezo Ya Mtu Maskini. | Malenga Wa Bara | uk. 15 |
| 12. | Enzi Za Mapambano......... | Kunga Za Ushairi | uk. 94 |

Maswala Mengine Ya Kijamii

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | Kisu Mkononi ............ | Kichomi | uk. 13 |
| 14. | Hadija.................. | " | uk. 22 |
| 15. | Karibu Ndani ........... | Karibu Ndani | uk. 34 |
| 16. | Hatima Ya Kila Mwali..... | Malenga Wa Bara | uk. 22 |
| 17. | Wimbo Uliosahaulika...... | " " " | uk. 87 |
| 18. | Habari Mpya............. | " " " | uk. 109 |

## 1.6. YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Swala la ushairi-huru limezusha mgogoro kuhusu umbo la shairi la Kiswahili. Katika uchunguzi na mapitio ya vitabu na majarida mbalimbali, si mengi ambayo yamewahi kufanywa kimtindo kuhusu ushairi-huru.. Hoja nyingi ni za kutajwa tu ambazo zahitaji kufanyiwa utafiti kama huu wetu.

Waandishi waliojishughulisha na aina hii ya utunzi wamekuwa wakitoa maoni tu kutetea hoja za wanajadi au wanamabadiliko. Hivi ni kusema kwamba swala hili halijashughulikiwa na wengi kwa nadharia muafaka.

Senkoro (1988) amechambua mashairi kadha wa kadha kwa kuzingatia mtindo wa watunzi pamoja na dhamira zao. Amefanya hivyo kwa kutazama baadhi ya mashairi ya wanajadi na wanamabadiliko. Kazi yake ilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu ilitupa mwelekeo. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu sisi tutashughulikia tu mashairi-huru. Pia, uhakiki wetu utaongozwa na nadharia ambayo itatuwezesha kuzingatia vipengele maalum.

S. Chiraghdin katika Nassir A. (1974:14) ameeleza kuhusu mashairi-huru kuwa:-

> ... Kwa Kiswahili, tungo zifuatazo mwendo huo mizani zake hazitakuwa na kichwa wala miguu. Pia kanuni zote za ushairi wa Kiswahili zitakuwa pindu pindu, vina havitajulikana mwanzo wala mwisho. Lugha yenyewe itakuwa chapwa au kuzidi.

Aendelea kueleza kwamba tungo hizi zikikubaliwa kuwa mashairi basi ushairi wa Kiswahili," utakuwa umeanguka kitakotako." Aonelea kuwa ushairi-huru unatokana na kule kufuata mitindo ya kigeni ya utunzi. Haelezi jinsi kutozingatia mizani na vina kutafanya lugha kuwa chapwa.

Mayoka J. (1986) aeleza kuwa vina na mizani ni utamaduni wa Waswahili na Wabantu kwa jumla. Asema kwamba kuacha matumizi yake kutakuwa ni kuharibu

utamaduni huo. Vile vile anasema kwamba shairi lisilokuwa na vina huwa limekiuka mipaka ya utamaduni ambao ndio mvyazi wa lugha. Hakufanya uchambuzi wowote kudhihirisha madai yake.

Topan F. (1973) amezungumzia umbuji wa Kezilahabi kwa kueleza kwamba hii ndiyo njia ya kwanza ya kuikuza fasihi ya Kiswahili kwa kuiletea mtindo mpya wa kutunga mashairi. Asisitiza kuwa hadhi ya ushairi haitegemei muundo au umbo fulani, bali yale yasemwayo na maneno ya shairi na jinsi yasemwavyo. Aeleza kwamba mawazo huletwa na mazingira, na mtu huchagua fani inayoambatana na uwezo wake. Maelezo haya kwamba shairi si lazima liwe na umbo maalum yanatilia nguvu somo la utafiti wetu, hasa lengo letu likiwa kuchambua iwapo umbo la nje tu ndilo muhimu katika ushairi wa Kiswahili.

Kahigi na Mulokozi (1982) wanaeleza kuwa miundo mipya katika ushairi wa Kiswahili ni nyongeza ya ile iliyopo na inabeba maudhui ya kileo. Wanasisitiza kwamba hali ya kushikilia vina na mizani inapingana kimsingi na kanuni ya sanaa ya uumbaji. Wanaeleza kwamba kanuni kuu katika utunzi wa mashairi ni uwiano kati ya fani na maudhui. Kwao, kanuni hii ndiyo inayoweza kuelezwa kuwa "roho" na "uti wa mgongo" wa ushairi na fasihi nzima kwa jumla. Maoni haya yamechangia somo letu la utafiti lenye lengo la kuchambua muumano wa fani na

ujumbe katika mashairi-huru. Mulokozi (1975) asema kwamba dhana kuwa ushairi wa Kiswahili una kanuni zisizobadilika za vina na mizani ina maana kwamba fasihi ya Kiswahili haikui licha ya mabadiliko ya hali za maisha na maudhui pia. Anasema kuwa maoni hayo yamepotoka kwa sababu kulingana na historia, ushairi wa Kiswahili, kama ulivyo ushairi mwingine wowote, umekuwa ukibadilika katika ujumbe na umbo kufuatana na mabadiliko ya wakati. Asema kuwa mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yataleta mabadiliko katika kila hali. Sifa hizi japo hazikuthibitishwa na Mulokozi kwa uchambuzi, ndizo lengo la uchambuzi wa kazi yetu ili kuzithibitisha.

Kezilahabi E. (1977) aeleza kwamba mshairi ana njia yake ya kutunga na kueleza mawazo yake kishairi. Asema kwamba jambo la kusisitiza mizani na vina limewafanya watu wengi kufikiri kwamba shairi bila mizani au vina si shairi. Aendelea kusema kwamba vitu hivi havina maana kama havikutumiwa vizuri ili kufanya shairi lieleweke vizuri zaidi. Kazi yetu itabainisha kwamba shairi ni zaidi ya umbile lake la nje.

Naye Kahigi K. (1975) aeleza kuwa mashairi ya Kiswahili yafaa kutazamwa kisayansi. Mtazamo huu ni wa kihalisi ambao huangalia historia nzima ya ushairi kwa jumla ukiihusisha na mabadiliko ya mfumo wa jamii, na ukizingatia dhima na maendeleo yake. Aeleza kuwa

mtazamo huu hukiangalia kitu kama kilivyo katika maisha, kama sehemu ya mchangamano wa mambo mengi katika maumbile, na kama kitu kinachobadilika kila wakati kutegemea mazingira ambayo yamekizunguka. Maelezo haya yana sifa ambazo ni muhimu katika somo letu la utafiti. Yeye ametoa maelezo ambayo tumeyashughulikia katika uchambuzi wetu.

Mberia K. (1990) aeleza kwamba inakubalika miongoni mwa wataalamu wa fasihi kuwa mojawapo ya sifa muhimu za fasihi, ukiwemo ushairi, ni kuwasilisha fikra, hisi na tajriba kwa njia ya kupendeza. Asema kwamba kupendeza huko kunatokana na urembo wa lugha ilivyotumiwa kisanaa. Aeleza kuwa vina na mizani si njia ya pekee ya kupambia shairi. Asisitiza kwamba kuna sifa nyingine ambazo huchangia urembo wa shairi na laweza kuvutia kwa sababu ya matumizi bora ya jazanda, tashibihi, tashihisi, balagha, chuku na kadhalika. Maelezo haya yana baadhi ya sifa za vipengele tulivyovitumia katika uchambuzi wetu.

Kwa hivyo, isipokuwa kazi iliyofanywa na Senkoro, wataalamu wengine wametoa tu maoni na kauli kuhusu mashairi-huru bila uchambuzi wowote. Hii ina maana kwamba kazi zao ni tofauti na yetu. Wao wanatoa maoni ya kijumla ambayo yanafaa kufanyiwa utafiti. Upungufu wa kazi zao ni ukosefu wa nadharia ya kuendeleza ithibati ya maoni haya katika uchambuzi. Kwa hivyo, kuna haja ya

kushughulikia mashairi-huru upya ili kufafanua zaidi hoja za wale wanaoyaunga mkono na kurekebisha hoja za wale wanaoyakaripia bila kuhusisha vigezo vya nadharia ya uchambuzi.

## 1.7. MSINGI WA NADHARIA

Nadharia ya uhakiki tutakayoitumia na ambayo tunaona kuwa itasadifu kwa utafiti wetu ni ile ya kimtindo. Nadharia hii ni muhimu tunapochunguza maudhui ya msanii pamoja na matumizi ya lugha ambayo ndiyo huibusha maudhui hayo.

Nadharia hii inaeleza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Kwayo, jinsi mtunzi atumiavyo lugha husaidia kutoa ujumbe wake kwa wasomaji au wasikilizaji. Hivyo, lugha huwa ndicho chombo muhimu cha mawasiliano katika jamii zote za wanadamu. Chambilecho Leech (1969:4):

> Kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na ufahamu mzuri wa lugha ambayo hutumiwa kuieleza. Ni muhimu kuelewa uhusiano ulioko kati ya lugha ya ushairi na ujumbe wa mwandishi.
> (Tafsiri yetu)

Wanamtindo husisitiza umuhimu wa lugha kama chombo tekelezi kinachosaidia katika kuelewa ujumbe au maudhui yaliyokusudiwa. Aidha, wanaeleza kuwa vipengele vya

kiisimu hutumika katika kueleza jinsi lugha hutumika. Mathalan, kutokana na mtindo wa kazi ya fasihi, inakuwa vigumu kubadili sentensi au hata neno katika kazi hiyo bila kuubadili mtindo wenyewe.

Nadharia hii husisitiza uwiano kati ya ujumbe na lugha. Ina misingi katika dhana kwamba lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwani hutumiwa katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi.

Kulingana na Leech (1969) kazi ya fasihi hukusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji au wasikilizaji. Aeleza kuwa nadharia hii ina vigezo vinavyotumiwa kuchambua kazi za kisanaa kwa kuangalia mitindo ya mwandishi. Utafiti wetu utatumia nadharia hii kama ilivyofafanuliwa na Leech kwamba:

a] Maudhui na dhamira, hushughulikia maoni au falsafa ya mtunzi juu ya jamii anayoizungumzia.

b] Muundo wa kazi za kubuni ndio hutumiwa na msanii kutoa ujumbe wake. Huu ni mkondo anaoufuata msanii katika kuifuma kazi yake. Kwa mfano, jinsi mtunzi alivyounganisha tukio moja na lingine, wazo moja na lingine, au ubeti na ubeti, ama msitari wa ubeti na mwingine.

c] Aina nyingine ya muundo hutokana na umbo na mpango wa kazi ya fasihi. Mathalan, katika ushairi wa Kiswahili, kunayo mashairi yenye miundo mbalimbali iainishwayo kulingana na idadi ya mistari katika kila ubeti.

Kuhusu muundo wa lugha, Leech aeleza kuwa kuna matumizi bayana na yenye ukiukaji. Katika matumizi bayana kuna usambamba, urari, tanakali za usemi, takriri na wizani au usuli. Katika ukiukaji, kuna tamathali na upotoshi sarufi maksudi.

Leech aeleza kuwa mshairi hutumia lugha "kiajabu", na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya lugha kisanaa. Kuyashadidia maelezo haya, Senkoro (1982) aeleza kwamba ushairi ni utanzu wa fasihi unaotumia mpangilio wa lugha mkato, ya picha, na yenye mapigo mahsusi katika kutoa maudhui. Kwa hivyo, vigezo vinavyotumiwa kuchambua na kubainisha shairi ni umbo lake pamoja na matumizi yake ya lugha. Aendelea kueleza kwamba ushairi hutumia lugha ya mkato yenye kueleza maudhui yake kimuhtasari, na aghalabu huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara. Hivyo, ushairi huwa hautumii lugha ya kinathari ya mjazo na mtiririko.

Nadharia hii itatusaidia kuchambua aina ya lugha iliyotumiwa katika mashairi-huru ili mtunzi ajieleze yeye

mwenyewe na kuathiri hadhira yake. Vipengele vya lugha tutakavyozingatia ni taswira, taashira, tamathali za usemi, takriri, misemo, na uhusiano kati ya maneno na maana yake. Ngara (1982) aeleza kwamba matumizi ya lugha katika kazi ya sanaa ni njia moja ya kuvuta hisi za hadhira. Kwa hivyo, tutachambua muundo wa lugha katika kujenga na kutoa ujumbe wa mwandishi.

Kutokana na maudhui, tutaonyesha dhamira za watunzi pamoja na kueleza jinsi maudhui hayo yalivyowiana na matumizi ya lugha. Kwa mujibu wa nadharia hii, tunapochambua maudhui, huwa pia tunachambua lugha iliyoyajenga. Kwa hivyo, hatuwezi kutenganisha lugha na maudhui tukaelewa ujumbe wa mtunzi.

Hivyo basi, nadharia hii itatuongoza vile ujumbe wa mtunzi na lugha yake hujengana na kuwiana katika ufanisi wa kazi ya ushairi.

## 1.8. NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu kwa kiasi kikubwa utafanywa katika maktaba. Tutasoma maandishi kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi katika utanzu wa ushairi. Pia, tutasoma maandishi kuhusu historia ya Tanzania hasa wakati wa ukoloni wa Mjerumani na Mwingereza. Vile vile tutajishughulisha na historia ya Tanzania baada ya uhuru.

Tutawahoji washairi Kahigi na Mulokozi juu ya maisha yao kuanzia utotoni hadi walipotunga mashairi tutakayochambua. Hoja zao kuhusu tajriba zao zitatusaidia kuelewa namna mazingira yalivyoathiri mtazamo wao wa maisha na utunzi pia. Maelezo ya tajriba za watunzi hawa yatasaidia kustawisha hoja za msingi wa dhamira zao pamoja na mkondo wa lugha walioufuata katika kutolea ujumbe wao.

Tutajadili mashairi tuliyochagua kama msingi wa utafiti wetu. Tutachunguza mambo yaongelewayo na jinsi yaongelewavyo. Hasa, tutachunguza ujumbe na jinsi lugha ilivyotumiwa kuutoa ujumbe huo wa mtunzi. Hapa, tutazingatia matumzi bayana na lugha nasibishi katika kila shairi.

Tutayashughulikia mashairi kulingana na maudhui. Kila shairi litatazamwa kwa kuzingatia vipengele vya yaliyomo na mtindo. Kisha uchanganuzi wa mashairi hayo utafanywa na kauli kutolewa kuambatana na aina hii ya utunzi kwa jumla kwa kurejelea ugunduzi utakaopatikana kuyahusu kama ithibati.

2.0. SURA YA PILI

## 2.1. MAZINGIRA YA MSANII

Mazingira ya kihistoria na kijamii huathiri utunzi wa msanii kifani na kimaudhui. Katika sura hii, tutajadili mazingira ya kihistoria na kijamii ya Tanzania wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Tutalazimika pia kurejelea hapa na pale mifumo ya kijamii kabla ya ukoloni kwa matarajio kwamba ulinganishi wa vipindi hivi vitatu katika historia ya Watanzania utatuwezesha kueleza kwa ukamilifu zaidi maudhui na dhamira za watunzi na hivyo kutuwezesha kuchambua mitindo iliyotumiwa katika miktadha ya maudhui na dhamira ya mashairi tunayoshughulikia.

Washairi wa Kiswahili kama walivyo wasanii wengine katika jamii yoyote ile ni zao la jamii hiyo. Mabadiliko yatokeayo katika nyanja zote za maisha kama vile ya kiuchumi, kisiasa na kijamii huwa hayakosi kamwe kuwaathiri. Athari hizi ndizo zinazompa mshairi hamu na ilihamu ya kuandika juu ya jambo linalomchochea au lililomkera moyo. Kwa hivyo, washairi wote ni zao la historia. Hali kadhalika, mshairi kama mwanajamii hawezi kuepuka kuathiriwa na mikinzano ya kitabaka ambayo inajidhihirisha katika jamii hiyo.

Tutashughulikia sera ya kikoloni na pia sera zilizobuniwa baada ya uhuru, na hali kadhalika katika

Azimio la Arusha la 1967. hali hizi ziliathiri ulimwengu wa watunzi kihulka.

Ukoloni ulivunja mifumo ya kijamii ya jadi ya Watazania. Baadhi ya sera na mifumo ya kikoloni ilihifadhiwa na kuathiri sera katika Tanzania huru. Azimio la Arusha lilidhamiria kurekebisha na kuondoa athari za kikoloni. Hii ni hatua muhimu sana katika historia ya Watanzania. Baadhi ya mashairi tuliyochagua yanazungumzia matumaini, kufaulu na kutofaulu kwa Azimio la Arusha.

Pia tutaangaza maisha ya watunzi wa mashairi tuliyochagua kuyafanyia utafiti. Hii ni kwa sababu tajriba za watunzi binafsi huathiri mielekeo yao. Kwa hivyo, historia ya maisha yao ni muhimu katika kueleza chimbuko la dhamira na mtindo katika usanii wao. Sura hii inadhamiria kuonyesha kwamba utunzi wao ni kioo cha jamii walimotungia.

## 2.2. WAKATI WA UKOLONI

Kipindi hiki katika historia ya siasa ya Afrika Mashariki kinaweza kuwekwa katika mihula mitatu maalum. Muhula wa kwanza, kama asemavyo Ogot, B.A. katika Anene (1966:487) kinaweza kuitwa 'Enzi ya Uhifadhi', hasa 1886-1914. Katika kipindi hiki, koloni za Afrika Mashariki

zilichukuliwa kama msingi wa fahari ya taifa na umuhimu wao ulithaminiwa na kutathminiwa katika mkabala wa Mng'ang'ano kisiasa baina ya mataifa makubwa. Uingereza na Ujerumani ni mataifa yaliyochukulia kwamba kazi yao ya kwanza ni kuhifadhi sehemu zao za utawala dhidi ya vitisho kutoka nje.

Muhula wa pili ulikwepo kati ya 1918 na 1939. Hiki ni kipindi baina ya vita vikuu viwili vya dunia. Muhula huu uliitwa 'Kipindi cha Udhamini'. Hiki ni kipindi kilichoshuhudia wakoloni wa Uingereza wakiwatumia Waafrika wateule katika utawala wao. Pia kulitokea uhusiano wa karibu kati ya mataifa ya Afrika Mashariki. Maongozi ya sera ya utawala wa Waingereza yalikuwa ya mabadiliko ya polepole au kulinda maslahi yao. Muhula wa tatu ulikuwepo kati ya 1945 na 1962, hasa baada ya vita vikuu vya pili vya dunia. Wakati huu unajulikana kama 'Kipindi Cha Uhuru'. Waafrika walipigania uhuru wao.

Katika kipindi cha ukoloni, wakoloni polepole walitumia hila zao ili kuwafanya Waafrika wapuuze na kudunisha utamaduni wa Kiafrika. Kwa upande mwingine wakoloni waliwafanya Waafrika kuutukuza utamaduni wa kikoloni, hivyo kuzamisha mirija ya kuendelea kuwategemea hadi sasa. Fanon (1963:218) asema kuwa:

30

Wasomi wa Kiafrika wameufanya
utamaduni wa Kizungu kuwa wao.

Pia utawala wa kikoloni uliathiri kwa njia mbalimbali utawala wa kiasili. Mathalan, jamii za kiasili zilizotawaliwa na Wafalme na ambazo hazikupinga utawala wa kikoloni zilihifadhi sehemu kubwa ya utawala huo.

Wakoloni pia walianzisha vituo vya kifalme mahali ambapo havikuwepo ili kuwatuza vibaraka wao wa Kiafrika. Kwa mfano, ufalme wa Sukuma Kaskazini mwa Tanzania.

Wale waliopinga utawala wa kikoloni kama vile Wahehe na Wanyamwezi walipoteza himaya zao. Gray, J.R. katika Anene (1966:484) atuarifu kuwa upinzani mkuu ulitokea kusini mwa Tanzania ambapo Wayao chini ya Abushiri, na Wahehe chini ya Mkwawa walipinga utawala wa kikoloni. Ni katika misingi hii ambapo, kwa mfano, Kezilahabi ametunga shairi 'Mkwava' kusifu juhudi za kizalendo za Mkwava wa Uhehe aliyepigania uhuru wa kujihami hadi dakika ya mwisho.

Athari nyingine ya utawala wa kikoloni ilikuwa kwamba watu wa asili tofauti walijumuishwa pamoja ili kurahisisha utawala wa kikoloni. Utawala huu ulibadili hali ya kuwaheshimu viongozi wa kiasili hadi kwa watawala wa kikoloni. Hali kama hii ilimomonyoa na

kuhujumu mamlaka ya utawala wa kiasili. Katika hali kama hii, watunzi walitunga mashairi kulilia utamaduni wa Kiafrika uliosahaulika. Mathalan, 'Wimbo Uliosahaulika' katika Malenga Wa Bara. Wanjala (1980:10) asema kwamba Mwafrika alipata usalama wake kutokana na asili yake.

Kulitokea sera mpya ya kikoloni ambapo kulikuwepo na korti ya wakoloni na nyingine ya Waafrika. Sheria za wakoloni zilikuwa kali kwa wenyeji na zilijaa maonevu ambapo baadhi ya Waafrika walihangaishwa bila sababu kwa kutumia polisi. Hali hii iliwaathiri watunzi kiasi kwamba walitunga mashairi kulalamikia uonevu na utawala wa kikatili. Kwa mfano, shairi 'Upepo Wa Wakati' katika Kichomi.

Viongozi Waafrika walioteuliwa katika utawala wa kikoloni walikuja kuwa vifaa vya utawala wa kikoloni. Walihitajika kutekeleza kila kitu kwa utii bila kusaili matendo yao. Kwa mfano, walikusanya kodi, kutoa chakula, kutoa watu wa kufanya kazi za shokoa na wengine kuingizwa katika jeshi la kikoloni. Machifu wa kikoloni waliathiri utaratibu wa kiasili kuhusu siasa, uchumi na hata maisha ya kijamii kwa jumla. Hawakuwa na huruma katika utekelezaji wao mradi tu waridhishe 'Mabwana' zao. Chambilecho Rodney (1972:72):

> ... walipatikana miongoni mwa Waafrika wale waliokengeuka kabisa na ambao walikuwa wamebobezwa.

Nchini Tanzania Wajerumani walitawala koloni yao kupitia Maakida waliotuzwa kwa kupewa sehemu ya kodi waliyokusanya, mshahara kila mwezi, kupewa mashamba na kuruhusiwa anasa fulani.

Jambo lingine kuhusu utawala wa Wajerumani ni unyonyaji kiuchumi. Walianzisha mashamba makubwa ya mimea kama vile pamba na mkonge. Pia walihimiza upataji wa wafanyikazi kwa urahisi na wakati mwingine kwa kuwalazimisha. Hawakuheshimu utu wa Mwafrika. Utawala wa kikoloni ulitwaa kwa nguvu mashamba ya Waafrika yenye rutuba na kuwalazimisha kwenda kwenye 'risavu' ambapo ardhi haikuwa na rutuba. Vilevile Waafrika wengi walilazimishwa kuwa maskwata katika ardhi yao ya zamani, licha ya kule kulazimishwa kulipa kodi na kuteswa. Jambo hili liliwashurutisha kwenda kufanya kazi katika mashamba ya Wazungu. Aidha, Waafrika walilazimishwa kufanya kazi ya ujenzi wa barabara na reli. Watunzi wanalalamikia hali kama hizi kupitia mashairi yao. Kwa mfano, shairi 'Maisha Yako' katika Kunga Za Ushairi ni taswira ya maisha ya mtu mnyonge wa tabaka la chini. Mfano mwingine ni shairi 'kauli ya Madhulumu.'

Kuletwa kwa pesa katika koloni la Tanganyika kulilazimisha Waafrika kutupilia mbali njia zao za kiasili za uchumi. Mishahara waliyopewa ilikuwa haba

mno. Hawangeweza kukimu au kukidhi mahitaji ya familia zao. Pesa ziliwashawishi vijana kughuria mijini na katika mashamba ya Wajerumani kutafuta kazi. Hali hii iliathiri mapato ya kilimo katika sehemu za mashambani. Pia, ubinafsi ulizuka na kuvunja maisha ya ujima ya Watanzania. Hali hii inabainika katika shairi 'Enzi Za Mapambano' katika Kunga Za ushairi.

Uchumi wa kikoloni uliwaathiri Waafrika kwa njia mbalimbali. Ulihimiza ubinafsi ambao unaambatana na unyonyaji usiojali utu. Ubepari ambao uliambatishwa na ulimbikizi wa mali kwa kuwanyonya waliozalisha mali hiyo ulizuka. Pia mabepari walitumia hila ili kuwa-zugazuga wanyonge na kuamwa jasho lao. Hali hii ya ubinafsi ilizusha wafanyikazi holela na ilivunja hali ya kiutu ambao Waafrika walikuwa nao katika ujima. Sera hii inadhihirika katika shairi 'Maombolezo ya Mtu Maskini' katika Malenga Wa Bara.

Kijamii, utamaduni wa Kiafria ulipuuzwa na kudunishwa. Shughuli zote za kimila zilipigwa marufuku. Kwa mfano, kuabudu miungu, kuoa wake wengi, elimu ya kienyeji, vyote vilipuuzwa kwa manufaa ya utamaduni wa Kizungu ambao ndio chanzo cha ukoloni mamboleo. Hii ndiyo sababu Wanjala (1980:15) asema kuwa:

> Mwafrika aliyesoma aliona vigumu kuhifadhi miiko na ibada zilizowaunganisha watu wake pamoja... alitenganishwa na sherehe za kuimba, kupiga ngoma...

Ni katika misingi hii ambapo watunzi wametunga kuufokea ukoloni mamboleo na hasa kuhimiza Uafrika asilia. Kwa mfano, shairi 'Hadithi Ya Kitoto' katika Kichomi laonyesha kuchukizwa kwa mshairi na hali halisi za Afrika leo.

Ogot, B.A. (1974) na Ilife, J. (1969) waeleza kuwa maasi ya Maji-Maji yaliyoanza 1905 yalikuwa utesi dhidi ya unyonyaji na unyang'anyaji wa Kijerumani. Maaasi haya yalisambaa katika sehemu nyingi. Japo yalizimwa mwaka 1907, yalikuwa na ishara ya kuwaunganisha Waafrika dhidi ya sera ya kikoloni yenye udhalimu na unyanyasaji. Funzo kwa wazalendo lilikuwa kuzinduka. Wakoloni, kama asemavyo Brett (1973:11), waliwavamia Waafrika, wakawafanya watumwa na kuwaweka chini ya utawala wao. Aidha, walinyakua mali yao kwa kuua, kutesa na kuhadaa. Aeleza kuwa ukoloni ndio uliozorotesha kustawi kwa Afrika nzima. Brett anasema kwamba ili maendeleo kupatikana, ni muhimu kujikomboa kutoka mfumo wa kibepari ili kuleta mfumo wa kijamaa. Ameumulika ubepari kama mnaso usio na utu na ambao unaharibu uhuru na kujitosheleza. Ni katika mtazamo

kama huu ambapo shairi 'Kifo Cha Mende Wekundu' katika Karibu Ndani lilitungwa. Ubepari, ubwanyenye na umwinyi vimeshutumiwa na kupigwa vita na watunzi. Waliopigania uhuru waliamini kuwa mifumo ya kikoloni ingebadilishwa uhuru upatikanapo.

## 2.3. KABLA YA AZIMIO

Tanzania ilipojipatia uhuru, ilikuwa muhimu kwamba iwe na sera mpya kisiasa, kijamii na kitamaduni ili malengo yake ya kupigania uhuru yafikiwe. Lakini sera za Tanzania huru kabla ya Azimio hazikufanikiwa.

Khatib (1987:37) asema kuwa kulikuwa na nguvu na mivutano ya kitabaka iliyokuwepo Tanzania Bara mara tu baada ya uhuru. Mathalan, walikuwepo wachache ambao waliitwa, 'naizesheni' au 'wabenzi' dhidi ya kundi kubwa la 'akina kabwela'. Mikinzano hii iliwavunja moyo 'akina kabwela' baada ya kuona uhuru walioupigania wote dhidi ya mkoloni ukiwa sasa unafaidiwa na wachache tu. Kwa sababu hii, washairi wametunga mashairi kueleza harakati za ujenzi wa jamii mpya na maana ya uhuru. Kwa mfano, shairi 'Vuteni Makasia' katika Malenga Wa Bara ni tahadhari inayotolewa kuhusu maana ya uhuru. Laonyesha kuwa uhuru si lelemama bali ni mapambano ya kuulinda, kuutetea na kuupalilia. Watunzi watahadharisha kuwa taifa lingeangamia kama lingesahau kuujenga uhuru kwenye misingi imara ya uchumi, utamaduni

na itikadi sahihi.

Pia, sera ya Tanzania-huru haikufanikiwa kutokana na sababu za nje. Kulikuwepo na nguvu nyingine, hasa katika 'medani' ya biashara ya kimataifa. Katika kipindi kifupi cha uhuru, serikali ilishindwa kuleta maendeleo ya haraka kwa watu wake baada ya kukosa misaada iliyotarajiwa kutoka nje. Aidha, bei ya mazao ya pamba, korosho na mkonge iliporomoka ghafla katika soko la kimataifa. Wakati huo, malighafi na vitu vilivyotengenezwa viwandani kutoka nje ambavyo vilihitajika vilikuwa ghali mno. Pia mabepari chwara, kama awaitavyo Khatib, walikuwa wakitia fora nchini kwa msaada wa mfumo wa ukoloni mamboleo. Aidha, ukoloni mamboleo ulizamisha mirija yake nchini katika kuhodhi faida ya vitegauchumi kama vile mabenki, viwanda, machimbo ya madini, mashamba makubwa na biashara ya nje na ndani.

Kilio cha Watanzania walioona kuwa nchi yao ilikuwa imesalitiwa kinabainika katika mashairi kama vile 'Mgomba' katika Kichomi. Mashairi ya aina hii yaonyesha tanzia ya uhuru uliosalitiwa na baadhi ya viongozi ambao walijitenga na kuwasahau wananchi waliopigania uhuru huo. Badala yake, walishiriki katika mfumo wa kinyonyaji wa ukoloni mamboleo kuzidi

kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini.

Mabadiliko yalitokea Zanzibar chini ya Abeid karume katika kipindi kifupi baada ya uhuru. Wananchi wa Zanzibar walishuhudia mapinduzi kisiwani. Vilevile, walikuwa tayari wamepatiwa huduma za bure za kiafya, elimu, maji na nyumba. Pia njia kuu za uchumi kama vile mabenki, viwanda, ardhi na mashamba zilikuwa mali ya umma. Mwelekeo wa sera wa itikadi ya serikali na chama chake cha Afro-Shirazi vilionyesha nia ya ujenzi wa taifa la usawa, haki na ujamaa.

## 2.4. AZIMIO LA ARUSHA NA BAADAYE

Baada ya Tanzania kujipatia uhuru wake mwaka wa 1961 kutoka kwa Uingereza, nchi hiyo ilifuata mfumo wa uchumi wa kibepari. Matokeo ya mfumo huo hayakuwafurahisha viongozi wa Tanzania,(Boesen (1977:14)). Chama Cha TANU kilichotawala Tanzania bara kilionelea kwamba kulikuwa na haja ya kuanzishwa siasa mpya ya ujamaa ambayo ingefuata maongozi tofauti na yale ya hapo awali.

Katika mwaka wa 1967, Azimio la Arusha lilitangazwa. Huo ukawa ndio mwanzo wa siasa mpya ya ujamaa. Siasa hiyo ilidhamiria kuwafanya watu waishi pamoja katika vijiji na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya

wote. Kadhalika, siasa hiyo ilikusudia kuleta usawa wa kiuchumi miongoni mwa wananchi na kuondoa kila aina ya unyonyaji na unyanyasaji. Kulikuwepo na matarajio makuu ya ufanisi kiuchumi, kisiasa na kitamaduni.

Pia, Azimio lilidhamiria kuonyesha kwamba uhuru unamaanisha kujitegemea. Kwa hivyo, maendeleo ya nchi huletwa na watu wake. Nguzo zake ni watu, mashamba, mashauri mema na uongozi bora. Elimu ambayo ingetolewa ingeenda sambamba na matakwa ya nchi pamoja na malengo ya kijamii. Ilinuiwa kujenga Tanzania huru yenye usawa na heshima kwa ubinadamu kwenye misingi ya Kiafrika. Chambilecho Rodney (1972:262):

> Muundo wa elimu katika mfumo wa elimu ya jadi ya Kiafrika ulikuwa unazifaa jamii hizo katika kupambana na mazingira yao. (Tafsiri yetu).

Hii ina maana kwamba elimu hiyo ilitokana na mfumo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii wa jamii husika. Ingezuia majaribu ya usodawi au usafihi ambao huwafanya walio-elimika kuwapuuza wale walio chini yao na kuwaona duni.

Hata hivyo, utekelezaji wa siasa hiyo haukuwa rahisi. Kulikuwa na matatizo mengi yaliyoukumba mpango huo. Mathalan, Boesen (1977:64) asema kuwa baadhi

ya viongozi mikoani hawakujua malengo ya siasa hiyo. Aidha, viongozi hao hawakuchaguliwa kwa madhumuni ya kutekeleza mpango huo. Kwa hivyo, uongozi katika utekelezaji wa siasa ya ujamaa waonekana kutokuwa na mwelekeo mzuri.

Tangu kutangazwa Azimio la Arusha, watunzi wamelizungumzia katika nyanja mbalimbali za maisha. Washairi tunaozungumzia katika tasnifu hii ni wapevu na ambao walipitia awamu tatu za mabadiliko ya kisiasa tokea wakati wa kudai uhuru, baada ya kupata uhuru na baada ya kuzaliwa Azimio la Arusha.

Tatizo kuu katika Tanzania huru lilikuwa kule kuwepo kwa matabaka ya wanyonyaji na wanaonyonywa. Hali hii ilisababisha Azimio la Arusha kama tulivyo-eleza, kisha kukawa na shangwe katika kukaribisha Azimio la Arusha, halafu kukatokea udhaifu fulani katika harakati za utekelezaji wa itikadi ya siasa ya ujamaa pamoja na kuzihusisha sehemu muhimu za uchumi wa nchi. Kwa hivyo, ubepari uliendelea, unyonyaji na unyanyasaji pia. Hivyo, kuna kutoridhika na kukata tamaa. K.m. shairi 'Mgomba' katika <u>Kichomi.</u>

## 2.5. EUPHRASE KEZILAHABI

Kezilahabi alizaliwa katika kijiji cha Namagondo huko Ukerewe katika mkoa wa Mwanza, Tanzania mnamo

tarehe 13-4-1944. Alielimishwa katika shule ya seminari ya kikatoliki ya Nyagezi kutoka darasa la nne hadi la kumi na nne. Alijifunza falsafa za kinadhifu za dini, lugha ya kilatini na masomo mengine.

Baada ya kidato cha sita, alitoka seminari. Kisha wazazi wake walimshauri asifuate mwenendo wa kakaye ambaye tayari alikuwa padri. Aliingia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alisomea ualimu, lugha na fasihi. Alijipatia shahada ya B.A. mwaka wa 1970 na kwenda kufundisha katika shule ya sekondari ya Mzumbe na baadaye huko Mwanza mwaka wa 1971.

Baada ya muda, Kezilahabi alijiunga na Chuo Kikuu cha Wisconsin, U.S.A. ambapo alifuzu kwa shahada za M.A. na Ph.D. Tasnifu yake ilihusu riwaya za Shaaban Robert. Vile vile, alisoma fasihi ya Kiafrika na fasihi linganishi. Kisha alijiunga na idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Baba yake alikuwa mkuu wa kijiji ambaye alikuwa akitoa ushauri na kuamua kesi zilizohusu maisha ya wanakijiji, mbali na kufanya juhudi za kuleta maendeleo kijijini. Kazi muhimu ya kijijini mwao ilikuwa ukulima na ufugaji. Hali hii imemuathiri kiasi kwamba hujishughulisha na maisha ya shamba

katika uandishi wake.

Pia, maisha ya mwanadamu ni swala ambalo mwandishi huyu hujishughulisha nalo katika kazi zake za sanaa. Analiangalia katika mkabala wa mtu binafsi na wa jamii. Anamchunguza mtu katika hatua zote kama vile kuzaliwa, ujana, malezi, ndoa, uzee na kifo huku akitathmini fumbo lililoko katika kila mojawapo ya hatua hizi maishani.

Kezilahabi ameshughulikia maswala ya utamaushi, falsafa ambayo imemwathiri sana katika mtazamo wake wa maisha na uandishi wake. Mengi kuhusu falsafa hii alijifunza akiwa chuoni ambapo aling'amua kwamba jamii ina vikwazo, miiko na masharti yake yanayoiongoza na kuidumisha. Maswala yajitokezayo katika utunzi wake ni:-

i) Maisha hasa ni nini na yana maana gani?

ii) Ni nini hasa umuhimu wa maisha ya binadamu ikiwa hatima yake ni kifo?

iii) Maana ya uhuru ni nini, mtu binafsi ana uhuru gani na ipi mipaka ya uhuru huo?

iv) Kuna uhusiano gani kati ya mwanajamii na jamii yake?

v) Tafsiri ya mapenzi ni ipi na kuna uhusiano gani kati ya mwanamume na mwanamke kimwili na kindoa?

vi) Shida za watu wenye madaraka pamoja na upotofu.

vii) Mikinzano na migogoro ya kitamaduni baina ya ujadi unaofifia na usasa unaochomoza vijijini na mijini.

viii) Malezi ya watoto na matokeo yake.

ix) Uzazi na ugumba.

x) Elimu ya kimagharibi na athari zake kwa msomi.

Ni katika misingi hii ambapo alitunga mashairi ambayo baadhi yake tumechagua kuyachambua kubainisha ujumbe huo. Katika utunzi wake, Kezilahabi amebainisha kwamba mazingira ya kijamii ndiyo yanayoiunda hulka na shaksia ya mtu. Pia amegusia athari zilizoletwa na elimu ya kikoloni kuwa zenye kutumikia uchumi wa kibepari, kujisahau, kujidharau, kutamani uzungu, kujichukia na kuchukia chochote cha Kiafrika, na kumfanya Mwafrika mtumwa. Kuhusu swala hili la kukengeuka, Ngugi wa Thiong'o (1977:14) asema:-

> Mfumo wa kikoloni ulizaa aina ya elimu ambayo ilikuza utii, kujichukia na kutojiamini. Uliwazaa watu ambao waling'olewa kutokana na asili zao, na ndio mwanzo wa uozo wa wasomi waliojitenga na jamii zao.

Hali kadhalika, Kezilahabi anashughulikia swala la maana ya maisha katika utunzi wake. Ameyadhihirisha kama adhabu kali, yasiyo na furaha ila huzuni tu. Ameonyesha kwamba binadamu hana chochote cha kujivunia. Maisha ya binadamu yamejaa ghururi. Kwa hivyo, hayatakuwa shwari. Ahimiza kwamba maisha ni kitu ambacho mwanadamu hapaswi kukitegemea kwani ni kitu kisicho na maana. Kuhusu uhuru wa mtu binafsi katika jamii, Kezilahabi katika vitabu vyake ameonyesha kwamba mtu hana uhuru wa kufanya alitakalo, ikiwa analotaka kulifanya linapingana na matakwa au matarajio ya jamii yake. Matakwa ya mtu binafsi yanapofarikiana na yale ya jamii, mtu binafsi ndiye anayeumia. Pia ameonyesha kwamba mtu binafsi hawi huru pale matakwa yake yanapopingana na yale ya jamii yake.

Kuhusu furaha, mwandishi ameonyesha kwamba mwanadamu hawezi kupata furaha kamilifu hapa duniani. Kwa sababu hiyo, awashauri wanadamu kuyaishi maisha kama yalivyo kwani kuitafuta furaha ni sawa na kupoteza wakati. Ni kujitafutia maangamizi.

Mwandishi vilevile ameshughulikia swala la ndoa ambapo ameonyesha kwamba hakuna matumaini katika ndoa za wasomi. Amebainisha kwamba ndoa za kiasili zilifaulu kwa sababu ya heshima, furaha na kukidhiana haja. Anasuta kule kuandama sera ya maisha ya kigeni ambapo hapana uaminifu katika maisha ya ndoa. Kuna uozo mwingi.

Kuhusu jambo hili, Adagala (1980:35) asema:

> Umalaya aghalabu huwa ni zao la mfumo wa kibepari. Wanawake ambao hawana njia nyingine ya kiuchumi hujiuza ili wajipatie pesa za kuendesha maisha yao.

Katika utunzi wake, mwandishi anasuta malezi mabaya ya wazazi. Vilevile ameonyesha kuwa dini imeibuka kutokana na kushindwa kwa mwanadamu kupata furaha duniani.

## 2.6. KULIKOYELA K. KAHIGI

Kahigi alizaliwa tarehe 4-8-1950 katika Utemi wa Busambilo, mpakani mwa Kahama na Biharamalo. Wazazi wake walikuwa, na bado ni wakulima.

Alianza shule ya msingi mwaka 1959 katika shule ya msingi ya Iyengamulilo ambapo alisoma hadi darasa la nne mwaka 1962. Kishapo akajiunga na shule ya kati ya Rubondo hadi 1966. Mwaka 1967 alijiunga na shule ya sekondari ya Kahororo ambapo alisoma hadi 1970. Katika mwaka ya 1971-72 alisoma kidato cha tano na sita katika shule ya Mkwawa. Katika miaka ya 1973-1976 alikuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alikosomea shahada katika Isimu, Fasihi, Masomo ya Maendeleo na Elimu. Alihitimu vizuri katika daraja la kwanza na kati ya 1976-1977,

alisomea shahada ya M.A. katika isimu. Mwaka wa 1988 alifuzu shahada ya Ph.D. katika isimu katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Michingan, East Lansing, Marekani.

Alianza kuandika mashairi, kwanza katika Kiingereza, halafu katika Kiswahili alipokuwa katika shule ya sekondari mnamo mwaka wa 1968. Mwaka wa 1969, aliandika tamthilia, Lengo Letu akishirikiana na A. Ngemera, na Lufalabamu Banobi. Aliirekebisha mwaka 1972 na kuiita Mwanzo Wa Tufani iliyochapishwa mwaka wa 1975.

Katika mwaka wa 1970 Kahigi alishirikiana na M.M. Mulokozi katika kuandaa muswada wa Mashairi ya Kisasa. Mashairi haya yalitolewa kitabu mwaka wa 1973. Katika mwaka wa 1971, yeye tena na Mulokozi waliandaa muswada wa mashairi ambao baadaye uliitwa Malenga Wa Bara.

Katika kipindi cha kati ya mwaka wa 1973 na 1976, Kahigi aliandika mashairi mengi yaliyochapishwa katika magazeti ya Uhuru, Mzalendo na Ngurumo. Pia, aliandika makala juu ya "Ushairi ni Nini?" yaliyotolewa katika Uhuru.

Mwaka 1978, Kahigi na Mulokozi walikusanya mashairi yao na kuandaa kitabu ambacho walikiita Kunga Za Ushairi na Diwani Yetu kilichochapishwa mwaka wa 1982.

Mnamo mwaka 1989, Kahigi aliwasilisha muswada wa mashairi uitwao "MIVUTANO" ambao bado haujachapishwa.

Kahigi pia ni mhariri wa magazeti na majarida. Mathalan, amekuwa mhariri mkuu wa majarida mbalimbali kama vile Kioo cha Lugha na Zinduko. Aidha, ameandika makala kadhaa ambazo zimechapishwa katika majarida mbalimbali.

## 2.7. MUGYABUSO MLINZI MULOKOZI

Mulokozi alizaliwa tarehe 7-6-1950 kule Bukoba, Tanzania. Kama vile mwenyewe alivyoniarifu mnamo tarehe 23-1-1992, alizaliwa katika familia maskini ambapo alikumbwa na matatizo mengi zaidi. Mathalan, ilibidi ng'ombe wauzwe, shamba na hata kuku ili kugharamia masomo yake.

Baada ya masomo ya shule za msingi, alijiunga na shule ya Taifa ya Iringa ambapo alimaliza masomo ya sekondari katika kidato cha sita mwaka 1971. Kidato chao cha tano kilikuwa na wanafunzi wenye hamasa akiwemo Senkoro huku wakifunzwa na Kezilahabi. Alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alifuzu katika shahada ya fani na elimu mwaka wa 1975. Kisha alifuzu shahada ya pili (M.A.) mwaka wa 1982 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baadaye shahada

ya Ph.D. mnamo 1987 katika Chuo hicho.

Ana ujuzi wa uhariri wa miaka mingi wa majarida ya MULIKA na KISWAHILI baada ya kuhudhuria mafunzo ya uhariri kule Liber Grafiska A.B., Sweden mwaka wa 1977. Pia amekuwa mkuu wa utafiti na vilevile mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, amekuwa mpangaji na mwenezaji habari katika Magazeti kama vile Uhuru. Hali kadhalika amekuwa mwanakamati wa kamati kuu la waandishi Tanzania na mshiriki wa vipindi vya radio kuhusu mijadala ya fasihi. Pia ameandika tahakiki nyingi kuhusu vitabu kama vile Kichomi, Al-Inkishafi, Siku ya Watenzi Wote, Kinjeketile, Dunia Uwanja wa Fujo miongoni mwa vingine. Isitoshe, Mulokozi ametoa maandishi mbalimbali kama vile maendeleo ya fasihi, ushairi na ukasuku, mashairi ya kisasa na utafiti wa fasihi simulizi. Aidha, amefanya utafiti kwingi. Mathalan, kule Mainz, U.S.A. New York na Brown University.

Kazi ambazo amewahi kutunga ni pamoja na Siri ya Bwanyenye (1976), Mashairi ya Kisasa (1973), Mukwava wa Uhehe (1979) na Mapinduzi ya Nyumbani. Maswala yajitokezayo katika utunzi wake ni:

(i) Ndoa. Anashughulikia uhusiano kati ya mume na mke, na haja ya kuwa na usawa baina yao na kuheshimiana katika ndoa

(ii) Unafiki wa mabwanyenye nchini Tanzania miaka ya 1970 (mwanzoni) baada ya utaifishaji wa majumba na viwanda. Vibwanyenye waliokuwa serikalini ilibidi watumie mbinu za unafiki ili waonekane ni wajamaa.

(iii) Ukoloni mamboleo.

(iv) Falsafa ya maisha.

(v) Ukombozi na Ujenzi wa taifa jipya.

(vi) Matatizo ya vijana na maana ya kukua kwa mtoto.

(vii) Jukumu la vijana katika ukombozi

(viii) Ujasiri na kujitoa muhanga.

Dhamira hizi zinajitokeza katika mashairi yake. Nilipowahoji Kahigi na Mulokozi, nilifahamikiwa kwamba watunzi hawa walikubaliana kwingi kama wasomi. Waliniarifu kwamba walipokuwa shuleni, walipata msukumo wa utunzi kutokana na vyama vya ushairi vilivyokuwepo. Hali kadhalika, waliathiriwa na mapinduzi ya kijumuiya katika dunia nzima. Kwa hivyo mashairi yao ni kioo cha tajriba zao zikiwemo mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo yaliwazunguka. Utunzi wao umejikita katika kila nyanja ya maisha.

Kuhusu fani yao, sitiari walizotumia 'zilichotwa'

moja kwa moja kutokana na mazingira yao. Walikuwa vijana ambao hisia zao zilijaa ari na matumaini. Walitaka Tanzania kufanikiwa kimaendeleo. Kwa hivyo, maendeleo na mabadiliko ya kijamii na kimazingira yaliathiri utunzi wao kifani na kimaudhui.

## 2.8. KIISHILIO

Mazingira ya waandishi hawa, kukua na kupanuka kwa elimu, hali ya uchumi na siasa, vyote vimechangia mtazamo wao wa maisha pamoja na utunzi wao. Mathalan, itadhihirika kwamba utunzi wao unazingatia hali halisi za watu wao kama vile umaskini. Pia walikuwa na matumaini makubwa katika mapinduzi ya Azimio la Arusha ambalo walitaka lifanikiwe. Kulikuwepo hasa na mapinduzi ya kitamaduni na kisiasa ambapo ukoloni ulikuwa umevunja mifumo ya kijamii ya jadi. Vilevile baadhi ya sera na mifumo ya kikoloni ilikuwa imehifadhiwa na kuathiri sera katika Tanzania huru. Kwa hivyo, utunzi wa washairi hawa ni mfano wa mabadiliko na maendeleo ambayo hutokea katika jamii za ulimwengu.

3.0. SURA YA TATU

## SIASA

### 3.1. SHAIRI: "MAFAHALI WAPIGANA"

Shairi hili limetungwa juu ya uongozi wa nchi ya Tanzania. Kezilahabi anazungumzia mfumo wa kibepari unaojitokeza katika umbo la ukoloni mamboleo. Katika shairi hili mtunzi aonyesha mzozo baina ya viongozi huku raia wakishangilia bila kung'amua kinachoendelea.

Hili ni shairi ambalo kichwa chake ni jazanda. Katika ubeti wa kwanza, mtunzi asema kwamba "Mafahali wenye matumbo wanapigana." Hii ni jazanda inayobeba ujumbe kwamba watu wenye madaraka wanazozana. Kwa kawaida, watu ambao hurejelewa kama "Mafahali" ni wale wenye uwezo mkubwa katika jamii. "Matumbo" hapa ni taashira ya mali. Mazingira yaliyomzunguka na ambayo pia yalimkuza mtunzi ni ya mfumo wa kibepari. Kwa hivyo, wanachozozania hawa viongozi ni mali. Kunao mvutano juu ya suala la ulimbikizaji wa mali. Mwandishi ameweka mkazo kwa kukariri kwamba wanapigana chini, chini, chini zaidi mpaka vichwa vyao vinagusana. Takriri hii ina maana kwamba mvutano huo ulikuwa wa kutoana jasho. Chambilecho Shivji (1974:37):

> Mvutano mkali ni baina ya viongozi wanamapinduzi na wale ambao maslahi yao ya kiuchumi yanahatarishwa na juhudi za maongozi mapya ya kijamaa...

Mtunzi anaendelea kueleza kwamba" Halafu watazamaji wakondefu wanaanza kupiga kelele." Jazanda hii imetumiwa kuwadhihaki raia wanaoshangilia viongozi ambao hawana haja na maslahi ya umma. Hii ni ishara kwamba raia hawakujua hasa kilichokuwa kikiendelea. Vilevile ukondefu wao ni taashira kwamba hali yao ni mbaya. Wanasononeka kutokana na viongozi ambao wamejitenga na wanaoshirikiana na wakoloni wanyonyaji kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa matabaka ya chini. Hii ni tanzia ya uhuru uliosalitiwa na baadhi ya viongozi ambao wamejitenga na kuwasahau wananchi waliopigania uhuru huo. Uwezo wa wananchi ni duni mbele ya mafahali wenye matumbo. Wananyanyaswa sana ndiposa wamekonda. Hawawezi kubadili mfumo huo kulingana na hali yao duni. Hii ndiyo sababu mwandishi asema kwamba pole pole hawaoni kitu.

Taswira ya vumbi hewani na machoni inaonyesha ukungu unaowaziba raia macho ili wasiweze kuona na kuelewa kinachoendelea katika jumuiya yao. Viongozi hao wana hila zisizofahamika kwa umma. Kezilahabi aonyesha kwamba baada ya vumbi kuisha, mshindwa alikuwa amekwisha kimbia, huku mshindi juu ya kichuguu amekaa akionyesha kidole kimoja sasa. Hii ina maana kuwa baada ya mzozano ambao ulisikika kwa mbali pamoja na kushuhudiwa na wananchi kwisha, mshindi alikuwa ameshikilia uongozi wa nchi huku akionyesha ishara

ya umoja. Mwandishi anabeza viongozi kama hao ambao wanawapuuza wananchi katika kuunda sera ya uongozi na haki kisiasa na kiuchumi huku matamshi yao yamejaa "Uhuru," "Demokrasia," "Umoja" na "Ushirikiano." Anabainisha kwamba matamshi kama hayo ni ya bandia tupu. Pia "kichuguu" hujengwa kwa ushirikiano wa 'mchwa'. jazanda hii ina maana kwamba taifa hujengwa kwa ushirikiano wa wananchi. Lakini mwandishi asema kwamba "mchwa ndio askari." Jazanda hii ina maana kwamba askari ndio hushirikiana na huyo kiongozi katika ujenzi wa taifa. Hii ni kinaya kwa kuwa mwandishi anamdhihaki yule kiongozi. Askari ni taashira ya udhaifu wa uongozi wa aliyefikiriwa kuwa "fahali." Kwa hivyo, suala hili linashikamana na dhuluma itokanayo na utawala wa kimabavu ambapo wanyonge wanalazimishwa kukubali sera hiyo huku wakibebeshwa mizigo mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa manufaa ya viongozi wenyewe. Kwa hivyo, umoja na ujinga ni vitu vilivyo-unganishwa pamoja.

Katika ubeti wa pili, mwandishi aeleza kwamba kilikuwa kivumbi. Hii ina maana kwamba jambo hili lilitokea kitambo. Anatumia tanakali ya usemi kwamba sasa pahali hapo pametulia tuli. "Kutulia" hapa kunaashiria kimya chenye mshindo. Makelele ya kutafuta kiongozi yalikuwa mazungumzo kisiasa, lakini sasa uhuru

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

wa kusema haupo. Hii ndiyo sababu mwandishi asema kwamba "kutembeza midomo ndio kusikika, kunyamaza ndio basi kudhamiwa." Kwa jinsi ambavyo kuna udhaifu uongozini, kutembeza midomo kunashukiwa kuwa ni kama kuikashifu serikali. Vilevile, kunyamaza ni balaa kwani watu bado watatuhumiwa. Kwa hivyo, watu hawana uhuru hata kidogo. Hali kadhalika, "Patulivu! Patulivu! Patulivu! Kweli!" ni msisitizo anaotumia mwandishi kama kejeli kuonyesha kwamba hapana demokrasia bali ni utulivu unaosetiri maangamizi, dhuluma na utawala wa kiimla.

Katika ubeti wa mwisho, Kezilahabi ametumia tashbihi kueleza wito wa viongozi wanaotaka wananchi washirikiane nao kujenga taifa. Anasema:

> Basi kama mchwa
> Tujenge kichuguu
> Kama mchwa tuungane
> na kuulainisha udongo.

Anakariri umuhimu wa kushirikiana kama mchwa. Kulainisha udongo ni jazanda inayoeleza dhana ya vitu ambavyo ni nguzo ya taifa. Mchwa hulainisha udongo ambao hutumiwa katika kujenga kichuguu. Kwa hivyo, ni kinaya ambapo mwandishi anasuta unafiki wa viongozi wasiowazingatia wananchi katika maamuzi yoyote muhimu yanayohusu ujenzi wa taifa. Hii ndiyo sababu anatumia takriri na nidaa kuonyesha shaka yake juu ya hali hiyo. Anasema:

Patulivu! Patulivu! Patulivu!
Lakini! Lakini! Lakini!

Dondoo hili laonyesha kwamba kuna dhuluma, lakini matumaini yapo. Kuna siku ambapo hali hiyo haitaweza kustahimilika tena.

3.2. SHAIRI: "KUCHAMBUA MCHELE"

Shairi hili laeleza jitihada za Watanzania katika ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa. Kezilahabi aonyesha kwamba kazi hii ni ngumu na inahitaji tahadhari kubwa. Pia aonyesha kuwa mafanikio yake ni haba mno.

Katika ubeti wa kwanza, mwandishi asema kwamba habari zilifika kutoka Arusha. Usemi huu una maana kwamba tangazo liliwafikia watu kutoka Arusha. Tangazo hili linahusu Azimio la Arusha la 1967. Tamko hili lamaanisha kuwa wananchi hawakuzingatiwa katika mijadala iliyozaa Azimio hili. Mshairi aeleza kwamba walianza kuchambua mchele wa ujamaa. Jazanda hii inamaanisha kuwa walianza kufanya juhudi za kuondolea mbali mfumo wa kinyonyaji wa kibepari. Ukoloni ulikuwa umevunja mifumo ya ujima ya kijadi. Baadhi ya sera na mifumo ya kikoloni ilihifadhiwa katika Tanzania huru. Kwa hivyo Azimio lilidhamiria kurekebisha na kuondoa athari za kikoloni ili kuwepo sera ya kijamaa. Kwa hivyo kuchambua mchele wa ujamaa ni taashira ya harakati za Watazania za

kuufyeka unyonyaji na unyanyasaji. Ni jitihada za kuchunguza welekeo wa kufaa wa kijamaa.

Kezilahabi aeleza kwamba walifanya kazi hiyo macho mbele, macho pembeni, wakitoa mchanga. Takriri hii ya 'macho' inaeleza dhana kuwa walichukua hadhari kubwa katika kuandaa sera ya ujamaa. Kwa kawaida kabla mchele haujapikwa, mchanga na chenga hutolewa ili ufae na uwe safi. Kwa hivyo, mwandishi ametumia jazanda ya mchanga kama taswira inayoonyesha 'uchafu' uliojikita katika jamii ya Watanzania wakati huo. Mwandishi anashutumu mfumo wa kibepari ambao uliruhusu unyonyaji na ukandamizaji wa watu. Aidha, mwandishi aeleza kwamba walifanya kaburi dogo la mchanga. Taswira hii inamaanisha kuwa waliyazika maovu ambayo yangezuia mfumo wa ujamaa kushamiri. Watanzania waliazimia kuvunjilia mbali vikwazo vya ujamaa. kwa hivyo, "kaburi dogo" ni ishara ya maovu ambayo yaliwekwa pamoja na kuwa mengi mno. Kaburi huwa mahali pa kuzika mtu aliyekufa na ambaye hatakikani tena miongoni mwa walio hai. Hivyo basi mbinu hii inaeleza harakati za kufyeka ubepari wa kikoloni na kuuzika katika kaburi la sahau.

Katika ubeti wa pili, mwandishi asema kuwa walianza kutoa chenga mojamoja. Taswira hii inaeleza dhana kwamba walitoa vikwazo vingine katika sera ya ujamaa

ambao ni mfumo usio na unyonyaji kati ya mtu na mtu. Kwa hivyo, 'chenga' ni vikwazo vilivyojitokeza katika harakati hizo. Mwandishi asisitiza kwamba vikwazo viliondolewa kimoja baada ya kingine. Mwandishi anatumia tashibihi kwamba vidole vilifanya kazi kama cherehani. Hii inaonyesha kwamba walifanya kazi hiyo hatua kwa hatua na kwa bidii. Anaeleza kwamba walifanya kazi usiku na mchana, macho yakauma. Usemi huu una maana kuwa hawakupumzika katika harakati hizo zenye uzingatifu mwingi. Kisha walifanya kichuguu kidogo cheupe. Taswira hii inaonyesha mavuno ya jitihada zao za kujenga ujamaa. Ni sawa na mchele ulioandaliwa kwa mapishi. Kichunguu hutengenezwa kwa ushirika wa mchwa. Kwa hivyo, hii ni sitiari-fiche inayoonyesha ushirikiano wa wananchi katika kuleta ujamaa baada ya kutangazwa Azimio la Arusha.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi aeleza kwamba chenga na mchanga vilikuwa vingi sana. Hii ni ishara kuwa vikwazo vilikuwa vingi. Aendelea kueleza kwamba walipika baada ya muda mrefu wa kazi. Anaonyesha kwamba harakati zao za kujenga mfumo wa ujamaa zilichukua muda mrefu. Hata hivyo, Kezilahabi anaonyesha mshangao anaposema kwamba walianza kula na kupata kuwa bado kuna mchanga na chenga! Mbinu hii ya nidaa imetumiwa kudhihirisha mshangao wake kuhusu jambo hili. Anaonyesha kwamba katika utekelezaji wa Azimio la Arusha, bado kuna athari za kikoloni na vikwazo kwani upinzani upo kutoka

kwa wale ambao maslahi yao yalielekea kuhatarishwa na nguvu hizo za kijamaa. Kwa hivyo, ni kielelezo dhahiri cha ugumu katika jitihada za Watanzania za kujenga ujamaa. Aidha, mwandishi anatumia mbinu ya balagha anapokariri kwamba:

> Lini tutaula bila mchanga,
> bila chenga?

Anabainisha kwamba ingawa kazi kubwa imefanywa kuhusu ujenzi wa ujamaa, juhudi hizi hazijafanikiwa vilivyo kwani bado kuna matatizo. Hali hii inakatisha tamaa ndiposa mwandishi hajui ni lini ujamaa utakuwa safi bila kughoshiwa na 'chenga' na 'mchanga'. Kwa hivyo, Kezilahabi amehakiki hali ya Azimio la Arusha kwa mafumbo yenye taswira ya upishi ambao bado haujalainika. Ujumbe upatikanao hapa ni kuwa upo umuhimu wa kuwa macho wakati wa kujenga jamii ya kijamaa kwani vikwazo na upinzani vitakuwepo kutoka kwa wale ambao maslahi yao yanahatarishwa na nguvu hizo za kijamaa. Shivji (1974:34) aeleza kwamba hatua nyingi za kijamaa haziwezi kutekelezwa kwa urahisi kwa sababu zinakumbwa na upinzani kutoka kwa wale ambao maslahi yao na nafasi zao zinahatarishwa.

Tamko hili lamaanisha kwamba wale ambao maslahi yao yanahatarishwa na nguvu za kijamaa watapigana kufa na kupona kuendeleza mfumo wa kibepari.

3.3. SHAIRI: "HATUMWONI"

Katika shairi hili mshairi aonyesha kuwa viongozi ni kikwazo kikubwa kwa watawaliwa. Pia anadhihirisha kwamba viongozi hawajali maslahi ya umma na inafaa waondolewe kabisa kwani tukio hilo laweza kuwa lenye faraja kwa umma.

Katika ubeti wa kwanza, Kezilahabi ahimiza kwamba wale 'miungu' waliosimama katika vichaka waambiwe wakae chini kwani ni warefu. Taswira hii ina maana kwamba viongozi wamejitenga na umma na ni vikwazo kwao. Miungu ni neno litokanalo na mungu ambaye ni chochote kinachoabudiwa na binadamu kwa kuamini kuwa kina uwezo wa kumsaidia au kumtimizia mahitaji yake. Kwa hivyo, 'miungu' ni jazanda inayoeleza dhihaka ya viongozi wasiojali umma. 'Vichaka' ni pahali palipotengwa na hii ni jazanda inayoibusha dhana ya kujitenga kwa viongozi. Pia kichaka aghalabu huwa ni kipande cha mti kinachotiwa katika mti mwingine baada ya kukatwa kidogo kwa ajili ya kuunyosha mti huo. Kwa hivyo, mwandishi ametumia jazanda hii kukashifu ukoloni mamboleo ambapo hulka za viongozi si halisi. Wamesaliti uhuru uliopiganiwa na wananchi kwa kujitenga na kuwasahau wananchi hao. Badala yake wanashirikiana na mfumo wa kinyonyaji wa ukoloni mamboleo kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini. Mwandishi aonyesha kwamba

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

viongozi waliotarajiwa kurekebisha na kuondoa athari za kikoloni ndio hasa wanaosaidia kuziendeleza. Vilevile mwandishi ametumia taswira ya 'warefu' kueleza dhana kwamba viongozi hao ni kizingiti kwa umma.

Mwandishi anakariri kwamba viongozi hao wakae chini kwani ni warefu. Taswira hii yaonyesha kwamba viongozi hao watoke mamlakani kwani ni vikwazo au vizuizi vya wengi walio chini ya utawala wao. Hii ndiyo sababu anasisitiza kuwa:

> Wengi nyuma, hatuoni!

Mshairi aendelea kusema kwamba hawataki kuona visogo vyao vichafu. Jazanda hii inadhihaki maongozi mabaya ambayo yamewachukiza na kuwachosha wananchi. 'Visogo' ni taashira ya kuwa nyuma ya utawala fulani. Kwa hivyo, maongozi yanayozungumziwa ni mabaya. Hii ndiyo sababu mwandishi anatoa wito kwa viongozi watoke. Akariri kwamba:

> Kaeni chini miungu, kaeni chini!

Dondoo hili linatilia mkazo dhana kwamba kutoka mamlakani kwa viongozi kutawawezesha wananchi kuona mbele. Wataweza kupiga hatua kimaendeleo. (Leaders without a vision)

Katika ubeti wa pili, mwandishi aendelea kukariri kwamba hao viongozi watoke. Hali kadhalika anasisitiza

kwamba viongozi hao waache "kelele za jaza-tumbo." Usemi huu unadhihirisha kuwa wanachong'ang'ania viongozi ni kujilimbikizia mali. Kwa hivyo, mshairi aendelea kukariri kwamba watoke kwani walio nyuma mioyo yawachoma. Msemo huu una maana kwamba watawaliwa wanaudhika na mienendo hiyo mibaya ya kinyonyaji ya kibepari isiyojali utu wala maslahi ya wengine. Hii ndiyo sababu Kezilahabi anakariri kwamba wanataka 'kuchagua watu'. Jazanda hii inaeleza dhana kwamba wananchi wangependa kuchagua viongozi wenye kujali maslahi ya umma na ambao wana utu. Kwa hivyo anawakebehi viongozi wa wakati huo. Aidha, anawasuta viongozi ambao walipewa uongozi uliowapaka rangi. Taswira hii inaashiria kwamba viongozi waliyatumia vibaya mamlaka yao. Waligeuka wanyama na kuwadhulumu wananchi ili kujiendeleza wao wenyewe. Hii ndiyo sababu mshairi anakariri kuwa viongozi walipewa madaraka yakawalevya. Mlevi huwa ni mtu anayetumia pombe, bangi au kasumba mpaka fahamu zake zikabadilika. Kwa hivyo, ni ishara kwamba mienendo ya viongozi ni mibaya mno ndiposa Kezilahabi anasisitiza kwamba wayavue madaraka hayo na kuwapisha wenye nia. Tamko hili lina maana kwamba haja ya viongozi hao ni kujinufaisha kibinafsi na sio kuhudumia umma. Kuna haja ya viongozi wenye nia ya kuongoza kwa mujibu wa umma.

Katika ubeti wa tatu, mwandishi anatumia maswali ya balagha yenye kuchipua mzinduko wa viongozi ili waache mamlaka. Anasema:

> Au hamjaona, ikifura ya wengi watu?
> Ulizeni ya Saidi aliyechomoa sokoni
> na ya Abadalla aliyegonga maskini?...

Mwandishi anatumia sitiari-fiche kuonyesha mfano wa wale waliochomolewa baada ya kuwadhulumu raia. Hii ina maana kwamba viongozi hao watatendewa vivyo hivyo wasipoacha mamlaka kwa hiari yao wenyewe. Anawebeza viongozi ambao angependa waache madaraka ili wananchi wapate fursa ya kwenda mbele. Anawahimiza wajipweteke chini raia wawakanyage wapite mbele ili wapate kujisukuma. Anawaangaza kama watu wasiofaa hata kidogo. Pia anaonyesha kwamba raia wananyonywa. Asema kwamba:

> Sisi twauza bidha ninyi mwauza
> maneno! Tuko sawa haikai mdomoni.

Ni dhihirisho kuwa viongozi wao hutamka kwamba watu wote ni sawa kwa mujibu wa ujamaa, lakini si hivyo. Kuyashadidia maoni haya, Muhammed Khatib katika mswada wa diwani yake ya Fungate ya Uhuru, aeleza kwamba wanaotenda kazi za sulubu na kuzalisha mali sio wapatao ziada na tija hiyo. Kwa hivyo anaona kuwa wale wakulima na wafanyikazi wanaozungumziwa katika majukwaa ya kisiasa

kwamba ndio wanaofaidika na matunda ya uhuru na ujamaa hawayapati hayo hata chembe.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi anawahimiza watu wakate misitu yote. Taswira hii inamaanisha kuondoa kila kitu ambacho chaweza kuwasetiri viongozi. Hivyo, raia watapata zana za ukombozi. Mwandishi anawadhihaki viongozi kwa kusema kuwa watawafanya vinyago vya kuchezewa na watoto. Hii yamaanisha kwamba viongozi wamedharauliwa kwa vitendo vyao visivyofaa. Kwa kawaida, kinyago ni kitu kilichochongwa na kufananishwa na kitu, mtu au mnyama mwingine.

Mtunzi ametumia stihizai ambapo ahimiza watu wakaushe maziwa ili viongozi wasipate maji. Pia angependa watu wawalovye maji viongozi ili wasiweze kuruka angani. Yaani kuwaondolea uwezo wowote ule ili wakwame. Aidha, anahimiza kwamba watu wakoke mioto ili wawachome mashujaa hao wa uonevu. Hii ina maana kwamba waliwatendea watu unyama bila kujali utu wao. Kezilahabi asema kwamba hapatakuwa na kilio wala matanga bali hoi hoi za ushindi na madaraka kwa umma. Kwa hivyo, maangamizi ya viongozi ni furaha na uhuru kwa umma.

Shairi hili linaonyesha kuudhika kwa mtunzi kutokana na maongozi ya kinafiki ya kibepari yenye

unyonyaji, uonevu na ugandamizi. Kwa hivyo, atoa wito kuwepo na ujenzi wa jamii-mpya yenye viongozi wenye kujali maslahi ya umma na wasio wanyanyasaji. Angependa dalili zote za kibepari ziangamizwe.

## 3.4. SHAIRI: "KIFO CHA MENDE WEKUNDU"

Katika shairi hili, mtunzi anazungmzia utawala wa nchi. Anaonyesha kwamba kujenga taifa ni kazi ngumu. Pia anaonyesha athari za ukoloni mamboleo na jinsi ya kukabiliana nao. Kichwa cha shairi hili ni jazanda inayojenga ujumbe wa mwandishi katika shairi zima.

Katika ubeti wa kwanza, Kezilahabi ametumia jazanda ya kujenga nyumba kueleza juhudi za kujenga taifa. Ameonyesha kwamba katika kujenga nyumba itabidi jasho jingi likuoshe. Tashihisi hii ina maana kwamba ni kazi ngumu ambayo ni ya kutoa jasho jingi. Vilevile ametumia taswira ya kufyeka, kupima na kuweka nguzo, paa na kukandika kueleza kazi ya ujenzi wa nyumba. Hizi juhudi ni sawa na kujenga taifa kwani kiongozi hutokwa na jasho jingi. Kufyeka ni taashira ya kuondoa vikwazo vya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Pia lazima afanye makadirio ya kitaifa katika idara mbalimbali na kuteua wasimamizi bora ambao watakuwa ndio nguzo ya taifa. Huu ndio ujumbe uliojikita katika ishara ya kupima

na kuweka nguzo. Usimamizi bora ni tegemeo na mhimili wa taifa. Aidha ametumia picha ya kuweka paa na kukandika kueleza dhana ya viungo vitakavyosetiri taifa kama vile idara ya ulinzi, elimu, afya, kilimo miongoni mwa nyingine. Baada ya kufanya hayo yote, mwandishi aeleza kwamba siku nyingi hazitapita kabla hujaingiliwa na mgeni. Usemi huu una maana kwamba utatembelewa na mgeni asiye na mwaliko.

Katika ubeti wa pili, mtunzi aeleza kwamba mende wataanza kutalii mipaka usiku. Mende ni mdudu anayependa kutafuna vitu na apendaye kukaa sehemu za giza. Jazanda hii imetumiwa na mwandishi kuwaeleza walanguzi ambao wanapenda kuendesha shughuli zao kisirisiri ili kulawiti wenzao. Watu kama hawa huzunguka kila pembe ya nchi kwa kutumia hila na mbinu zisizoeleweka. Hawa ni watu haramu. 'Kutalii mipaka' ni usemi unaomaanisha kuzunguka nchini. 'Usiku' ni taashira ya kutenda mambo faraghani au kiharamu. Mwandishi aendelea kueleza kwamba watazunguka "nje na ndani ya nyumba" kuonyesha kwamba watazuru kila pahali. Vilevile anakariri kwamba watakula ulicho nacho bila woga wala ruhusa. Hali hii ni kielelezo cha jinsi ambavyo mataifa yaliyoendelea huyanyanyasa yale yanayostawi. Mataifa 'Makubwa' yana nguvu ambazo mataifa 'Machanga' hayawezi kushindana nayo. Hii ndiyo sababu yanatenda lolote bila kujali. Mwandishi aeleza kwamba masalia yatakuwa ndiyo ijara ya kazi yako. Usemi huu

unaeleza dhana kwamba watu kama hao watanyakua kila kitu chenye thamani. Kitakachoachwa ndio mshahara wa kazi ngumu ya kujenga taifa lako. Mwandishi anabainisha kwamba mataifa machanga yamefanywa fukara kulingana na sera kama hii. Hii ndiyo sababu yameendelea kutegemea mikopo na misaada kutoka nchi zilizostawi. Huu ukosefu wa uwezo ndiyo njia moja ya kurutubisha ukoloni mamboleo na kunyanyaswa.

Katika ubeti wa tatu, mwandishi asema:

> Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima
> uihame,
> Ukae nje nzima siku usubiri,
> Wazima wamelala ukirudi usiku,
> Vichwa ngumu hawafi mende rahisi

Taswira katika ubeti huu ni kwamba tahadhari zinazochukuliwa kuwaangamiza walanguzi wa kibepari hazifai chochote na haziwadhuru kamwe. Hii ndiyo sababu mwandishi akatumia msemo "vichwa ngumu" kumaanisha kwamba si rahisi kuwaangamiza. Ni wakaidi ambao wana hila nyingi za kujiendeleza.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi anatumia mbinu ya nasiha kueleza namna ya kukabiliana nao. Anatoa wito kwamba kifo cha mende sharti miguu juu, na kichwa ukikanyage kipasuke usikie. Taswira hii inaeleza dhana

kwamba watu kama hawa ni lazima uhakikishe kwamba umewaangamiza kabisa. Usipofanya hivyo, watatumia hila nyingine na kuendelea kudumu. Hii ndiyo sababu Kezilahabi anasisitiza kwamba:

> ... Na kisha wengine usiku mchana
> uwasake, mpaka watakapokwisha.
> Usiseme nao.

Msemo wa kuwasaka wengine usiku na mchana unamaanisha kwamba kila juhudi lazima zifanywe kila mara ili kuwatafuta wale wanaoshirikiana nao na kuwamaliza vivyo hivyo. Aidha ametumia usemi wa kutosema nao akimaanisha kwamba kusiwe na huruma wala mawasiliano na watu kama hao ili kukomesha kabisa ushirikiano nao pamoja na shughuli zao za kinyonyaji.

Shairi hili linapiga vita ukoloni mamboleo katika mataifa-huru ya Kiafrika. Mwandishi amedhihirisha kwamba sera hiyo ni hatari kwa ustawi wa nchi yoyote ile. Kwa hivyo, suluhisho ni kukomesha ushirikiano na mfumo kama huo.

## 3.5. SHAIRI: "JUA LA DHAHABU"

Shairi linazungumzia Azimio la Arusha. Mulokozi alipitia awamu tatu za mabadiliko ya kisiasa tokea wakati wa kudai uhuru, baada ya kupata uhuru na baada ya kuzaliwa

Azimio hili. Katika shairi hili, anatubainishia matumaini yake juu ya Azimio la Arusha. Amelipokea kwa shangwe.

Kichwa cha shairi hili ni jazanda inayobeba ujumbe wa shairi lote. Jua ni sayari itoayo mwangaza wa kumulika nchi na hivyo kuwaongoza watu. Dhahabu ni madini yenye thamani kubwa na ambayo hutumiwa kufulia vyombo au kutengenezea sarafu za matumizi. Kwa hivyo, Mulokozi ameliona Azimio kama tumaini la wanyonge ambalo lingewaongoza hadi kwenye ustawi.

Katika ubeti wa kwanza, mwandishi asema kwamba ameona jua la dhahabu katika mji wa Arusha. Taswira hii inaonyesha tumaini kubwa la mtunzi katika Azimio. Anasema kwamba miale yake imepenya anga la nchi yake na kukifukuza kiza mbele ya macho yake. Miali ya jua ni jazanda inayoeleza dhana ya nguvu ambazo zingeondoa mfumo wa kibepari uliojaa dhuluma, unyonyaji, maonevu na unyonyaji. Nguvu hizo zingeondoa "giza" ambalo ni jazanda la kuonyesha kudharauliwa, kugandamizwa na kunyonywa kwa watu wanyonge.

Katika ubeti wa pili, mwandishi akariri kuwa ameona jua la dhahabu katika mji wa Arusha ambalo litammulikia njia asiweze kujikwaa. Taswira hii yaashiria kwamba Azimio lilikuwa tegemeo kubwa kwake na hasa

wanyonge na ambalo lingewaongoza katika kila nyanja ya maisha ili waendelee bila tatizo. Katika ubeti wa tatu, Mulokozi anaendelea kusisitiza upokeaji wa Azimio kwa kushangilia tukio hilo ambalo ameeleza kwamba lingemulika vidato vya wanyonge kupandia na kuonyesha njia ya kufuatia. Vidato huwa kwenye ngazi na aghalabu humwezesha mtu kupanda juu. Hii ni ishara ya kuwaongoza wanyonge kujiendeleza kijamii, kiuchumi na kisiasa. Vilevile, hivi vidato ni taashira ya kuendelea hatua kwa hatua. Kwa hivyo, Azimio la Arusha lilichukuliwa kama muokozi wa wanyonywa jasho. Lilitarajiwa kuondoa athari za kikoloni na ni hatua muhimu katika historia ya Watanzania.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi aendelea kukariri kwamba ameona jua la dhahabu katika mji wa Arusha ambalo miali yake imepenya anga la nchi na kuwasha tabasamu ndani ya moyo wake. Taswira hii inaeleza dhana ya mapambazuko mema maishani mwa wanyonge. Kulikuwa na matumaini ya kuongozwa vyema ili wanyonge wapate fursa ya kupanda ngazi na vidato vya kuushikilia uchumi wa nchi na madaraka mikononi mwao. Matumaini ya mapinduzi kutoka hali yao duni ya kudharauliwa, kudhulumiwa na kunyonywa yanawapa tabasamu na ndiposa wanalipokea Azimio kwa vifijo na nderemo. Lingewaokoa kutoka katika 'ngome' ya ubepari uliokithiri.

Shairi hili lina mwelekeo sawa na lile la Kezilahabi la Ukucha wa Jadi ambapo mshairi anaonyesha matumaini yake makubwa juu ya Azimio na kuitoa sumu ya ubepari wa wanyonyaji. Anaonyesha kuwa Azimio lingeangamiza mabepari katika jamii.

## 3.6. SHAIRI: "DAMU MPYA YATIRIRIKA"

Shairi hili limetungwa juu ya uongozi wa nchi. Kahigi anaonyesha kuwa kuna harakati za ujenzi wa utawala mpya katika nchi ili kuondoa ule wa zamani. Kuna msisimko na ari miongoni mwa vijana wenye matumaini makuu ya kuendeleza na kufanikisha taifa.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi awanasihi wenzake kwamba wao ni wimbi la ujana ambao nyota yao inawaka na njia waiona mbele. Ametumia jazanda ya "wimbi la ujana" kueleza dhana kwamba kama wimbi lilivyo mtutumko wa maji baharini, ziwani au mtoni, nao wana fursa ya kutumia nguvu za ujana wao kuleta mabadiliko katika utawala wa nchi. Jazanda hii inasaidia kuibusha ujumbe wa shairi ambao umejikita katika kichwa cha shairi hili. Kizazi kipya cha vijana kimekasirishwa na uongozi mbaya. Mshairi ametumia taswira ya "nyota yao kuwaka" akimaanisha kwamba maoni yao ndiyo yanayotia fora katika nchi hiyo iliyooza. Mwandishi analinganisha vijana na nuru ya nyota ambayo huonekana zaidi wakati wa usiku. Hii ina

maana kwamba kuna maovu mengi nchini ambayo yamemulikwa na vijana.

Katika ubeti wa pili, Kahigi ametumia takriri kuonyesha kuwa "damu mpya yatiririka katika mishipa ya bahari hii." Mwandishi ametumia jazanda ya "damu" kuonyesha kuwa kuna nguvu mpya ambazo ni nguzo ya taifa kwani damu inahusika na usafirishaji wa hewa na chakula mwilini. Bila damu, hakuna uhai. Kwa hivyo, nguvu za vijana ni tegemeo la taifa. "Bahari hii" ni jazanda ielezayo nchi yake. Mwandishi aeleza kwamba damu mpya yachemka katika ubongo wa kizazi kipya. Taswira hii yabainisha kwamba kuna ari na mori miongoni mwa vijana.

Katika ubeti wa tatu, mtunzi anaashiria kwamba mapengo na mashimo ya jana na leo sasa yameshaanza kuzibwa. Mapengo na mashimo ni jazanda zielezazo udhaifu katika uongozi. 'Jana' ni kielelezo cha utawala wa awali, na 'leo' ni utawala wa sasa. Kahigi aendelea kusema kwamba hirizi na midali za uwongo wa jana na leo sasa zinapigwa teke. Hizi zinaashiria itikadi zilizo-dumisha utawala ambao mwandishi nausuta na kuudhihaki. Ni vitu vinavyoaminiwa kuwa ni kinga dhidi ya madhara. Kwa hivyo, mwandishi anakejeli sera hiyo ya uongozi kwa msemo kwamba 'imepigwa teke' akimaanisha kwamba imepigwa

marufuku na vijana. Maongozi kama hayo yenye imani potofu hayana nafasi tena.

Katika ubeti wa nne, mshairi akariri kuwa vijana wataweka mbolea kwenye shamba lao na wapande mbegu bora za maharagwe na mtama pamoja na mimea yenye rutuba itakayoota, ikue na wavune. Taswira hii yaeleza dhana kwamba nguvu za kizazi kipya zitaongeza uhai katika nchi kama mbolea iongezavyo rutuba ardhini ili kuwe na mazao mema. "Shamba" ni jazanda inayoeleza maongozi mapya ya nchi. "Mbegu"ni sera ya utawala wa nchi ambao vijana wanuia kuanzisha na kuuendeleza ili nchi ipate fanaka. Kadhalika, mwandishi ametumia jazanda kwamba "misuli yao lazima ijenge nyumba mpya pahali pa nyumba za jana". Anamaanisha kwamba nguvu zao lazima ziunde serikali mpya katika nafasi za zile zilizotangulia.

Katika ubeti wa tano, mshairi anakejeli utawala wa awali kwa msemo kwamba "damu kongwe yenye ukaidi haifui dafu kwa damu mpya." Hii ina maana kwamba maongozi ya awali yaliyokosa ushupavu hayana nafasi katika kizazi kipya. Pia mtunzi anatumia jazanda ya "ndege wa matumaini anaimba"kueleza kwamba kuna ishara njema ya kufanikiwa kwani ndege mwema huwa ni msemo wenye kueleza ishara ya wema. Kahigi anaendelea kueleza kwamba damu mpya kwa furiko inachemka kwa mwendo wa mbele. Msemo huu unaashiria kwamba kuna

ari miongoni mwa vijana wengi ambao wameshamiri nchini.

Mwandishi anaendelea kueleza kwamba kule upeoni, "Mawingu yanakusanyika kama ishara ya matumaini yenye kuneemesha maisha." Taswira hii inaeleza dhana kwamba mbeleni, kuna dalili za matokeo mema kwa kuwa mawingu huwa dalili ya mvua. Mwandishi aonyesha matumaini makubwa katika ufanisi wa maongozi ya vijana ambao wameghadhabika na kununa.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi anasisitiza kwa kuwanasihi wenzake wasikilize wito wa "wimbi," ambayo ni jazanda ya ari na msisimko. Anawazindua wanajeshi kutumia fursa yao ili kuondoa utawala wa sasa kwa nguvu. Anatilia mkazo dhana ya matumizi ya nguvu ili kuleta utawala mpya.

Shairi hili ni mfano wa utunzi uonyeshao kutoridhika na utawala kaidi wenye kutumia nguvu kunyanyasa raia. Mwandishi amebainisha kwamba utawala kama huo hauna nafasi sasa. Pia, anadhihirisha kuwa kuliko kukaa tu na kulalamikia maongozi mabaya, watu hawana budi kuzinduka ili wachukue silaha na kujihami wenyewe. Huu si wakati wa kukaa tu kitako na kulalamika. Kunahitajika ujasiri na kujitoa mhanga ili lengo la ufanisi lifikiwe.

4.0. SURA YA NNE

## UCHUMI

### 4.1. SHAIRI: "AZIMIO"

Shairi limetungwa juu ya Azimio la Arusha la 1967. Kezilahabi amewahi kuishi katika awamu tatu za historia ya Tanzania. Alishuhudia harakati za kupigania uhuru wa nchi yake. Pia alishuhudia matukio ya nchi yake mara tu baada ya uhuru na Azimio la Arusha. Katika shairi, mshairi anabainisha mwelekeo wake katika kulipokea Azimio. Anaonyesha kwamba halikuleta mabadiliko wala manufaa yoyote. Pia anaeleza kwamba hakuna chochote cha muhimu ambacho kimetekelezwa.

Katika sehemu ya kwanza ya shairi, Kezilahabi asema kwamba Azimio sasa ni mabaki ya chakula kwenye sharubu za bepari. Kwa kawaida mabaki ya chakula huwa ni chakula kilichoachwa baada ya watu kula na kushiba. Sharubu ni unywele uotao karibu na mdomo. Naye bepari ni mnyonyaji mwenye kumiliki rasilimali na njia kuu za uchumi katika kuzalisha mali kwa faida yake mwenyewe. Kwa hivyo, mwandishi ametumia taswira hii kuonyesha kwamba kiuchumi, Azimio lilikuwa sasa ni mabaki ya sera ya kibepari na lingeongozwa na wenye kuathiriwa na mfumo huo. Hakungekuwa na chochote kipya. Hata baada ya kuzaliwa Azimio la Arusha, mabepari weusi walikuwepo.

Kezilahabi aeleza kwamba Azimio ni kalamu inayovuja katika mfuko wa mwanafunzi. Usemi wa kalamu inayovuja waonyesha kuwa kalamu inatoa wino. Jambo hili latatiza elimu ya mwanafunzi huyo. Ni ishara ya vikwazo katika elimu yake. Kwa hivyo jazanda hii inaeleza dhana kwamba badala ya Azimio kuwa lenye manufaa kwa Watanzania, liliwaharibia mambo hata zaidi. Halikutekeleza mambo kama ilivyotarajiwa. Hakuna cha maana cha kuinua uchumi wa taifa hili changa. Pia mwandishi anakariri kwamba Azimio ni vumbi zito baada ya ng'ombe kupita. Kwa kawaida, ng'ombe wapitapo hutimua mchanga hewani na huwa vigumu kwa mtu kuweza kuona vizuri. Kwa hivyo, jazanda hii inaashiria hali yenye hila nyingi ambazo zilitumiwa na viongozi ili kuendeleza ubepari wao kwa kuwaziba watu macho. Mathalan, kuhubiri ujamaa huku wakinyonya raia.

Mshairi aeleza kuwa "hakunyolewa, hakupewa kalamu mpya na njia haikuzibwa." Hakunyolewa ni jazanda ionyeshayo kwamba mkoloni hakuondolewa kamwe. Hakupewa kalamu mpya ni jazanda yenye maana kwamba Watanzania wangeendelea kufuata sera ya kikoloni ya kibepari. Njia haikuzibwa ni usemi wenye maana kwamba wakoloni wangeendelea kunyonya taifa la Tanzania chini ya utawala 'Mweusi' chini ya sera ya ukoloni mamboleo. Anachosisitiza mwandishi kupitia jazanda hizi ni

kwamba baada ya Tanzania kujipatia uhuru wake mwaka wa 1961 kutoka kwa Mwingereza, nchi hiyo ilifuata mfumo wa uchumi wa kibepari. Lakini kulitokea haja ya kuwepo sera mpya ambayo ingefuata maongozi tofauti katika Tanzania huru ndiposa kukawa na Azimio la Arusha kama mwanzo wa siasa mpya ya ujamaa. Mfumo huu mpya uliazimia kuleta usawa wa kiuchumi miongoni mwa wananchi na kuondoa kila aina ya unyonyaji. Hata hivyo, mwandishi abainisha kuwa kulikuwa na matatizo mengi ambayo yaliukumba mpango huo. Anaona kwamba hata baada ya Azimio, matunda ya uhuru bado hayajafaidia umma na hakuna neema kwa mafukara. Mwandishi anaashiria kwamba walichopata "akina kabwela" ni kuongezeka umaskini na dhuluma chini ya utawala wa uongozi wa Waafrika wenzao. Anacholalamikia mwandishi ni ile hali ya "unaizesheni" wa Kiafrika ambapo viongozi wanahodhi mali na uchumi wa taifa. Kwa hivyo, ubepari ni itikadi ya kinyonyaji wala sio rangi ya mtu.

Vilevile, mwandishi kupitia kwa jazanda za hapo juu anaona kuwa Azimio la Arusha limetangazwa lakini mipango ya kiuchumi si dhahiri. Hii ndiyo maana kuna "vumbi zito baada ya ng'ombe kupita." Maadam njia haikuzibwa na bepari hakunyolewa, tatizo la kule kuwepo kwa matabaka ya wanyonyaji na wale wanaonyonywa litazidi kuwepo. Hali hii ya mvutano itaendelea kushamiri kama ilivyokuwa mara tu baada

ya uhuru. 'Ukoloni' wa Kiafrika utaendelea.

Kezilahabi aendelea kueleza kwamba kilichosalia sasa ni punje za ulezi zilizosambazwa jangwani na mpandaji kipofu. Punje ni chembe ya nafaka; jangwani ni eneo kubwa lenye mchanga na lisiloota nyasi wala miti. Kipofu ni mtu asiyeona kwa kupofuka kwa ajili ya kuugua au kuzaliwa hivyo. Kwa hivyo, mwandishi ametumia taswira hii kueleza dhana kwamba mali chache iliyobaki ni kama shukrani kwa kuitunza nchi. Hata hivyo, anawakebehi viongozi kwa kuonyesha kwamba mali hiyo haina manufaa yoyote kwani imewekwa katika miradi isiyo na faida na kiongozi asiye na mwelekeo wowote. Mali kama hiyo itazidi kupotea na haitawanufaisha raia wa nchi hata kidogo. Mwandishi abainisha kwamba Azimio la Arusha limetangazwa lakini bado kuna tabaka la wanyonyaji. Hali hii inadhoofisha uchumi wa nchi na kuongeza ufukara na unyonge kwa umma. Kwa hivyo, mwandishi haoni mabadaliko yoyote kwa ajili ya umma. Kezilahabi anahakiki hali ya Azimio kwa kejeli na stihizai. Halikuwa na chochote cha manufaa kwa Watanzania. Viongozi wa Kiafrika wanaendeleza ubepari uliojaa ubinafsi, ugandamizaji na unyonyaji. Hali kama hii ni ya kukatisha tamaa katika mataifa huru ya Kiafrika, ikiwemo Tanzania. Hali kama hii ni ithibati ya maelezo ya Rodney (1972:284) kuwa:

> Ili kukawilisha au kuteka nyara mapinduzi ya Kiafrika, wakoloni waliligeukia kundi lile ambalo walikuwa wameliunda kwa madhumuni maalum...

Dondoo hili laonyesha kwamba viongozi walioteuliwa waliendelea kuwa na uhusiano na dola lililokuwa linatawala wakati wa ukoloni kwa sababu ya elimu yao ya kikoloni waliyoipata katika lugha, mawazo na hata nafsi. Elimu hiyo imewafanya waendelee kuutumikia ubepari hata baada ya kuondoka wakoloni.

## 4.2. SHAIRI: "NGOMA YA KIMYA"

Katika shairi hili, Kezilahabi azungumzia amali za kitaifa nchini mwake baada ya uhuru. Aonyesha kwamba nchi yake iliathiriwa sana kiuchumi wakati wa ukoloni. Pia aeleza kwamba Waafrika hawaelewi vyema hulka za kikoloni. Aidha ameazimia kukusanya mali iliyoachwa ili ajijenge na kujiendeleza kisirisiri kwa mujibu wa hali ya maisha katika jumuiya. Kichwa cha shairi ni jazanda inayoongoza ujumbe wa shairi zima. Kwa hivyo yeye ni kielelezo cha watu waliojificha katika ujamaa huku wakinyonya umma.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi aeleza kuwa wacheza ngoma wamekwishaondoka na kilichobaki ni uwanja

uliokauka majani, njuga, manyoya na kindu zilizodo-ndoka toka kwa wachezaji waliozidisha mbwembwe nao watazamaji wakipiga kelele na vigelegele. Ngoma ni mchezo wa kufuata mdundo wa ala hiyo. Kwa hivyo, wacheza ngoma ni jazanda inayoeleza dhana ya wakoloni walionyonya nchi kulingana na mfumo wa kibepari usiojali maslahi ya umma. Uwanja uliokauka majani ni taswira inayoashiria uchumi wa nchi ambao uliathiriwa mno na ubepari wa kikoloni. Njuga ni kengele ndogondogo zifungwazo miguuni, mikononi au shingoni wakati wa kucheza ngoma. Manyonya, na kindu pia huvaliwa wakati wa kucheza ngoma. Kwa hivyo, ni mabaki ya athari baada ya ubepari wa kikoloni. Wachezaji waliozidisha mbwembwe ni msemo wenye maana kwamba wakoloni walijaa majivuno.

Mwandishi ametumia jazanda ya watazamaji akimaanisha Waafrika ambao amewatweza kwa kushangilia tendo hilo kwa kukosa kuelewa. Amewabeza kwa kupiga kelele na vigelegele kushangilia "uhuru" kwani hawaelewi kuwa ni uhuru wa bendera tu. Hivyo, mwandishi aonyesha kuwa uhuru waliopata haufai chochote. Unyonyaji utaendelea. Kezilahabi asema kwamba ni jana tu walikuwa hapa. Usemi huu una maana kuwa si muda mrefu uliopita tangu wakoloni wawe hapa. Hali kadhalika aeleza kwamba wachezaji sasa wafikiria

ngoma ijayo. Taashira hii yamaanisha kwamba wakoloni sasa wafikiria mbinu nyingine za kutumia ili kuzidi kunyonya uchumi wa Tanzania, hasa kudumisha ukoloni mamboleo.

Mwandishi anakariri kwamba "watazamaji" hawayakumbuki maneno ya nyimbo zote zilizoimbwa. Jazanda hii ina maana kwamba Waafrika hawaelewi hulka zote za matendo ya kikoloni. Hii ndiyo sababu anatumia msemo kwamba zilizobaki ni taswira hai na vivuli. Hii inadhihirisha kwamba Waafrika wanaona athari za matendo ya kikoloni lakini kuna ukungu wa ujinga unaowafanya kukosa kuelewa uhalisi wa mambo. Hawaelewi hila zitumikazo. Hawaelewi mienendo ya wakoloni.

Katika ubeti wa pili, mwandishi asema kwamba labda "miti" hii michache yakumbuka. Miti michache ni jazanda ya watu wachache ambao waweza kung'amua sera ya kikoloni. Aendelea kueleza kwamba "ataviokota" atengeneze vazi lake. Usemi huu una maana kwamba atakusanya vitu vilivyoachwa na wakoloni ili kujijenga kiuchumi. Hii ndiyo sababu Kezilahabi asema kwamba kisha atacheza ngoma yake kimyakimya katika uwanja huo mpana ulioachwa wazi bila watazamaji. Hasa anuia kujiendeleza kisirisiri katika mfumo wa kiuchumi ulio tupu bila chochote. Pia mwandishi anaashiria

umma uliokumbwa na umasikini. Mwandishi pia asema kwamba upepo utamfundisha lugha ya kimya maana "yule mwanamke amekwishajifungua." Upepo ni hewa isiyotulia. Kwa hivyo, ni jazanda ya mfumo wa kiuchumi unaobadilika na ambao ungemfunza jinsi ya kuendesha shughuli zake kisirisiri. Baada ya uhuru, Tanzania ilitarajia kuwa na mfumo wa kijamaa ili kuondoa mfumo wa kinyonyaji wa kibepari. Kwa hivyo, Kezilahabi ametumia tashtiti kuwabeza wale watu walionuia kwa kuongozwa na ubinafsi, kujinufaisha wao wenyewe katika mfumo wa kijamaa. Hii ndiyo sababu ametumia msemo kuwa "maana yule mwanamke amekwishajifungua." Azimio lilikuwa limewisha tangazwa. Matendo kama hayo yanaashiria viongozi ambao ni nguzo ya ukoloni-mamboleo katika Afrika huru. Huu ni mfano wa viongozi waliojitenga na umma ili washirikiane na waendelezaji ubepari kuzidi kuwanyonya na kuwagandamiza wananchi wa tabaka la chini. Ni viongozi kama hawa ambao hasa wanasaliti uhuru wa nchi zao. Hawajali maslahi ya umma bali ubinafsi unawafanya kuwa makaragosi wanaohudumia 'mabwana' zao kutoka nje. Viongozi kama hawa hawawezi kamwe kuhudumia vyema watu wanaowaongoza. Kwa sababu ya ubinafsi wa "kucheza ngoma ya kimya," huwa hawana mawasiliano mema na jamii wanazohudumia. Kwa hivyo huzuka dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji wa umma.

## 4.3. SHAIRI: "AFRIKA NA WATU WAKE"

Shairi hili limetungwa juu ya jitihada za Watanzania katika kujenga upya uchumi wa nchi. Kezilahabi anaonyesha kuwa harakati hizi ni ngumu na zinahitaji tahadhari kubwa pamoja na umadhubuti. Pia ahimiza kuchunguza mahali udhaifu ulipotokea.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi asema kwamba anaona mgonjwa amelala kitandani. Taswira hii inaeleza dhana kwamba nchi bado inaharibiwa kiuchumi hata baada ya uhuru kupatikana. Ugonjwa ni ishara ya uchumi wa nchi kuwa katika hali mbovu, na kulala kitandani ni taashira ya kukwama kiuchumi.

Mwandishi anakariri kwamba kama Watanzania hawatamtoa miiba iliyobaki, mgonjwa hataweka miguu yake chini na kutembea bila kujiegemeza. Miiba ni sehemu za mimea zenye ncha kali na zinazoweza kuchoma. Kwa hivyo ni jazanda inayoeleza athari na vikwazo vya kibepari vilivyobaki. Mgonjwa ni mtu aliye na maradhi au maumivu fulani katika mwili wake. Kwa hivyo, ni jazanda inayoeleza nchi iliyokumbwa na hali mbovu kiuchumi. Kutoweza kuweka miguu chini ni ishara ya kutoweza kujiimarisha kiuchumi. Kutembea bila kujiegemeza ni usemi wenye maana ya kujitegemea kiuchumi.

Katika "kutembea bila kujiegemeza", Kezilahabi anaashiria mfumo wa kujitegemea, aina ya sera ambayo Tanzania ilikusudia kuijenga wakati wa Azimio la Arusha. Mfumo wa ujamaa ulidhamiriwa kuwa dawa ya kutibu ugonjwa wa kijamii nchini Tanzania. Vilevile, ilikusudiwa kuondoa matatizo kama yale ya unyonyaji, unafiki na udhalimu. Kwa hivyo, ilikuwa muhimu kuunga mkono harakati zote zinazotetea haki, usawa na amani katika taifa la Tanzania ili nchi ipate kujiimarisha kiuchumi ndipo ipate kuendelea na kujitegemea.

Katika ubeti wa pili, mwandishi asisitiza kuwa miiba iliyomo ndani mwao lazima iondolewe upesi kabla haijaingia kati ya mifupa na kufa pamoja nao. Mfupa huwa kiungo kigumu mwilini mwa mtu au mnyama. Kwa hivyo, ni jazanda yenye kueleza hulka za maisha ya watu nchini. Mwandishi atoa wito kwamba athari za kikoloni ziondolewe miongoni mwao kabla hazijakolea katika mienendo ya watu na kuwaangamiza. Pia Kezilahabi aeleza kwamba baada ya kuitoa, Watanzania wavae viatu vya chuma halafu wacheze nao mchezo wa siasa na uchumi. Chuma ni aina ya madini yaliyo magumu na ambayo hutumiwa kujengea na kuundia vitu. Kwa hivyo, "viatu vya chuma" ni jazanda yenye maana ya kuwa imara. Mchezo ni tendo lifanywalo na mtu au upande zaidi ya mmoja kwa ajili ya mashindano au kuchangamka. Kwa hivyo, mwandishi ananasihi kuwa Watanzania hawana

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

budi kujiimarisha wenyewe kabla ya kushindana na wakoloni kisiasa na kiuchumi.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi akariri kwamba kuitoa miiba hii, Watanzania wanahitaji macho makali, mikono isiyotetemeka, moyo usio na huruma na kuona miiba ilipoingilia. Macho makali ni msemo wenye kueleza dhana ya kuchukua hadhari. Mikono isiyotetemeka ni kuwa madhubuti. Kuona miiba ilipoingilia ni taswira yenye maana kwamba Watanzania lazima wajue mahali ambapo athari mbaya za kiuchumi zilipotokea ili kuziba njia hizo. Mbinu hii ya tashihisi yaonyesha kuwa lazima athari zote za kikoloni zikomeshwe. Kuepukana na athari hizo ili maendeleo yapatikane ni kujiondoa katika mfumo wa kibepari kwa njia ya ujamaa. Njia nyingine ambapo miiba iliingilia ni kupita elimu ya kikoloni ambayo imewakengeusha wasomi, kuwafanya kuchukia chochote cha Kiafrika, kujidharau, kuwafanya wajitenge na jamii zao, pamoja na kuwafanya wapende chochote cha Kizungu. Kwa hivyo, mwandishi anaashiria kwamba kuna haja ya kuwa na mfumo wa elimu ambao utaenda sambamba na matakwa ya nchi na madhumuni ya kijamii katika mazingira ya Kiafrika. Aidha, elimu hiyo haina budi kuwaandaa watu kwa uanachama wao katika jamii na kushiriki kwao katika maendeleo ya taifa lao. Pia njia kuu za uchumi zisihodhiwe na mabepari. Halikadhalika, viongozi wa nchi hawana budi kuchaguliwa na wananchi wenyewe kwa njia ya kidemokrasia.

Mwandishi ahimiza kwamba ili nchi ijikwamue kiuchumi na kujiendeleza, lazima raia wake wajikinge dhidi ya ukoloni mamboleo. Lazima waondoe miongoni mwao nyenzo za unyonyaji wa kibepari. Watu lazima wajikinge dhidi ya vishawishi vya kuupunja uchumi wa nchi. Kwa hivyo, kuna haja ya kuwa macho kuilinda nchi dhidi ya uvamizi wa kutoka ndani na nje ya nchi kiuchumi. Watu lazima wajisake wenyewe na wawe imara katika matendo yao kwa manufaa ya umma.

## 4.4. SHAIRI: "ULIZA WANAOJUA"

Katika shairi hili Kezilahabi anawasuta viongozi wa taifa kuhusikana na uchumi. Dhamira yake ni kuonyesha kwamba baada ya kustaafu, viongozi wa Tanzania hawatilii mkazo wito wa ujamaa. Pia anaonyesha kwamba serikali ina njia zake za kuwanasa watu kama hao ambao hatimaye huaibishwa hadharani.

Katika ubeti wa kwanza, mwandishi atumia mbinu ya balagha kwa kuuliza walikoenda wale waliokuwa viongozi wa zamani na ambao walikuwa wakitoa hotuba za kuupigania ujamaa. Anawasuta kwamba sasa wamestaafu na ndio wafuga kuku. Mwandishi amekariri wazo hili kwa mbinu ya nidaa anaposhangaa kuona kwamba wao ndio wenye majumba na wenye kurithisha ubepari. Kezilahabi anashutumu unafiki miongoni mwa viongozi ambao "utakatifu"

wao ni kupigana na kuhimiza maongozi ya kijamaa wakiwa tu uongozini. Muda wao ukimalizika, wao huwa si wajamaa tena wala hawana habari na maadili ya ujamaa. Kichwa cha shairi ndio mkarara wa shairi lote.

Katika ubeti wa pili, mwandishi aendelea kuwakebehi viongozi kwa kueleza kwamba wao ndio makabaila wenye mashamba na wamilikaji wa matrekta. Anabainisha kwamba watu kama hao ingefaa wawe ruwaza njema kwa umma. Mwandishi aeleza kwamba "zungumza juu ya vijiji na watakuonyesha kidole". Huu usemi ni dhihaka kwa kuwa hawataki uendelezaji wa mapambano dhidi ya unyonyaji na ugandamizaji. Kwa hivyo ni shutuma kuwahusu viongozi wa Tanzania. Methali "pilipili usiyoila yakuwashiani!" imetumiwa na mwandishi kuonyesha kwamba watu kama hao hawaoni sababu ya raia kulalamikia hali au mambo yasiyowahusu. Kwa hivyo hii ni mikinzano ya kitabaka ambapo uchumi wa taifa unafaidiwa na wachache. Hii ndiyo sababu mwandishi anakariri kwamba "uliza wanaojua ukweli watakwambia." Tabaka la juu lanyanyasa lile la chini.

Katika ubeti wa tatu, Kezilahabi asema kwamba darubini la serikali ni kubwa sana tena lina nguvu sana na lina sumaku. Darubini ni chombo chenye lensi na ambacho kinafanya vitu vilivyo mbali vionekane karibu,

na vidogo vionekane vikubwa. Kwa hivyo hii ni taswira inayodhihirisha kwamba serkali inayo macho makali na nguvu nyingi katika utendaji wake wa kazi. Sumaku ni nguvu inayoweza kuvuta vitu vya chuma. Kwa hivyo, ni jazanda iliyotumiwa na mshairi kueleza dhana kwamba serikali ina nguvu ya kuvuta watenda maovu. Hii ndiyo sababu akatumia msemo kwamba linawavuta wakapimwa na chote walichokwisha kula kikaonekana. Hii ina maana kwamba serikali huwachuja vilivyo na kubainisha chochote walichokipata kiharamu.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi aendelea kukariri nguvu za serikali kwa kuonyesha kwamba ina dawa ya kutapisha. Kutapisha ni kutoa uchafu katika koo. Taswira hii imetumiwa kuonyesha kwamba serikali ina nguvu za kutoa uhalifu katika jamii. Hii ndiyo sababu Kezilahabi aeleza kwamba mabepari na makabaila wametapishwa hadharani wakaona aibu mbele ya wake zao. Msemo huu unamaanisha kwamba watu kama hao wamewahi kuonyeshwa hadharani ambapo waliaibika mno. Pia, mwandishi anawadhihaki kwa kusema kwamba:

> Wananchi tuliwazomea tena tukacheka
> sana.

Usemi huu una maana kwamba wananchi waliwatolea maneno ya dharau kulingana na matendo yao maovu. Pia waliwafanyia mzaha.

Kezilahabi anawakejeli viongozi wa zamani ambao sasa ndio wanatenda kinyume cha maadili ya kijamaa. Anaonelea kwamba badala ya kuwa makabaila na mabepari wenye kuzamisha mizizi ya ubinafsi na unyonyaji, watu kama hao ingefaa wawe kielelezo bora kwa umma kwa kuendelea kutetea sera ya ujamaa.

## 4.5. SHAIRI: "MAOMBOLEZO YA MTU MASKINI"

Katika shairi hili, Mulokozi anashughulikia dhamira ya kumtetea mtu mnyonge. Ametumia tamathali nzito kuonyesha undani wa dhiki za maskini. Ameyamulika maisha ya mtu kama huyu kuwa yenye dhiki na azaliwapo huwa tayari amekwisha kufa. Anaona kuwa haishi bali yupo tu kama kitu kingine chochote. Hata hivyo, aonyesha kuwa siku itafika ambapo ataanza kuishi. Kichwa cha shairi ni jazanda inayobeba ujumbe wa shairi zima.

Katika ubeti wa kwanza, mwandishi asema kuwa panya wa uhitaji amguguna tumboni na kumkeketa kama msumeno. Uhitaji ni ugumu wa kupata kitu cha lazima kama vile chakula au pesa. Kukeketa ni kutafuna au kukata kitu kigumu kwa kutumia kitu butu. Msumeno ni kifaa chenye meno ambacho aghalabu kinatumiwa kwa kukatia mbao. Kwa hivyo, panya wa uhitaji ni jazanda inayoeleza dhana ya maumivu anayoyapata maskini kutokana na unyonyaji usiojali hali ngumu aliyomo. Mwandishi ametumia

tashibihi kuonyesha kwamba madhara anayopata maskini ni kama msumeno unavyokata ubao.

Mwandishi akariri hali mbovu ya maskini kwa kueleza kwamba simba wa ubepari ampachika makucha na kumtia mashimo mifukoni. Simba ni mnyama ambaye huaminiwa kuwa ni mfalme wa wanyama wote na ambaye matilaba yake ni nyama. Kupachika ni kuweka kitu baina ya vitu vingine viwili. Ubepari ni mfumo wa kiuchumi unaowezesha watu wachache kumiliki rasilimali na njia kuu za uchumi wa nchi. Huwa ni unyama usiojali utu. Kwa hivyo, Mulokozi ametumia jazanda hii kuonyesha kuwa mabepari wakuu wambana maskini bila huruma na kumdhulumu kwa kunyakua chochote alicho nacho na kumwacha fukara. Hii ndiyo sababu anaeleza kwamba anabakia kutangatanga na kupepesuka kama utete tufanini. Tashibihi hii yamaanisha kuwa maskini hana tegemeo ndiposa ayumbayumba kama unyasi katika upepo mkali. Maonevu ya unyonyaji yamemkosesha nguvu.

Katika ubeti wa pili, Mulokozi akariri kwamba tanuu ya jua imeikaanga ardhi yake, jabali la udongo limebutisha jembe lake na matiti ya uwingu wenye ubahili yamemnyima maziwa ya kuinywesha ardhi yake ya riziki ya maisha. Tanuu ni jiko lililojengwa linalotumika kuchomea vitu. Kwa hivyo, tanuu ya jua ni jazanda yenye maana kwamba kiangazi kikubwa kimekausha ardhi

yake. Jabali ni mwamba mkubwa. Mwandishi ametumia taswira ya jabali la udongo kuonyesha ugumu wa ardhi iliyobutisha jembe lake. Pia ametumia jazanda ya matiti ya uwingu wenye ubahili kueleza dhana ya ukosefu mkubwa wa mvua. Ni ukame mwingi. Kitu bahili huwa chenye uchoyo au ugumu wa kutoa. Aidha mwandishi ametumia takriri kwamba ardhi yake ni ya riziki ya maisha. Usemi huu una maana kwamba ardhi ndiyo tegemeo lake la maisha. Hana kimbilio jingine.

Katika ubeti wa tatu, anaeleza kwamba radi ya maradhi imeuangukia mti wa nasaba yake na kuung'oa hadi mizizini. Radi ni sauti kubwa inayotoka mawinguni na inayosababishwa na umeme. Kung'oa ni kuondoa kwa nguvu. Mwandishi ametumia jazanda hii kuonyesha kwamba maradhi makuu yamevamia jamii yake nzima na kuiangamiza. Mwandishi aendelea kueleza kwamba mishale ya upofu imemfuma macho na barafu ya umri imegandia kichwani pake. Mishale ya upofu ni jazanda inayoeleza uchungu wa kutoweza kuona ambao umefuma macho yake. Barafu ni maji yaliyoganda kwa baridi na kufanya kama jiwe jeupe. Kwa hivyo, mwandishi ametumia jazanda hii kumaanisha kwamba umri mkubwa umemkumba. Hii ndiyo sababu anakariri kwamba hana kimbilio, tegemeo na hisi yoyote ya faraja upeoni. Usemi huu una maana kwamba hana pa kwenda wala matumaini yoyote ya wema katika siku za usoni.

Katika ubeti wa nne, Mulokozi anaeleza kuwa shubiri ya ufakiri umeizimua sukari yake ya maisha na miiba ya dhuluma imeitoboa mikono yake asiweze kujikimu. Shubiri ni utomvu mchungu. Kwa hivyo, mwandishi ametumia jazanda hii kuonyesha kwamba uchungu wa umaskini umemzuia kupata utamu wa maisha. Haoni uzuri wowote maishani. Miiba huwa na ncha za kuchoma. Mwandishi ametumia taswira hii kuonyesha kuwa mateso anayopata kutokana na dhuluma yametoboa mikono yake hata asiweze kujiendeleza kimaisha. Hii ndiyo sababu anatumia msemo kwamba maradhi yamezidi dawa kuonyesha kwamba hakuna tumaini au suluhisho muafaka. Pia, Mulokozi aeleza kuwa funza wa shutuma amemtekenya nyayo asiweze kusonga mbele. Jazanda hii inabeba ujumbe kwamba wadudu wameharibu miguu kiasi kwamba hawezi kutembea. Kadhalika, hali hii yatokana na mateso anayopata kutokana na mfumo wa kibepari unaomdhulumu.

Katika ubeti wa tano, mwandishi akariri kuwa amekuwa mtumwa katika dunia huru, na fakiri katika jumuiya tajiri. Msemo huu unadhihirisha kuwa hali yake ni ya kusukumiwa tu. Ni kuonewa na kunyimwa tu maksudi. Hii ndiyo maana anatumia tashibihi kwamba achungwa na kuswagwaswagwa kama sarakasi katika uzi. Katika hali kama hii, Mulokozi atumia mbinu ya balagha ambapo anakariri kwa kuuliza kwa nini hali yake

ni mbovu hivyo! Hajui kwa nini asumbuka, ateseka, atangatanga, adidimia na kila siku yu safarini hivyo. Yote hayo yamemwandama mtu maskini ndiposa mwandishi aonyesha kwamba mtu kama huyu azaliwapo huwa tayari amekwishaanza kufa. Asisitiza kwa nidaa kuwa haishi bali yupo tu. Anatumia tashibihi anapojiona kama kitu tu, kama kijiwe tu au kama kijiti tu. Aonyesha kukata tamaa anaposema kwamba "labda haipo siku ya wokovu abadan!"

Katika ubeti wa sita Mulokozi awanasihi maskini kwamba siku ya wokovu ipo. Akariri kuwa siku hiyo itafika na itakuwa siku isiyo kifani. Usemi huu wamaanisha kuwa itakuwa siku ya kipekee. Hii ndiyo sababu mwandishi aeleza kwa kutumia taswira kwamba dunia itapinduka na mambo yatasawazika. Picha hii ina maana kuwa hali ya maskini itabadilika kuwa njema. Ametumia usemi kwamba mtu atakuwa "mtu" akimaanisha kuwa unyama na uonevu havitakuwepo tena. Heshima itatang'aa. Pia mwandishi ametumia dhihaka anaposema kwamba miungu ya ukabaila itakufa. Jazanda hii ina maana kuwa wale waliokuwa wakiheshimiwa kama makabaila wakuu hawatakuwepo tena. Huu ndio wakati ambapo mwanadamu atakuwa huru. Huu ni wakati ambapo mwandishi aeleza kuwa "makanisa ya udhalimu yatabomoka na misahafu ya ubepari itafutika." Kanisa ni nyumba maalumu ya kufanyia ibada za wakristo.

Msahafu ni kitabu kitakatifu cha Waislamu chenye mkusanyiko wa sura za Kurani. Kwa hivyo, taswira hii imetumiwa kuonyesha kwamba wadhalimu wa kibepari watang'olewa katika jamii.

Katika ubeti wa mwisho, Mulokozi aendelea kuonyesha kwamba siku ya wokovu itakuwa ya makubwa. Aeleza kuwa itakuwa siku ya ufunuo na ufufuo. Ishara hizi zaonyesha kuwa maskini ataacha kuwapo na kuanza kuishi ambapo kila mtu ataishi. Lakini ili ukombozi huu upatikane, harakati lazima ziwepo kwa kuwa, kwa mfano, siku hiyo ni ya kitimbanga kuanguka na chamchela kucharuka.

## 4.6. SHAIRI: "ENZI ZA MAPAMBANO"

Katika shairi hili, Mulokozi anaonyesha matatizo yaliyoikumba nchi kutokana na hali ngumu ya maisha. Anadhihirisha kwamba uchumi wa nchi umeathiri hulka za watu na kusababisha hekaheka nyingi. Pia abainisha kwamba watu sasa hawajali utu.

Kichwa cha shairi hili ni jazanda inayobeba ujumbe wa shairi zima. Katika ubeti wa kwanza, mwandishi asema kwamba enzi hizi ni za mapambano. Kupambana ni kushindana kwa maneno au vitendo, kugongana kwa nguvu au

kukumbana. Kwa hivyo, mwandishi ametumia taswira hii kuonyesha kwamba nyakati hizi ni za watu kushindana kimaisha.

Ili kueleza jinsi muda unavyokwenda mbio, mwandishi ametumia tashibihi kwamba nukta zinadunda kwa haraka kama pumzi ya mgonjwa anayekata roho, au kama moyo wa kibarua mbele ya meneja. Usemi huu waashiria kuisha kwa maisha ndiposa mtunzi aeleza kwamba hizi ni enzi za jua lielekealo machweo daima. Machweo ni wakati au sehemu jua linapozama wakati wa magharibi. Ni jazanda yenye kueleza ukosefu wa wema maishani kwani tunaelekea kwenye giza.

Katika ubeti wa pili, mshairi asema kuwa mchicha umepanda bei na kauzu wana mchanga. Mchicha ni mmea ambao majani yake hupikwa na kuwa mboga. Kauzu ni mtu asiye na haya. Jazanda hii inaeleza dhana kwamba chakula kimekuwa ghali na watu hawajali matendo yao. Pia mwandishi ametumia jazanda kuwa nyama huliwa na mwinyi na chake huliwa na wazungu. Mwinyi ni bwanyenye apendaye kustarehe. Mzungu ni kitu au tendo lisilo-fahamika. Hii inamaanisha kwamba chakula kizuri sasa huliwa na matajiri. Pia mali ya mtu mnyonge hutwaliwa na watu wenye mienendo isiyofahamika. Hii ndiyo sababu asema kuwa "Namnuuia ngoma ni unga mtupu." Usemi huu waonyesha kuwa chakula cha maskini daima

ni cha aina moja na cha hali duni. Aeleza kwamba kuna mapambano mabarabarani kuonyesha kwamba kuna mashindano ya usafiri na hata utafutaji mali. Ametumia mbinu ya uhuishi anaposema kwamba mavolvo yanafanya fujo mitaani na marenja yanabomoa njia zao za udongo. Hii inaashiria hali ambapo watu tajiri wamevamia sehemu za maskini na kuvuruga hali zao duni za maisha. Wanawafukarisha maskini hata zaidi na kufanya hali zao kuwa ngumu.

Katika ubeti wa tatu, Mulokozi aeleza kuwa kuna mashindano mahotelini, katika mbuga za wanyama, katika mitaa ya kati mchana na mitaa ya pembezoni usiku. Mitaa ya kati ni taswira ionyeshayo watu wenye pato la kadiri ambao huendesha shughuli zao mchana. Mbuga za wanyama ni taashira ya matajiri wanaostarehe mahotelini wanapotalii. Mitaa ya pembezoni ni jazanda ielezayo watu wa pato la chini ambao huendesha shughuli zao kisirisiri na wenye kutenda maovu gizani.

Mwandishi anatumia tashibihi kwamba manywele wametanda kama wimbi la sokota ambapo wanakuja na dola katika dola inayowaabudu na kuleta kanuni mpya ya kuishi kwa watu wasio na maisha. "Manywele" ni jazanda iliyotumiwa kuwadhihaki wazungu. Dola ya kwanza inamaanisha pesa, na ya pili ni taifa. Usemi wa dola inayowaabudu unamaanisha kuwa watu wanawaheshimu. Mwandishi

aonyesha kuwa maisha yamebadilishwa na pesa ambazo zimefanya maisha ya wanyonge kuwa mabaya zaidi.

Katika ubeti wa nne, mwandishi akariri kwamba kuna mashindano vilabuni ambapo bia hazinunuliki. Ametumia taswira ya chibuku kuwa ndio uji wa jioni. Aeleza kwamba polisi huwafumania makabwela na kuwatia kifungoni kwa kunywa pombe haramu.

Katika ubeti wa tano, mwandishi atumia usemi kwamba "siku zimepanda bei" kumaanisha kwamba maisha yamekuwa ghali. Mulokozi asisitiza kuwa kila dakika ni mpwito wa mapambano. Mpwito ni hali ya kuwa na furaha au huzuni kupita kiasi kwa kujiona kuwa wewe ni mmoja katika kundi lililofanya jambo fulani. Mwandishi ametumia taswira hii kuonyesha kwamba mapambano yamewaweka watu katika matabaka kijamii. Vilevile ametumia msemo kwamba kuna mapambano kitandani. Hii ina maana kwamba watu sasa hawaelewani katika maisha ya ndoa. Aidha mwandishi aeleza kwamba dhiki ya mapambano haina kabila. Taashira hii yaonyesha kwamba mvutano wa maisha umepenya kila mahali.

Katika ubeti wa sita, mwandishi aeleza kwamba kuna mapambano kanisani. Ametumia jazanda kuwa "kasisi ataka zaka gwanda limechakaa." Hii ina maana kwamba

padri ataka malipo ya kanisani ili anunue vazi jipya. Vilevile mwandishi ametumia taashira kwamba mbao hazina watu ila wazee na watoto. Inaonyesha kwamba watu wengine wamo mbioni kutafuta riziki na mali. Mbinu ya tashihisi imetumiwa ambapo mshairi asema kwamba sanamu ya Maria imekusanya vumbi. Inaonyesha kuwa watu wamepuuza shughuli za kanisa kwa sababu ya ugumu wa maisha. Hii ndiyo sababu anaeleza kwamba msalaba wa Yesu umepata kutu. Aidha, anakariri kwamba kengele ya Jumapili ni mwito wa mapambano. Taswira hii yaonyesha kuwa badala ya kuja kanisani kusali, watu huwa na shughuli mbalimbali za kukidhi maisha yao.

Katika ubeti wa saba, mshairi aonyesha kwamba kuna mivutano hata shuleni. Ametumia taashira kwamba vijana wagoma kula ugali ulio na wadudu. Pia ametumia takriri kusisitiza neno "amri" kuonyesha kuwa zimeshamiri shuleni. Hali kadhalika ametumia sitiari-fiche anapoeleza kwamba vyuo vimekuwa seminari. Hii ina maana kwamba vyuo vina maongozi sawa na ya seminari. Pia, mwandishi asema kwamba mapenzi hayana nidhamu. Usemi huu una ujumbe kwamba watu sasa hawajiheshimu kimapenzi. Anaashiria kwamba mradi tu mtu amepata pesa, hajali tena heshima zake. Wasichana wako radhi kujivunjia heshima zao kwa ajili ya pesa. Hawajali mtu wanayefanya naye mapenzi. Hii ndiyo sababu anatumia

picha ya Chuo Kikuu kuchua na wazee kuwa ni watoto. Watu sasa hawathamini utu bali pesa pekee. Mwenye pesa ndiye mwenye sauti. Chambilecho wahenga, "mkono mtupu haulambwi, na aliyepeleka mkono kutamalaki si shida." Katika ubeti wa nane, mwandishi atumia dhihaka asemapo kwamba kibwanyenye chafungiwa chooni viwandani. Hii ni jazanda ielezayo kwamba wafanyikazi wadogo huwashika matega wale ambao ni viongozi wasiojali maslahi yao. Pia ametumia usemi wa "mtukula" kuonyesha kwamba kuna shughuli zenye kutumia hongo mipakani. Kuna rushwa ambazo hupokewa ili shughuli zipate kunoka.

Katika ubeti wa mwisho, Mulokozi asema kwamba shida zimepanda bei. Usemi huu umetumiwa kuonyesha kwamba shida zimekuwa nyingi mno. Mwandishi anatumia taswira kwamba maisha yananunuliwa na mauti pia. Picha hii yaonyesha kwamba watu sasa watumia pesa ili kupata kile watakacho. Kunao ufisadi mwingi katika jumuiya. Mtu anaweza kutumia nguvu za pesa kupanda ngazi kazini, au atumie pesa ili kumwangamiza mwenzake. Hii ndiyo sababu mwandishi akasema kwamba hivyo ni vibaya lakini ni vizuri kwa kuwa ndio mwito hasa wa mapambano. Alidhamiria kuonyesha kwamba hivyo ndivyo ulimwengu wa sasa ulivyo. Gharama za maisha zimekuwa juu, kuishi kumekuwa shida na watu sasa hawajali maslahi ya wengine.

## 4.7. KIISHILIO

Uhakiki umeonyesha kwamba watunzi wa mashairi wana mbinu zinazotumiwa kuibusha ujumbe wao. Maudhui ya uchumi katika sura hii yameshughulikiwa kwa mitindo mbalimbali ya lugha yenye kugusa hisi za wasomaji au wasikilizaji. Watunzi wametumia mbinu ambazo zimesaidia kueleza na kutoa ujumbe wao ipasavyo.

## 5.0. SURA YA TANO

## MASUALA MENGINE YA JAMII

### 5.1. SHAIRI: "KISU MKONONI"

Katika shairi hili, Kezilahabi anatoa falsafa yake ya maisha. Anayaona maisha kuwa ni adhabu na tanzia kali iliyo kichomi. Maisha yameonyeshwa kuwa yaliyojaa upweke. Haya yote yanamsukuma mshairi hadi kwenye hatua ya kutaka kujiua kwa kisu hata ingawa mwishoni anaghairi uamuzi huo na kuyakabili maisha vilivyo.

Katika ubeti wa kwanza, mwandishi atumia usemi kwamba wakati miaka inaibwa mmoja mmoja, kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo hawezi. Hii ina maana kwamba kadiri siku zinavyosonga mbele, mtu hana hiari ila kufuata mdundo wa maisha. Hii ndiyo sababu mtunzi anatumia tashibihi kwamba kama gurudumu atajiviringisha. Popote ambapo maisha yatamsukuma, ataenda. Aeleza kwamba ni mtelemko mkali huu. Taswira hii inayamulika maisha kama yenye ghururi, vitisho na yaliyojaa wingi wa ukosefu wa matumaini kwa kuwa mtelemko mkali unaweza kumwangamiza mtu. Hii ndiyo sababu mshairi asema kwamba hajui lini na wapi mwisho wake.

Katika ubeti wa pili, mshairi aeleza kwamba mbele chui mweusi, nyuma mwanga. Chui ni mnyama mkali na mkatili.

Kwa hivyo, Kezilahabi ametumia taswira ya chui mweusi kuonyesha kuwa maisha ya mbeleni yamejaa hatari nyingi zenye maangamizi. Anaonelea kwamba afadhali maisha ya hapo awali ambapo pana mwanga. Watu wangejua la kufanya. Anayaangaza maisha ya baadaye kama yenye kukatisha tamaa. Hii ndiyo sababu anatumia tanakali ya usemi kwamba "Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya dhambi." Anaonyesha kwamba dunia imefurika dhambi za aina mbalimbali ndiposa ameamua kujiua kwa kisu ili asijekumbana nazo. Anatumia msemo wa "maisha kafiri" kuonyesha kwamba binadamu hana hiari. Hii ndiyo sababu anakariri kwamba kutazama nyuma au mbele ni kufa moyo mzima. Hana matumaini yoyote maishani.

Katika ubeti wa mwisho, Kezilahabi aeleza kwamba sasa kama simba-mtu amekata shauri. Mbinu hii ya tashibihi yaonyesha kwamba ameamua kuwa kama simba. Amejipa ujasiri ili ya nyuma sana asiyajali bali ayakabili ya mbele. Asema kwamba atazunguka kwa ujasiri na uangalifu akifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa. "Kamba" ni jazanda yenye kubeba ujumbe kwamba maisha yamemwekea mtu mipaka ya uhuru wake. Kwa hivyo, tashibihi hii yaonyesha kwamba sawa na ng'ombe asiye na uhuru wa kufanya apendavyo, naye pia atazunguka akifuata sera ya maisha kama yalivyo. Hii ndiyo sababu anasema kwamba kila mpigo wa moyo wake ni mpigo wa muziki wa maisha.

Usemi huu unamaanisha kwamba kila afanyalo linaambatana na mdundo wa maisha duniani. Yaani maisha yanafuata mkondo fulani ambao umepangwa na ambao hauwezi kukiukwa. Mwanadamu haonekani kuwa na hiari yoyote katika kuyaendeleza maisha yake. Yanaendeshwa na uwezo fulani ambao mwanadamu hawezi kuutawala. Kwa hivyo, maisha yamepangwa (fated) na ni dhana ya majaaliwa. Mwanadamu hana hiari kwani hatima yake imepangwa tayari.

## 5.2. SHAIRI: "HADIJA"

Kezilahabi ametunga shairi hili juu ya maisha ya ndoa. Anaonyesha msiba wa mke aliyemuua mumewe. Katika shairi hili kuna welekeo wa kukatisha tamaa kuhusu maisha duniani.

Katika sehemu ya kwanza ya shairi, mtunzi asema kwamba Hadija amekata mti mtima na umeangukia nyumba yake. Usemi wa "kukata mti mtima" una maana kwamba Hadija ametenda tendo la kuua. Kuangukia nyumba yake ni taswira ionyeshayo kwamba msiba huo utamrudia yeye mwenyewe. Mwandishi anakariri kwamba Hadija ameziba mto hasira na nyumba yake itakuwa mafurikoni ambapo atahama na kuwakimbia watoto. Mafuriko ni maji yaliyojaa kwenye mto mpaka yakavuka kingo zake. Mwandishi ametumia jazanda ya kuziba mto hasira

kumaanisha kwamba amechochea msiba nyumbani kwake. Nyumba yake kuwa mafurikoni ni ishara ya kukumbwa na matatizo mengi. Kwa hivyo, Kezilahabi aonyesha kwamba Hadija hataweza kukabiliana na shida zitakazomkumba ndiposa aeleza kuwa atahama na kuwakimbia watoto.

Mtunzi ametumia sitiari-fiche anapomlinganisha Hadija na mbuzi aliyetaka kumkimbia chui akajigeuza panya ambaye alilia kuliwa na paka. Jazanda hii yaeleza dhihaka ya mwandishi anayemkebehi Hadija kwa kumuua mumewe kwa shauri ya tamaa. Sasa badala ya kupata wema alioutarajia, amekumbwa na adhabu kali zaidi ambapo mwisho wake ni kuteseka na kuangamia. Pia, mwandishi anambeza Hadija kwa kutumia taswira ya mchawi aliyetamani sana kutisha watu na akajigeuza kuwa simba ambaye alilia na risasi kichwani. Anamsuta Hadija kwa tamaa iliyomkosesha akatenda unyama wa kuua mumewe. Kule kutaka kuonekana bingwa kumemfanya akose salama.

Hali kadhalika, mwandishi ametumia jazanda ya jongoo kutaka sana kukimbia aliomba miguu elfu akaachwa na nyoka. Hii ina maana kwamba tamaa aliyokuwa nayo Hadija imemletea mkosi ambapo badala ya kufurahia tendo lake, amebaki kusononeka. Hawezi kuona wema wowote na amebaki akihangaika tu.

Katika ubeti wa mwisho, Kezilahabi anatumia mbinu ya balagha ambapo anamwuliza Hadija atakakokwenda kwa kumpa bwanake sumu. Anatumia taswira ya kumshika nyoka kwa mkia kuonyesha kwamba ameyahatarisha maisha yake mwenyewe. Hii ni kwa sababu mtu amshikapo nyoka mkia huwa amemchokoza na ana hatari ya kuumwa na kuuawa. Vilevile mwandishi ametumia taswira ya kupita nyuma ya punda kusisitiza dhana kwamba Hadija amehatarisha maisha yake kwani kuna hatari ya kupigwa teke na kudhuriwa au kuangamizwa na punda. Dunia itamwangamiza.

Kwa hivyo, mwandishi ameonyesha hali ya kukosa matumaini. Hadija ni kielelezo cha wanawake watendao unyama wakitarajia wema, lakini mwandishi amebainisha kwamba hawana salama. Pia, Hadija aweza kuwa jazanda ya watu ambao huwatendea wenzao maovu wakitarajia wema. Ni heri kutosheka na kile ulicho nacho kuliko kuongozwa na tamaa ambayo itakuja kukuangamiza.

## 5.3. SHAIRI: "HATIMA YA KILA MWALI"

Shairi hili limetungwa juu ya kifo. Mulokozi anaonyesha kwamba kufa ni jambo la kawaida na kwamba hakuna haja kusikitishwa nacho kijapo. Pia anaonyesha kuwa maisha ni jambo ambalo kama lilivyo na mwanzo, lazima liwe na mwisho pia. Kichwa cha shairi ni taswira ambayo imetumiwa kuonyesha hatima ya maisha ya mwanadamu.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi asema kuwa mtu asihofu kamwe kuondolewa kabla ya kuvaa kofia ya pili. Kuondolewa ni usemi wenye maana ya kufa. "Kuvaa kofia ya pili" ni jazanda inayoeleza dhana ya kufikia hatua nyingine maishani. Kwa mfano, kuwa mtu mwenye cheo au kuoa. Anaeleza kwamba yeye ni mwanamwali ambaye alichumbiwa siku ile mama alipomzaa. Mwanamwali ni msichana ambaye amekwisha baleghe lakini bado hajaolewa na aghalabu hajapoteza ubikira wake. Uchumba ni makubaliana ya pande mbili baina ya mwanamke na mwanamume wanaotaka kuoana. Kwa hivyo, jazanda hii yaonyesha kuwa mtu hupangiwa siku yake ya kufa wakati ule anapozaliwa.

Katika ubeti wa pili, mwandishi akariri kwamba yeye ni mwali na hivyo anajua kuwa hatima yake asilia ni kuolewa na kuacha ndugu pamoja na wote anaowajua. "Mwali" ni jazanda ya kumaanisha mtu, na hatima yake asilia ni usemi unaomaanisha desturi au kawaida ya mwisho wake. "Kuolewa" ni jazanda inayoeleza dhana ya kufa. Kwa hivyo, Mulokozi alimaanisha kwamba akiwa mwanadamu, anajua kwamba kama desturi mwisho wake ni kufa na kutengana na ndugu pamoja na wale wote anaowajua. Anatumia taswira ya kuchukuliwa ng'ambo ya pili akimaanisha kwenda ahera.

Katika ubeti wa tatu, mshairi akariri kuwa huko ng'ambo ya pili ndiko anakoambiwa nyanya zake walikoolewa naye angefurahia kwenda huko japo kiza totoro kimepajaa. "Nyanya" ni jazanda inayoeleza wale waliotangulia kufa. Pia mwandishi ametumia onomatopea ya "kiza totoro" kuonyesha kwamba hakuna ajuaye hali ya kule waendako watu wanaokufa (Kuzimuni).

Katika ubeti wa nne, Mulokozi aeleza kwamba kimila, jioni jua likivia, mchumba huja kumchukua mkewe, na hapo mwali huabiria mashua ambapo harudi tena akisha twaliwa. "Kimila" ni usemi unaomaanisha kidesturi; "jioni jua likivia" ni taswira inayoonyesha kwamba uhai wa mtu unapokumbwa na matatizo yasiyo na suluhisho. "Mchumba" ni jazanda yenye maana ya kifo au mauti. "Kuabiria mashua" ni usemi unaomaanisha kufunga safari kwenda ahera, yaani kufa. "Harudi tena akishatwaliwa" ni usemi wenye maana kwamba mtu harudi akishakufa. Kwa hivyo, mwandishi ametumia mbinu hizi kumaanisha kwamba kwa kawaida, hali ya mtu ififiapo, kifo humchukua ambapo harudi.

Katika ubeti wa mwisho, mwandishi aeleza kwamba anakaa akitambua kuwa mumewe atakuja jioni kumtwaa. Taswira hii ina maana kwamba yeye anajua kuwa mambo yawapo mabaya, yeye anakaa akijua kwamba kifo kitamchukua.

Anakariri kwamba anajirembua, anajikwatua na kujiandaa kwa harusi yake. Taswira hii inaonyesha kwamba yeye anakaa akijitayarisha kwa siku yake ya kufa.

Kulingana na mwandishi, kifo ni mwisho wa maisha tunayoishi duniani. Amebainisha kwamba msichana mzuri tumwonaye akimeremeta twamwona mwishowe akiwa amezeeka na sura yake nzuri ikiwa imechuchuka. Kwa hivyo, binadamu azaliwaye hana budi kufa hatimaye.

## 5.4. SHAIRI: "WIMBO ULIOSAHAULIKA"

Shairi limetungwa na Mulokozi juu ya utamaduni. Anasuta kuabudu mambo ya kigeni. Anaonyesha kwamba hali kama hiyo husababisha utumwa na kujidunisha wenyewe. Kwa hivyo anatoa hatua za kuchukuliwa katika kurudia utamaduni asilia na kutupilia mbali kujidharau. Kichwa cha shairi ni taswira inayobeba ujumbe wa shairi zima.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi aeleza kuwa atauimba wimbo wa kale uliosahaulika. Usemi huu unamaanisha kwamba atafuata utamaduni asilia ambao umesahaulika. Anakariri kwamba atauimba wimbo wa jandoni na kucheza manyanga kwa mchagisho wake. Taswira hii yaonyesha kwamba ataufuata utamaduni wake katika ukale wake.

Katika ubeti wa pili, mwandishi anaudhihaki utamaduni wa nje kwa usemi kwamba"atajitakasa na najisi hii inayonuka, matope yanayochubua ngozi yake, mitishamba ya kigeni inayoukwajua mwili wake, dondandugu linaloitafuna roho yake, na ukoma unaoihusuru nafasi yake." Kutakasa ni kufanya kuwa safi. Najisi ni kitu au uchafu wowote unaotengua tohara, au unaoweza kumkirihi mtu. Kwa hivyo, taswira ya "kujitakasa na najisi inayonuka" ni kuonyesha hali ya kuepukana na kufuata mambo asiyoyaelewa vizuri. "Matope yanayochubua ngozi na mitishamba ya kigeni inayoukwajua mwili wake" ni jazanda zinazomaanisha madawa ya kigeni kama vile Ambi ambayo inatumiwa na baadhi ya Waafrika ili kujaribu kuondoa "aibu" ya weusi wa ngozi zao na kuwafanya wawe weupe kama Wazungu. "Dondandugu" ni usemi unaomaanisha donda lisiloweza kupona. Mwandishi ametumia jazanda hii kuonyesha madhara yampatayo mtu afuataye vitu vya kigeni bila kujua. Huwa kama mtu mwenye ugonjwa usioweza kupona. Ukoma ni ugonjwa wa mabatomabato ambao unaharibu na kukata viungo vya mwili. Mwandishi ametumia jazanda hii kusuta wale watumiao virembesho vya kigeni ambavyo huwaletea maradhi mabaya na kuhusuru nafasi zao maishani.

Katika ubeti wa tatu, mwandishi aendelea kukariri kwamba ataukata mnyororo wa utumwa unaoning'iniza talasimu za kigeni shingoni pake. "Talasimu" ni kipande cha karatasi au ngozi kilicho na maandishi maalumu ambacho huangikwa ukutani au mlangoni na ambacho huaminiwa na baadhi ya watu kuwa ni kinga ya madhara. Mwandishi ametumia taswira hii kudhihaki tabia ya kuwa mtumwa mwenye kufuata dini na imani za kigeni zinazomfanya mtu kukosa uhuru nchini au kwake nyumbani. Hii ndiyo sababu anasisitiza kwa usemi kwamba atakataa kuzainiwa na uwongo wao na kutetemeshwa na mizimu asiyoijua. Hapendi kushawishiwa na chochote cha kigeni ili atende uovu. Ametumia takriri kwamba hataingia kumbi zao wala kushiriki katika ufasiki wa ngoma zao.

Kuanzia ubeti wa nne hadi wa saba, dhamira ya Mulokozi ni kuhimiza utamaduni wa kiasili. Katika ubeti wa nne, anatumia taswira ya kujifunga 'kishenshe' kiunoni, kujifunga lubega kwa fundo la jadi na kuchukua ngao na mkuki kutetea hadhi ya mababu kuonyesha Uafrika katika uasili wake. Ametumia usemi wa kujikatia njia katika safu zao hadi ng'ambo ya pili penye mbuyu wa mahoka kumaanisha kufuata hulka ya mababu kwa itikadi za kiasili.

Katika ubeti wa tano, mwandishi aendeleza ujumbe wake kwa taswira kwamba atatambaa kwa tumbo lake kuuendea mbuyu umwitao na kusujudu kwa moyo wa toba chini ya ngao ya mikono yake iliyonyooshwa kumkumbatia. Hii ina maana kwamba atajinyenyekeza mbele ya miungu ya kiasili inayomhitaji na ambayo itampa hifadhi inayo-takikana.

Katika ubeti wa sita, mwandishi ametumia takriri ya "kurudia mizimu ya kiasili kwenye mbuyu" ambapo pana ala za kiasili kama vile ngoma, simbi takatifu, mikia, tunguni za ajabu na damu ya baraka ieuayo. Pia akariri kufuata uasili kwa taswira kwamba atacheza na kufanya miujiza yote ya kale chini ya moto uchangamshao chini ya mbuyu. Anaonyesha matumaini mema kwa taswira kwamba atacheza ngoma kuu ya zamani na kufarij ika. Hii ina maana kwamba utamaduni wake ndio ridhaa kamili. Kucheza ngoma kuu ya zamani ni msemo wenye maana ya kufuata utamaduni asilia.

Katika ubeti wa mwisho, Mulokozi ametumia tashibihi anapoeleza kwamba atawasihi wahenga wa ukoo wake kuteua Beberu mweupe mwenye ndevu,ambaye sufu yake i kama theluji,ambaye pembe zake zi kama meno ya ndovu ili wamlete penye madhabahu yaliyosahaulika penye shina la mbuyu. Hii ni taashira yenye kubeza utamaduni mgeni na angependa kufanya tambiko ili apate kuokolewa.

Anakariri jambo hili la kutoa kafara ili apate kutakaswa na kutusi ambalo ni masalia ya ustaarabu uliokufa. Taswira hii yaonyesha dhihaka ya mtunzi kuhusu utamaduni wa kigeni ambao amechukizwa nao na kuuona kama kwamba unanuka. Ameumulika kama ustaarabu usio hai tena.

Katika shairi hili, mwandishi anasisitiza kutupilia mbali utumwa wa kufuata utamaduni wa kigeni ili kuurudia utamaduni wa Mwafrika bila kujidharau.

### 5.5. SHAIRI: "HABARI MPYA"

Katika shairi hili, Kahigi anaonyesha nafasi ya dini katika maendeleo ya jamii. Haamini kuwa dini ina nafasi yoyote muhimu katika maendeleo ya jamii. Anamkejeli Mungu na kuhimiza tujitegemee wenyewe katika kuleta maendeleo yetu. Kichwa cha shairi ni taswira inayobeba ujumbe wa shairi zima.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi ametumia msemo kwamba "dunia ni mja mzito wa maovu." Hii ni taashira ya kutokea maovu mengi duniani. Pia anakariri kwamba yafaa kuchomwa moto kwani wokovu waupatao watu ni haba. Taswira hii ya mwandishi yaimulika dini kama taasisi ambayo yafaa kubomolewa. Maoni haya ni sawa na ya Mulokozi anaposema kwamba hakuna Mungu. Waandishi

hawa wawili wanaamini kuwa dini haihitajiki katika jamii mpya tunayojenga. Mwandishi wa shairi hili haoni wokovu wa maana waupatao watu. Hii ndiyo sababu anaibeza dini kwa msemo kuwa "wengi wetu hatuukumbati fuadini katu." Hii inaashiria kwamba watu hawatilii maanani imani zao. Kuna unafiki na uzandiki mwingi.

Mwandishi anakariri kwamba hawamhitaji Mungu wala wokofu. Anatumia msemo wa "kubwata bila hofu" kuonyesha madharau. Ametumia taswira ya ukosefu wa Mungu mtukuka ambaye eti kesha kufa kuonyesha kwamba tusimtegemee Mungu kamwe. Vilevile ametumia msemo kwamba "majuto ni mjukuu" kumaanisha kwamba watu watakuja juta baadaye.

Katika ubeti wa pili, Kahigi ametumia mbinu ya uhuishi anaposema kuwa kanisa lilizima pumzi. Hii ni ishara ya mshangao mkuu kijana mmoja alipokufuru maadili ya dini. Mwandishi anasisitiza kwamba dini imejaa uongo na maovu kwa usemi kuwa "Dini ni mja mzito wa uongo na maovu!" Pia ametumia taswira ya "ushirikina uliowatia wengi makovu" kudhihaki dini na kuonyesha kwamba ni imani ambayo ni ugonjwa au ndwele kwa jamii. Hali kadhalika, anatumia taswira ya "gofu la taasisi linalojikongoja" kuonyesha kuwa ni taasisi kuukuu isiyo na maana. Aidha, amebeza dini kwa usemi kwamba ni "Fikira na maendeleo ya mtu kufuja." Hii ina maana kuwa dini

huharibu fikra za watu na kukwamisha maendeleo.

Kahigi anakariri kwamba yafaa kuchomwa moto kwani uwongo huu umewaangamiza wengi. Anaeleza kuwa watu wanaukumbata kwa kiruu, unawapofusha, unawapumbaza na kuwalemaza. Usemi huu unawasuta waumini ambao hufuata dini bila kudadisi chochote ambapo mwishowe mwandishi aonyesha kuwa hukosa mwelekeo, wakaduwaa na kukwama maishani.

Vilevile, mwandishi ametumia takriri anaposisitiza kwamba wokofu wa mtu hautoki mbinguni bali hapa duniani. Anaeleza kuwa vitisho vya Jahanam siku zake si hizi. Anakariri kwamba siku hizi ni za zinduko na mapinduzi. Usemi huu unaashiria kwamba dini kwa sasa zinazorotesha maendeleo ya jamii. Pia mwandishi anawachochea watu kubadili maisha yao duniani huku wakijua kuwa hakuna maisha baada ya kifo. Anapinga dhana ya dini kuwaambia watu kuvumilia maovu wanayotendewa ati kwa sababu watapata heri yao mbinguni. Aonelea heri hiyo ije hapa duniani wakati tunaishi. Mawazo haya yameungwa mkono na Mulokozi katika shairi "Mimi ni Nani?" katika Malenga Wa Bara. Katika ubeti wa tatu, mwandishi ametumia tashihisi anaposema kuwa "kanisa likazima pumzi kwa kimako kikuu." Hii ni ishara ya mshangao mkuu. Pia ametumia tanakali za sauti anaposema kuwa "kasisi macho matumbwi kawayawaya... Pumzi kote twii." Hii ina maana kwamba kasisi alizirai.

Aidha, mwandishi ametumia tashihisi anaposema kwamba kanisa likashikwa mashaka. Hii ni ishara kwamba waumini walihuzunika.

Katika ubeti wa nne, mwandishi aendelea kukariri kwamba kanisa lilinyamaza. Ametumia taswira ya kutanda wasiwasi baridi kuonyesha hofu ya watu wasiojua la kufanya. Pia ametumia usemi wa "kuhofu jicho la kifo" akimaanisha kuogopa kushuhudia mtu akifa. Aidha ametumia usemi wa "vilio vya wanawake na watoto vikaanza kupa-hinikiza pahali" akimaanisha kuwa watoto kwa wazee walilia kwa sauti kuu.

Katika ubeti wa mwisho, Kahigi ametumia tashihisi anaposema kuwa radi ikanguruma. Hii ni taashira ya kutokea habari ya ajabu ndiposa anatumia taswira kwamba umeme ukafyatuka na mvua kunyesha . Mvua ni ishara ya ustawi. Habari mpya ambazo ni za kushangaza na zenye kukufuru Mungu zilikuwa zimetangazwa kanisani. Mwandishi ametumia taswira ya "kusikika ng'ambo" akimaanisha kusikika mbali.

## 5.6. SHAIRI: "KARIBU NDANI"

Shairi hili limetungwa na Kezilahabi juu ya mgogoro katika ushairi wa Kiswahili. Anawasuta

wanamapokeo ambao hoja zao zina upungufu fulani. Aonyesha kuwa utunzi mpya ni mchango katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Hivyo, wanamapokeo hawana sauti tena katika taaluma inayopanuka sasa.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi aeleza kuwa washairi wa mapokeo sasa "wacheza lalasalama." Taswira hii yaonyesha kuwa siku zao zinayoyoma. Hii ndiyo sababu asema kwamba wanacheza lalasalama katika mionzi hafifu ya jua machweoni. Pia mwandishi aeleza kuwa mahadhi yagaagaa juu ya bahari ya utenzi na yameshindwa kuzama chini kwenye kina cha urazini. Taswira hii yaonyesha kwamba hoja za wanamapokeo hazina mashiko kitaaluma ambapo zimekosa mantiki katika sanaa ya utunzi. Hii ndiyo sababu anasema kuwa wahenga hawatoki vibandani, na hakuna tena ngoma ya kugeeana kani, na ushairi umehama kurudi upeponi. Jazanda hii inawakebehi washairi wa awali ambao sasa hawaafikiani. Uwanja wa ushairi sasa u wazi na yeyote aweza kutunga shairi kwa mbinu mpya.

Mwandishi ametumia taswira ya "majani makavu yasiyotingizika" kuonyesha waandishi wanamapinduzi ambao wako imara. Ametumia jazanda ya madirisha ya nyumba kufungwa imara huku waliomo ndani wahofu hasira ya muzimu kumaanisha kuwa wanajadi wamekazania

arudhi wakihofu kwamba zisipofuatwa, "utamaduni" wa utunzi utakuwa umekiukwa.

Katika ubeti wa pili, mtunzi asema kuwa muda si mrefu patakuwa kiza totoro. Onomatopea hii yaashiria kwamba hivi karibuni, wanamapokeo watasahaulika. Ametumia jazanda ya wanyama wa usiku kutawala taswira akimaanisha kuwa watunzi kutoka sehemu zisizo asili ya Kiswahili wataingia uwanjani. Hii ndiyo sababu anaeleza kwamba atauingia msitu kwenye kiza cha karne pasipo vichochoro mkato. Taswira hii yaonyesha kuwa yeye ni miongoni mwa watunzi wapya ambao wanuia kuandika kwa mbinu mpya katika nyanja hii ya kizazi kisichojulikana ambapo hapana njia rahisi.

Mwandishi atumia usemi kwamba akiwa na nanga yake, atatongoa nyimbo mpya. Hii ina maana kwamba ana sababu ambazo zitamkinga dhidi ya mashambulizi kuhusu utunzi mpya na atatunga mashairi yake akitumia silika ya uzawa. Ametumia taswira ya "kuupata mwelekeo maana ushanga wa shingoni bado hajautupa." Hii inaonyesha majisifu yake kuwa alizaliwa na kipawa cha kutunga ambacho kitamwezesha kuukabili uwanja huu mpya.

Katika ubeti wa tatu, Kezilahabi atumia nidaa kuonyesha kwamba amekumbana na "kibanda" ghafla. Kibanda

ni jazanda ielezayo dhana ya utunzi usiofuata arudhi. Hii ndiyo sababu anatumia taswira ya "mlango mmoja ulio wazi na ndani mna moto unaowaka." Hii yaashiria kwamba uwanja wa ushairi u wazi, lakini kuna mgogoro mkali wa kutisha. "Mlango mmoja" ni jazanda ya wanavina wanaosisitiza kwamba shairi ni shairi lifuatapo arudhi za utunzi. Hii ndiyo sababu mtunzi abisha hodi kwa wenyewe akisema kwamba yeye ni kichwa-maji anayetafuta njuga zake na lile vazi la kindu ingawa hana ubuyu, lakini aja kukesha nao. Usemi wa "kichwamaji" waashiria kuwa yeye ni mkaidi wa arudhi. Njuga na kindu ni taswira ionyeshayo ala za utunzi. "Ubuyu" ni jazanda ielezayo dhana ya kufuata arudhi. Kukesha ni ishara ya kujumuika katika utunzi.

Katika ubeti wa nne, mtunzi aeleza kuwa kibanda kuukuu kimekaribia kuanguka ambapo mhimili wake mmoja umeanza kukatika. "Kibanda kikuukuu" ni jazanda ya tapo la watunzi wanaosisitiza arudhi. Mhimili ni kitu kinachozuia kingine kisianguke. Ni nguzo au mwimo. Kwa hivyo, hii ni jazanda inayoeleza kwamba sababu wanazotoa wanamapokeo zimeanza kukosa mashiko na hivi karibuni zitakuwa chapwa. Anatumia taswira ya "mchwa wanaolialia ambapo paa si paa tena" kuonyesha kwamba kuna watunzi wapya ambao wamevamia sababu wanazotoa wanamapokeo na kuziraruararua. Usemi huu una maana kwamba watatupilia mbali hoja hizo na hivyo, kutupilia mbali

kusisitiza utunzi wa arudhi. Mwandishi ametumia taswira ya kigoda kikubwa kuwa karibu na mhimili huo ambacho kina umbo la chui huku mbele kuna moto na vijinga vyake mifupa. Hii inaashiria kuwa hoja za wanajadi haziegemei popote japo zinatisha. Hata hivyo, moto ni ishara ya kuziteketeza na kuziacha magofu tupu.

Katika ubeti wa tano, mwandishi ametumia taswira ya kutundikwa ala nyingi za muziki ukutani mwa kibanda. Hii yaonyesha kuwa kuna miundo mingi ya utunzi katika uwanja wa ushairi. Kezilahabi anawabeza wanamapokeo kwa usemi kwamba"pamekaa vizee kimya, vichwa vyao vimeinama chini kifikra vyatazama." Anatumia jazanda ya ajuza anayeinua kichwa karibu na mhimili akimaanisha mmoja wa wanamapokeo. Pia ametumia tashititi ambapo anasema kwamba "mbwa ghafla ainuka akibweka huku meno mdomoni hana, lakini povu lamfura." Taswira hii yaonyesha kuwa kulitokea mwanajadi aliyekaripia utunzi wa kisasa (ushairi-huru) kwa hamaki lakini bila sababu zenye mashiko. Ukosefu wa meno ni ishara ya ukosefu wa hoja zenye athari yoyote. Hii ndiyo sababu Kezilahabi akariri kuwa "Vizee vingine vilishtuka na kuinua vichwa vyao kwa macho makali yakitua usoni pake." Hii ina maana kwamba wanamapokeo walimtisha.

Taswira ya kumshauri mwanavina kulala chini yaonyesha kuwa kulikuwa na haja kwa wanajadi kutoendelea

kung'ang'ania hoja zao za kijadi. Hii ndiyo sababu mwandishi aeleza kuwa ajuza alimuasa "Wa Vina" huku akimtazama kwa makini, akichunguza kimya. Taashira ya ajuza ni kuwa mabadiliko ni jambo lisiloweza kukwepeka.

Katika ubeti wa sita, mtunzi atumia taswira ya kukaribishwa ndani na kuambiwa kuwa hajawa mgeni. Hii yaonyesha kuwa utunzi wake wa ushairi-huru ulikubaliwa katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili kwani hakuwa limbukeni katika utunzi. Ametumia usemi kwamba: "Tumekuwa tukikusubiri, ingawa umefika mapema." Hii yaonyesha kwamba utunzi "mpya" ulikuwa ukitarajiwa ingawa ulijiri mapema zaidi. Hii ndiyo sababu asema kuwa alikuwa ndani ya duara akinaswa nasika. Alikuwa miongoni mwa watunzi maarafu ndiposa asema kwamba:

> Ulipo umezingirwa, kumbukumbu zilokufinyanga.

Mwandishi ametumia taswira ya hapo kuwa ndipo aliposafisha fizi zake kwenye titi la mama ambaye ni mbwa aliyemlamba kidevu chake, na hizo kuwa ndizo nyuso zilizopima hatua zake. Taashira hii yaonyesha kuwa ushairi-huru umekuwa maendeleo ya ushairi wa wanajadi waliomlea mtunzi. Hii ndiyo sababu anaambiwa kuwa "juu ya hili paa, palitupwa meno yako."

"Kitovu cha utambulisho" ni usemi wenye maana kwamba mshairi huyu alikuwa nguzo ya utambulisho kwani ushairi-mpya unakuja. Anakaribishwa ngomani ili afunge

fundo la kitali. Jazanda hii yaeleza kwamba Kezilahabi angeingia katika uwanja wa utunzi wa mashairi na kukomesha "vita" vya mgogoro katika ushairi wa Kiswahili.

Katika ubeti wa saba, Kezilahabi atumia usemi wa "kuwa na ala" kumaanisha fani ya utunzi ambao tenzi zake zakumbukwa. Aonyesha kwamba mgogoro umefika mbali. Aeleza kuwa nyimbo za wanamapokeo ni nzuri na zina mahadhi na mdundo. Pia zinatia hamasa. Hii ni taashira ya kukubali utunzi wa kimapokeo. Mwandishi ametumia usemi kwamba "zilitulaza usingizi mapema mno ikawa kama kwamba Mungu alitusahau." Hii inaashiria kuwa ziliwafanya kuamini kuwa ndizo pekee zinazofaa. Hali hiyo ilikwamiza maendeleo ya utunzi wa mashairi ya Kiswahili katika umbo lisiloweza kubadilika. Hii ndiyo sababu Kezilahabi aambiwa kwamba "nyimbo zake zimezindua taaluma, mlango sasa u wazi na wajao wafuate nyayo." Picha hii yaonyesha kwamba mashairi ya Kezilahabi yalifungua ukurasa mpya katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili ambapo sasa watu wengine wako huru kutunga kwa miundo yao wakifuata mfano wake.

Katika ubeti wa nane, mwandishi atumia jazanda ya "kuchagua ala moja na kukaa juu ya kigoda" kumaanisha kuchagua muundo mmoja wa utunzi na kuendeleza uwanja huo. Ametumia taswira ya kuwa na hamu ya kucheza ili kupata kukoga karne, kuonyesha kuwa kuna ari ya kutungia

mitindo mipya ili kufurahisha kizazi cha karne hii kitakachojivunia utunzi mpya.

Katika ubeti wa tisa, anawadhihaki wanajadi waliofurahia utunzi wake ambao ametumia msemo kwamba uliwatonesha vidonda vyao vya hisia. Hii ina maanisha kinaya ambapo wazee waonyesha kufurahi lakini wakumbushwa uchungu wa awali. Anawakejeli wanajadi kwa usemi kuwa kizee kimoja kilipiga kelele kwa kukariri kuwa "Huu ndio mdundo wenyewe, ngoma ya watu wazima." Anatumia takriri kuonyesha mshangao anapokariri neno "Ai!" kuonyesha dhihaka na vilevile mshangao wa utunzi mpya.

Katika ubeti wa kumi, mwandishi atumia mbinu ya nasiha anapotumia msemo kuwa "moyo wako uwe mgumu kuwakabili wahakiki." Hii ni ishara ya kujishajiisha maoni ya wahakiki yasimtishe kwa mujibu wa utunzi mpya. Anatumia taswira ya "kufumba macho vile wanavyoyeyeuka" kuonyesha dhihaka dhidi ya wanajadi ambao wameona aibu kutokomea mbali sasa.

Katika ubeti wa kumi na moja, mwandishi ametumia jazanda ya "mlio wa simba" kuonyesha kuwa yeye ni bingwa. Hii ndiyo sababu atumia taswira kwamba wanyama kila upande waliinamisha vichwa vyao alipopita kati. Ana maana kwamba aliheshimiwa kulingana na utunzi wake.

Hii ndiyo sababu aeleza kwamba alipoacha msitu, alitazama nyuma na kumwona mbali "Mavina" akitangatanga msituni. Hii ni jazanda yenye kukejeli wanavina ambao waliachwa bila kujua la kufanya. Wamebaki kuhangaika mahali palipotengwa.

## 5.7. KIISHILIO

Katika sura hii uhakiki wetu umeonyesha kwamba mtindo wa mtunzi unaweza kufanya mawazo yake yaguse hisi za msomaji au msikilizaji kutokana na matumizi muafaka ya lugha. Pia, imebainika kuwa maudhui ya msanii yana istilahi na msamiati maalumu. Uchambuzi wetu umedhihirisha upekee wa lugha iliyotumiwa kuibusha maudhui na dhamira za washairi kwa namna muafaka zaidi. Chambilecho Senkoro (1988:vii):

> Ushairi ni aina ya fasihi inayotofautiana na hadithi na tamthilia hasa katika umbo na matumizi yake ya lugha... ushairi hutumia lugha ya mkato yenye kueleza maudhui yake kimuhtasari na aghalabu huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara.

Katika uchambuzi, sifa anazozitaja Senkoro zimethibitishwa. Kwa hivyo, ijapokuwa mashairi-huru hayafuati arudhi za kimapokeo, umbo wa ndani ni sawa na ule wa wanamapokeo tukizingatia matumizi ya lugha. Tunaafiki

maelezo ya Kezilahabi (1974:xv) kwamba:

> Mawazo yaliyomo katika ushairi wa aina yoyote huonekana kama shilingi iliyo majini, lakini kuipata shilingi hiyo msomaji asipeleke mkono wake wima tu bali lazima apige mbizi...

Hivyo ndivyo kazi yetu inavyotuelekeza.

6.0. SURA YA SITA

## 6.1. HITIMISHO

Kutokana na uchambuzi ambao tumefanya kuhusu dhamira na mtindo katika mashairi-huru, imebainika kwamba mashairi-huru ni mashairi ya Kiswahili. Dhamira za watunzi zimejikita katika kila nyanja ya maisha ya binadamu ambapo falsafa zao zimedhihirisha mtazamo pamoja na msimamo wao kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Tumeona kuwa dhamira ya mtunzi na mtindo anaoutumia katika kutoa ujumbe wake ni vipengele vinavyotegemeana. Hatuwezi kamwe kutenganisha lugha na ujumbe. Ni kama pande mbili za sarafu moja. Msanii anapofikiria juu ya ujumbe fulani, anafikiria pia juu ya lugha atakayotumia ili kuuendeleza ujumbe huo ukaifikia hadhira vile anavyotarajia. Kwa hivyo, mtunzi hutumia lugha kuibusha mawazo yake katika kazi yake na ndiyo njia aitumiayo kuyaeleza mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya kubuni.

Kulingana na nadharia yetu, lugha husaidia kutoa ujumbe wa mwandishi kwa hadhira iliyokusudiwa. Uchambuzi umeonyesha kwamba mtindo wa mwandishi huathiri namna anavyotoa ujumbe wake. Ni kupitia kwa lugha na mtindo ndipo tunapopata mguso. Ni kupitia mbinu kama hii ambapo hadhira itahisi tajriba, mtazamo na mwelekeo

wa msanii kuhusu swala analolishughulikia. Pia tulipata kwamba kuna uwiano kati ya fani na maudhui. Uwiano huu waweza kusemwa kuwa ndio "uti wa mgongo" wa ushairi na hata fasihi nzima kwa jumla. Aidha, tulipata kwamba mawazo yanayozungumzwa na msanii katika utunzi wake huathiri jumla ya vipengele vya lugha anayotumia katika mpangilio mahsusi ili kutoa maana fulani. Hali kadhalika, tumeona kuwa shairi linaweza kuwa halijafuata mpangilio uliozoewa na wanamapokeo, lakini athari ya mguso ikaletwa na vipengele vingine kama vile picha, takriri na sitiari.

Tasnifu yetu yaonyesha kwamba mtindo ni muhimu katika kueleza jinsi msanii alivyoteua maneno yake; namna alivyoyapanga katika kujenga ujumbe wake. Kupitia kwayo, dhamira ya mtunzi hubainika kwa sababu lugha yake itaonyesha mwelekeo wake. Katika shairi kila kitu kinao uhusiano na kingine ambapo umuhimu pamoja na maana ya shairi hilo hutegemea uhusiano uliotokana na vipengele mbalimbali vya shairi hilo. Kwa hivyo, vipengele vya shairi kama vile sauti, maneno, misemo, taswira na tamathali nyinginezo hupewa umuhimu kutokana na jinsi vimeundwa au kutumiwa katika shairi.

Uchambuzi wetu wa dhamira na mtindo katika mashairi-huru umetusaidia kuielewa jamii inayohusika. Imebainika kwamba mazingira ya mwandishi katika ujumla wake huathiri uteuzi wake wa lugha na mitindo anayotumia.

Vile vile misingi na mikondo ya historia ya jamii huipa fasihi umbo kimaudhui na kifani pamoja na mwelekeo. Tunaafiki maoni ya Kahigi (1975:3) kwamba watu wenye mtazamo halisi wa kisayansi huangalia ushairi wa Kiswahili au fasihi ya Kiswahili kama vitu viwezavyo kubadilika kifani na kimaudhui kufuatia mabadiliko ya kimfumo katika jamii. Hivyo, mhakiki hana budi kuzingatia mazingira ya kijamii ili kugundua vipengele vinavyoihuisha kazi fulani. Pia ushairi kama kazi ya sanaa utaeleweka na kuthaminiwa vyema zaidi katika mazingira ya wakati maalum wa kihistoria. Hii ina maana kwamba fasihi, ukiwemo ushairi, hupata uhai wake kutokana na hali halisi za jamii. Kwa hivyo, fasihi ikiwa ni zao la jamii, matukio makuu ya kipindi fulani yanaweza kutambulika kutokana na fasihi ya wakati huo. Ushairi-huru ni mfano kama huo wa fasihi kama taasisi ya jamii inayoonyesha maendeleo.

Dhamira ya mwandishi hutokana na mazingira yake ambayo humpa tu msukumo wa kutunga shairi ili apate kutoa falsafa yake pamoja na hisia. Shairi hupata maana na umuhimu wake sio kutokana na umbo lake la nje bali pia matumizi ya lugha katika kujenga dhamira ya mwandishi. Kwa hivyo, uchambuzi wa lugha ndio unaodhihirisha sifa za ndani za shairi na kuonyesha kwamba upekee wa shairi umo katika kunga za lugha

zilizotumiwa.

Kwa kutumia nadharia yetu, imebainika kwamba mgogoro kuhusu maana ya shairi la Kiswahili haupaswi kuwepo. Wanajadi wanapaswa kutumia vigezo vyote vinavyohusisha sifa zote za ushairi wala sio kipengele kimoja tu. Uchambuzi umeonyesha kwamba shairi lina sifa za kimtindo za kipekee, na kuwa umbo la ndani la shairi ndilo muhimu katika kuainisha utanzu huu wa fasihi. Aidha, kauli ya wanajadi kuwa shairi la Kiswahili sharti lifuate arudhi za kimapokeo ni mtazamo finyu wa ushairi na fasihi nzima kwa jumla. Hivyo basi isiwe kwa wahakiki na wasanii kukemeana kijazba. Ni muhimu kuelewa kwamba fasihi, kama taasisi nyingine za jamii zilivyo, haina budi kubadilika wakati taasisi nyingine zinapobadilika pia. Mabadiliko hayo yatakuwa katika kipengele cha lugha, ubunifu wa kijamii na mfumo wa maisha kwa jumla. Kwa hivyo, usanii wa kifasihi na uhakiki wake ni mambo yanayoweza kubadilika kwa mujibu wa wakati ili yatangamane na kiwango cha urazini wa jamii inayozungumziwa.

Tasnifu hii yaonyesha kwamba uhakiki wa matumizi ya lugha katika ushairi-huru ni sehemu ambayo haijazi-ngatiwa mno. Kazi yetu ni hatua katika kuingilia nyanja hiyo. Tumepata kwamba uhuru wa mshairi wa kuchagua muundo fulani kupanga vipengele vyake kwa njia fulani ni uhuru unaotawaliwa na kanuni za sanaa yake. Pia

inategemea uwezo wake wa kuvipanga vipengele hivyo ili vilete athari iliyokusudiwa kulingana na hali aliyo nayo mwandishi wakati wa kutunga shairi lake.

Ushairi-huru unapata uhai wake kutokana na uchambuzi wa umbile lake la ndani. Huu ni mfumo wake wa ndani ambao unafungamana na matumizi mahsusi ya lugha yenye kuibusha maudhui na hisia za mtunzi. Mashairi haya yanahitaji kwamba msomaji atafakari zaidi na kujihusisha katika hisia za mtunzi ili ayang'amue. Kwa hivyo, maana ya shairi haitokani na umbo lake la nje tu bali matumizi yake ya lugha. Mshairi yeyote awe huru kutumia fani inayofungamana vizuri zaidi na maudhui yake kwa mujibu wa hadhira iliyokusudiwa. Katika mashairi-huru, tumepata kwamba mpangilio wa herufi, silabi, mofimu hadi maneno na sentensi umeoana na maudhui ya mtunzi kwa madhumuni maalum. Mathalan, washairi hutumia kunga mbalimbali za kisauti na kimpangilio ili kuleta hisia fulani kwa msomaji au msikilizaji. Hii ina maana kwamba hisia za kishairi humfikia mtu anayesoma au kusikiliza katika lugha teule yenye mpangilio mahsusi wa maneno, picha, sauti na mdundo.

Tasnifu hii yaonyesha kwamba shairi ni muungano wa fani na maudhui. Mshairi hutunga shairi ili kueleza jambo fulani kwa hadhira fulani. Kwa hivyo, mshairi wa wakati fulani hulazimika kutumia kunga fulani pamoja na miundo ili kueleza fikra zake kishairi na

kueleweka vizuri. Pia kadiri wakati unavyobadilika, kunga na miundo ya utunzi pia hubadilika. Tunaafiki maelezo ya Kezilahabi katika Topan F.M. (1977:60) kuwa:

> Hakuna sheria za kutunga... zile ambazo wataalamu wanaita 'sheria' ni yale mambo yanayofanana katika mashairi fulani kwa wakati fulani: lakini si sheria.

Dondoo hili laonyesha kwamba miundo ya mashairi yanayosisitizwa na wanajadi si ya kipekee kama wanavyotaka watu waamini. Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa sanaa ya ushairi wa Kiswahili imepanuka na kuendelezwa na watunzi wasio Waswahili wa Pwani pekee. Tunakubaliana na Kahigi na Mulokozi (1982;56) kwamba:

> ... Uwanja wa ushairi ni mpana sana, hauanzii wala hauishii katika vina na mizani. Washairi wa Kiswahili wasitosheke na ujuzi walio nao na vilemba vya 'ustadh' na 'ushaha wa malenga' ... lakini si uthibitisho kuwa wamefikia upeo wa taaluma ya ushairi...

Ni dhahiri basi kuwa kuna mengi ya kufanya katika fasihi na hasa ushairi. Wale wanaoshikilia muundo mmoja wataachwa nyuma. Miundo mipya katika umbuji wa ushairi wa Kiswahili ni kioo cha jamii za sasa. Kwa hivyo, shairi la Kiswahili si lazima kuendelezwa kwa kanuni maalum zisizobadilika. Mashairi-huru ni mfano wa mazingira mapya.

Kazi hii yaonyesha kwamba kuendelea kutumia vina na urari wa mizani katika ushairi wa Kiswahili kwapasa kutegemea umuhimu wa matumizi ya vitu hivyo katika kujenga maudhui ya msanii. Ikiwa kutovizingatia kama ilivyodhihirika katika uchambuzi wetu hakufaidi au kuhasiri ushairi wa Kiswahili, si lazima kuendelea kuvitilia mkazo.

Mashairi-huru yaonyesha kwamba mdundo, ukiwa ni kule kurudiwarudiwa kitu au kurejelewa utaratibu fulani, kunaweza kujengwa katika viwango mbalimbali vya lugha: fonolojia, mofolojia, sarufi au mantiki. Katika kila mojawapo ya viwango hivi vya lugha kuna uwezekano wa midundo kadha wa kadha. Vina na mizani, yaani sauti na silabi, ni sifa za kifonolojia ambayo ni njia mojawapo tu ya kujenga mdundo katika mashairi. Mdundo pia unaweza kujengeka katika kiwango cha mofolojia, sarufi na mantiki ambapo mtunzi aweza kutumia takriri na tamathali nyingine za lugha ili kueleza ujumbe wake.

Uwasilishaji fikra, hisi, mawazo pamoja na tajriba kwa lugha inayovutia na kupendeza msomaji au msikilizaji ni sifa muhimu ya ushairi na fasihi kwa jumla. Kupendeza huko kunatokana na sababu ya lugha kutumiwa kisanaa. Uchambuzi wetu waonyesha kuwa mojawapo ya sifa za lugha

iliyotumiwa kisanaa ni urembo wake. Mdundo ni sehemu mojawapo tu ya pambo katika shairi. Kwa sababu hiyo, si lazima kila shairi liwe na mdundo ulio wazi ili livutie hisia za wasomaji au wasikilizaji. Kazi yetu yaonyesha kwamba kuna sifa nyingine za kifasihi ambazo huchangia urembo wa mashairi. Mathalan, shairi laweza kuvutia kwa sababu ya matumizi bora ya tamathali kama taswira, jazanda na tashihisi.

Uchambuzi wetu umedhihirisha kwamba muwala au mtiririko mzuri wa ujumbe hutokea katika lugha ya msanii ili kuleta mawasiliano yaliyonuiwa. Katika mashairi-huru, wazo linafululiza bila kusita au kukatishwa hadi mwisho kama vile ambavyo maudhui ya shairi lenyewe yanavyofululiza bila kutetereka hadi mwisho. Muundo wa shairi huoana na maudhui yake. Washairi hutumia kunga mbalimbali za kisauti na kimpangilio ili kuleta hisia fulani.

Ni dhahiri kwamba ushairi-huru hautaangusha ushairi wa Kiswahili bali utausukuma na kuukuza kufuatana na mwendo wa nyakati. Pia utaihuisha sanaa ya utunzi. Vina na urari wa mizani ni sifa za kijuujuu ambazo kutotumiwa kwake hakutaathiri ushairi wa Kiswahili ambao unaendelea kukua. Swala la uvyazi wa mitindo mipya katika ushairi wa Kiswahili lafaa kutiwa hima ili kuchangia ukuzaji na maendeleo ya ushairi wa

Kiswahili. Kwa hivyo, watu wenye dhana finyu, fikra potofu na ufilisi wa mawazo kuhusu ushairi wa Kiswahili yapaswa wakubaliane na ukweli wa mambo kuhusu maendeleo ya fasihi kwa jumla, ukiwemo ushairi wa Kiswahili. Kazi yetu imeongozwa na nadharia ya uhakiki hadi kufikia uamuzi wetu.

## 6.2. PENDEKEZO KWA UTAFITI ZAIDI

Uhakiki wa matumizi ya lugha katika mashairi-huru ni sehemu ambayo haijazingatiwa sana kinadharia. Mtindo ni swala linaloweza kujadiliwa kwa urefu tukizingatia mashairi haya. Inafaa utafiti zaidi ufanywe katika nyanja hii ya ushairi kwa kuzingatia watunzi kutoka Kenya ili kuona jinsi mazingira yalivyoathiri uteuzi wa lugha pamoja na maudhui ya watunzi.

Pia tungependekeza utafiti ufanywe kuhusu vipengele vingine vya ushairi ambavyo kazi yetu haikuzingatia. Navyo ni pamoja na ukiukaji na upotoshi sarufi maksudi, usuli au wizani na usambamba. Utafiti kama huo utawezesha kuonesha jinsi watunzi wanavyotumia uhuru wa kutamba katika uwanja wa lugha ya usanii ili waweze kueleza hisia na mawazo yao.

Ni matumaini yetu kwamba utafiti kama huu ukifanywa,

watu wengi watapewa hamasa ya kujitokeza na kutunga mashairi bila kubanwa na kutatizwa na arudhi za wanamapokeo ambazo hawazimudu. Hivyo, ushairi wa Kiswahili utapanuka na fasihi ya Kiswahili itakuzwa katika mazingira yasiyo ya Waswahili asilia.

MAREJELEO


Abdilatif, A. (1981). "Tanzu za Ushairi wa Kiswahili na Maendeleo yake." Karatasi ya Semina za kimataifa, Nairobi. (Haijachapishwa).

______________ (1973). Sauti ya Dhiki, O.U.P. Nairobi.

Abedi, M.A. (1954). Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri. E.A.L.B., Nairobi.

Adagala, K. (1981). Petals of Blood: A Study of Women Question and Imperialism. Karatasi ya Semina ya Wakurufunzi, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Anene, J.C. na Brown, G.N. (1966). Africa in the 19th and 20th Centuries: A handbook for Teachers and Students, Ibadan University Press.

Bakari, M. (1978). "The stage of the Art: Swahili Literature in the 19th Century." Makala katika Jarida La Historical Association of Kenya, Nairobi.

Boesen, J. na Wengine. (1977). Socialism from Above, Scandinavian Institute of African Studies, Uppsala.

Brett, E.A. (1973). Colonialism and Underdevelopment in East Africa, H.E.B., Nairobi.

Calvert, A.F. (1917). German East Africa, Negro University Press, New York.

Chacha, N.C. (1987). Meaning and Interpretation of Swahili Poetry: A Portrayal of a Changing Society. Tasnifu ya Ph.D. Yale University. (Haijachapishwa).

Chapman, R. (1973). Linguistics and Literature: An Introduction to Literary Stylistics. Edward Arnold.

Chiraghdin, S. na Nabhany, S. (1975). "Tarehe ya Ushairi wa Kiswahili" katika MULIKA NA 7, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar Salaam.

Coombes, H. (1965). Literature and Criticism, Penguin Books, Middlesex.

Crystal, D. na Davy, D. (1969). Investigating the English Style, Longman, New Zealand.

Dorch, T.S. (1965). Classical Literary Criticism Penguin Books, London.

Fanon, F. (1963). The Wretched of the Earth, Presence Africainne, Paris.

__________. (1967). Black Skins White Masks Grove Press, New York.

Fischer, E. (1959). The Necessity of Art, Penguin Books, London.

Harries, L. (1962). Swahili Poetry, Claredon Press, London.

__________. (1966). Poems from Kenya, University of Wisconsin Press, London.

Hough, G. (1973). An Essay on Criticism, Duckworth, Britain.

Hussein, E. (1969). Kinjeketile, O.U.P., Nairobi.

__________. (1971). Mashetani, O.U.P., Nairobi.

Hyden, G. (1980). Beyond Ujamaa in Tanzania, H.E.B. Nairobi.

Illife, J. (1969). Tanganyika Under German Rule, 1905-1912, East African Publishing House, Tanzania.

__________. (1973). Modern Tanzanians, East African Publishing House, Tanzania.

__________. (1979). A Modern History of Tanganyika, Cambridge University Press, London.

Imbosa, R. (1990). Jazanda Katika Ushairi wa Muyaka. Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kahigi, K.K. (1975). "Ushairi: Mtazamo wa Kisayansi" Makala katika KISWAHILI JUZUU 45/1, Jarida la TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

__________ na Mulokozi, M.M. (1973). Mashairi ya Kisasa, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

__________. (1976). Malenga wa Bara, East African Literature Bureau, Arusha.

__________. (1982). Kunga Za Ushairi na Diwani Yetu, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Kandoro, S. (1975). Ushairi Wa Mashairi Ya Kiswahili. Longonman, Nairobi.

Kaplan, C. (1975). Criticism: The Major Statements, St. Martins, New York.

Kezilahabi, E. (1974). Kichwa Maji, East African Publishing House, Dar es Salaam.

__________. (1974). Kichomi, H.E.B., Nairobi.

__________. (1975). Dunia Uwanja Wa Fujo, East African Publications Ltd., Arusha.

__________. (1980). Rosa Mistika. Kenya Literature Bureau, Nairobi.

__________. (1981). Gamba La Nyoka, East African Publications, Dar es Salaam.

__________. (1983). "Historia Fupi Ya Ushairi wa Kiswahili." Makala ya Semina ya Waandishi III, Dar es Salaam.

__________. (1988). Karibu Ndani, Dar es Salaam. University Press.

__________. (1990). Nagona, Dar es Salaam. University Press.

______________. (1991). Mzingile, Dar es Salaam. University Press.

Khatib, M.S. (1975). "Washairi Wa Kiswahili Wanavyoliona Azimio La Arusha" katika KISWAHILI JUZUU 45/2, Jarida la TUKI, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Kirumbi, P.S. (1975). Misingi ya Fasihi Simulizi, Shungwaya Publishers Ltd., Nairobi.

Kitsao, J. (1982). An Investigation of Themes in Swahili Literature and Application of Stylistics to Chosen Texts. Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Knappert, J. (1979). Four Centuries of Swahili Verse, A Literary History and Anthology, Heinemann, Nairobi.

Knud, E.S. na Marete, T. (1969). Self-Reliant Tanzania, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Leech, N.G. (1969). A Linguistic Guide to English Poetry, Longman, London.

____________ na Short, M. (1981). Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose, Longman, London.

Lodge, O. (1972). 20th Century Criticism, Longman London.

Mayoka, J. (1977). "Vina na Mizani ni Uti wa Mgongo wa Shairi wa Kiswahili" katika MULIKA NA 7, TUKI, Dar es Salaam.

___________. (1986). Mgogoro na Ushairi na Diwani ya Mayoka. Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mazrui, A. (1982). Kilio cha Haki, Longman, Nairobi.

____________ na Kazungu, K. (1981). "Historia na Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili." Karatasi ya Semina za Kimataifa, Nairobi. (haijachapishwa).

Mbaabu, I. (1985). New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research and Literature. Kenya Literature Bureau, Nairobi.

__________. (1985). Utamaduni wa Waswahili. Kenya Publishing and Book MWAMKO Toleo la 5 Jarida La Chama Cha Kiswahili, Chuo Kikuu, Nairobi.

Mnyampala, M. (1965). Waadhi Wa Ushairi, E.A.L.B. Kampala.

Mohamed, M. (1981). 'Fani na Maudhui'. Misingi ya Nadharia ya Fasihi. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Tanzania.

__________. (1981). Fasihi na Lugha, Taasisi ya kiswahili na Lugha za Kigeni, Tanzania.

Momanyi, C. (1991). Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mulokozi, M.M. (1975). "Revolution and Reaction in Kiswahili" katika KISWAHILI Toleo 45/2, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

__________. (1982). "Protest and Resistance in Swahili Poetry, 1600-1885" katika KISWAHILI JUZUU 49/1, TUKI, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

__________. (1992). Ngoma ya Mianzi, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

__________. (1974). "Mapinduzi ya Nyumbani." Makala katika MZALENDO, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

__________. (1976). "Siri ya Bwanyenye" katika MZALENDO, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

__________. (1973). "The Revolutionary Tradition in Swahili Poetry." MAJI MAJI NA 8, Dar es Salaam.

______________. (1974). "Fasihi na Mapinduzi" Kioo cha Lugha NA 6, Dar es Salaam.

______________. (1977). "Ushairi na Ukasuku", katika KISWAHILI JUZUU 47/2, TUKI, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

______________. (1977). Fasihi na Mapinduzi, Kioo Cha Lugha, Jarida La Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

______________. (1979). Mukwava Wa Uhehe, East African Publishing House, Nairobi.

Nassir, A. (1971). Malenga Wa Mvita, Diwani ya Ustadh Bhalo, O.U.P., Nairobi.

Ngara, E. (1982). Stylistic Criticism and the African Novel, H.E.B., Ltd. Nairobi.

Ngugi wa Thiong'o (1977). Home Coming, H.E.B., Nairobi.

Nowottny, W. (1962). The Language Poets Use, The Athlona Press, University of London.

Nyerere, J. (1973). Freedom and Socialism, O.U.P., Nairobi.

______________. (1973). Freedom and Development, O.U.P., Nairobi.

Ogot, B.A. (1974). A Survey of East African History. New Edition, Longman, Nairobi.

Peck, J. na Coyle, M. (1984). How to study Literature, Literary Terms and Criticism, Macmillan Educational Books, London.

Pope, A. (1961). Pastoral Poetry and An Essay on Criticism, Methuen and Co. Ltd., London.

Rodney, W. (1972). How Europe Underdeveloped Africa, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Ruo, K.R. (1989). *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili.* MacMillan, Nairobi.

Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi,* Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

_______________. (1987). *Fasihi na Jamii,* Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

_______________. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki,* Dar es Salaam University Press.

Shivji, I.G. (1974). *The Silent Class Struggle,* Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Short, M. (1989). *Reading, Analysing and Teaching Literature,* Longman, London.

Svendsen, K.E. (1969). *Self-Reliant Tanzania.* Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Topan, F. (Mhariri) (1977). *UChambuzi wa Maandishi ya Kiswahili,* Kitabu cha Pili, O.U.P. Nairobi.

Turner, G. (1983). *Stylistics,* Penguin Books, Harmondsworth.

Wanjala, C. (1980). *For Home and Freedom,* Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Wanyoike, E.N. na Wengine. (1976). *Lugha.* A Journal for Language Teachers in Kenya Vol. 5, No. 1 Kenya Language Association.

Wellek, R. na Werren, A. (1982). *Theory of Literature,* Penguin Books, Harmondsworth.

Widdowson, H. (1975). *stylsitics and the Teaching of Literature,* Longman, London.

## FAHARASA

## NYONGEZA 1

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIWA KATIKA TASNIFU

### (I) TASWIRA

Ni picha ziundwazo na maelezo ya msanii katika shairi. Ni picha ya chochote kile kinachofanana na kitu au jambo fulani katika maelezo ya msanii. Ni mbinu ya kimtindo ambayo msanii hutumia kuifinyanga kazi yake ambapo anatajirisha kazi yake ya sanaa kwa kutafsiri maana kupitia kwa mahusiano fulani kwa lugha ya picha.

Madhumuni ya taswira ni kurahisisha njia ya kufanya msikilizaji au msomaji aupate ujumbe wa mwandishi kwa kuhusisha taswira hiyo na hali halisi za jamii. Kwa hivyo, jukumu la taswira ni kuweza kujenga dhana katika akili na kusaidia kuumba na kuangaza uhalisi wa mambo ya jamii.

### (II) TASHIBIHI

Hii ni tamathali ya ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Ni mtindo wa kifani ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au hufananishwa

## NYONGEZA 2

## MASHAIRI YENYE MAUDHUI YA SIASA

### 1. Mafahali Wapigana

1. Mafahali wenye matumbo wanapigana.
Chini, chini, chini zaidi
Mpaka vichwa vyao vinagusana.
Halafu watazamaji wakondefu.
Wanaanza kupiga kelele.

2. Haya! Haya! Machakulo* haya!
Pole pole hawaoni kitu.
Vumbi hewani, vumbi machoni.
Vumbi kuisha, mshindwa amekwisha kimbia.

3. Mshindi juu ya kichuguu amekaa,
Akionyesha kidole kimoja sasa
Mchwa ndo askari.

4. Kilikuwa kivumbi hicho.
Sasa pahali hapo pametulia tuli,
Ambapo kutembeza midomondo kusikika
Kunyamaza ndo basi kudhaniwa.
Patelivu! Patulivu! Patulivu kweli!

*Machakulo: Jina la fahali mmoja kati ya hauo wawili.

5. "Basi kama mchwa
Tujenge kichuguu
kama mchwa tuungane
Na kuulainisha udongo," anasema.

6. Patulivu! Patulivu! Patulivu!
Lakini! Lakini! Lakini!

## 2. Kuchambua Mchele

1. Habari zilifika kutoka ARusha
Tukaanza kuchambua mchele wa ujamaa
Macho mbele, macho pembeni, tukitoa mchanga.
Tukafanya kaburi dogo la mchanga.

2. tukaanza kutoa chenga, mojamoja.
Vidole vikafanya kazi kama cherehani
Usiku na mchana; macho yakauma.
Tukafanya kichunguu kidogo cheupe.

3. Chenga na mchanga vikawa vingi sana.
Tukapika baada ya muda mrefu wa kazi.
Tukaanza kula,
Tukakuta bado mchanga na chenga!

4. Lini tutaula bila mchanga, bila chenga?

## 3. Hatumwoni

1. Hao miungu waliosimama vichaka
Wambieni wakae chini warefu.
Kaeni chini! Wengi nyuma, hatuoni!
Hatutaki vyenu vichafu visogo kuona.
Kaeni chini miungu, kaeni chini!

2. Ndugu kaeni chini, kaeni chini ndiyo amri
Acheni acheni kelele. Kelele za jaza-tumbo
Kaeni chini! tulo nyuma kweli yatuchoma mioyo.
Twataka chagua watu, watu watu.
Mlipewa uongozi, ukawapaka rangi
Na madaraka, madaraka yakawalevya
Sasa yavueni wapisheni wenye nia!

3. Au hamjaona hasira, ikifura ya wengi watu?
Ulizeni ya saidi aliyechomoa sokoni
Na ya Abadalla aliyegonga maskini?
Miungu, nanyi ndugu, chini pwetekeni
tuwakanyage tupite mbele tujisukume
Sisi twauza bidhaa ninyi mwauza maneno!
Tuko sawa haikai mdomoni.

4. Kateni yote misitu, fimbo tuenee
Na vinyago tuwachonge watoto wachezee.
Kausheni yote maziwa maji tuwalowanishe
Kukipambazuka wasiweze ruka angani.
Kokeni mioto, mashujaa wa uonevu tuwabanike.
Kamswe hapatakuwa na kilio wala matanga
Bali hoi hoi za ushindi na madaraka kwa umma.

## 4. Kifo cha Mende Wekundu

1. Na ujenge yako nyumba, jingi jasho likuoshe
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

2. Wataanza kutalii mipaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yao, ijara ya kaziyo.

3. Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa ngumu hawafi mende rahisi.

4. Kifo cha mende sharti miguu juu,
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake,
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

## 5. Jua la Dhahabu

1. Nimeona Jua la Dhahabu
Katika mji wa Arusha:
Miali yake imepenya
Anga la nchi yangu
Na kukifukuza kiza
  Mbele ya macho yangu.

2. Nimeona Jua la Dhahabu
Katika mji wa Arusha
Likanimulikia njia
  Nisiweze kujikwaa.

3. Waka!
Waka Jua la Dhahabu
Toka mji wa Arusha!
Waka ulete mwangaza
Mahali palipo kiza
Waka, mulika vidato
Vya wanyonge kupandia:
Waka, nionyeshe njia
  Ya kufuatia.

4. Nimeona Jua la Dhahabu
Katika mji wa Arusha,
Miali yake imepenya
Anga la nchi yangu
Na kuwasha tabasamu
  Ndani ya moyo wangu.

### 6. Damu Mpya Yatiririka

1. Sikiliza ndugu zangu
Sisi ni wimbi, wimbi la ujana
Nyota yetu inawaka
Na njia twaiona mbele.

2. Na damau mpya yatiririka
  Katika mishipa ya bahari hii;
Damu mpya yachemka
  Katika ubongo wa kizazi kipya.

3. Naam: oneni hayo mapengo
  na mashimo ya jana na leo
Sasa yameshaanza kuzibwa.
Oneni hirizi na midali
  Za uwongo wa jana na leo:
Sasa zinapigwa teke.

4. Na sikieni sauti ya damu mpya:
"Tukaweka mbolea kwenye shamba letu
Tupande mbegu bora za maharage
  na mtama
Na mimea yenye rutuba iote, ikue,
  tuvune.
Na misuli yetu
lazima ijenge nyumba mpya
Pahali pa nyumba za jana."

5. Damu kongwe yenye ukaidi
Haifui dafu kwa damu mpya;
Na ndege wa matumaini anaimba.
Damu mpya kwa furiko
Inachemka kwa mwendo wa mbele.
Tazama! Kule upeoni
Mawingu yanakusanyika
Ishara ya matumaini yenye
kuneemesha maisha.

6. Sikiliza ndugu zangu
Sikiliza ujumbe wa wimbi:
"Enyi wanajeshi!
Nyota yenu inawaka:
Shot - kulia; shot - kulia -
MBELEE tembea - !"

## MASHAIRI YENYE MAUDHUI YA UCHUMI

### 1. Azimio

1. Azimio sasa ni mabaki ya chakula
Kwenye sharubu za bepari
Kalamu inayovuja
Katika mfuko wa mwanafunzi
Vumbi zito
Baada ya ng'ombe kupita.
Hakunyolewa
Hakupewa kalamu mpya
Na njia haikuzibwa.
Kilichosalia sasa
Ni punje za ulezi
Zilizosambazwa jangwani
Na mpandaji kipofu.

## 2. Ngoma ya Kimya

1. Wacheza ngoma wamekwishaoondoka
Kilichobaki ni uwanja uliokauka majani,
Njuga, manyoya na kindu zilizodondoka
Toka kwa wachezaji waliozidisha mbwembwe
Nao watazamaji wakipigia kelele na vigelegele.
Ni jana tu walikuwa hapa.
Wachezaji sasa wafikiria ngoma ijayo.
Watazamaji hawayakumbuki maneno
Ya nyimbo zote zilizoimbwa.
Zilizobaki ni taswira hai na vivuli.

2. Lakini labda miti hii michache yakumbuka.
Nitaviokota nitengeneze vazi langu
Kisha nitacheza ngoma yangu kimyakimya
katika uwanja huu mpana ulioachwa wazi
Bila watazamaji
nao upepo ukinifundisha lugha ya kinya
Maana yule mwanamke amekwishajifungua.

## 3. Afrika na Watu Wake

1. Mimi ninaona mgonjwa
Bado amelala kitandani.
Kama hatutamtoa miiba iliyobaki
Mgonjwa hataweka miguu yake chini
Ili kutembea bila kujigemeza.

2. Miiba iliyomo ndani mwetu lazima
Pia iondolewe upesi kabla haijaingia
Kati ya mifupa na kufa pamoja nasi.
Baada ya kuitoa tuvae viatu vya chuma
Halafu tucheze na mchezo wa siasa na uchumi.

3. Lakini kuitoa miiba hii
Tunahitaji macho makali
Mikono isiyotetemeka
Moyo usio na huruma
na kuona miiba ilipoingilia.

### 4. Uliza Wanaojua

1. Wako wapi waliokuwa viongozi zamani
Waliokitoa hotuba ujamaa kuupigania?
Sasa wamestaafu ndio wafuga kuku
Ndio wenye majumba ubepari kurithisha!
Kama weere hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.

2. Au hujaona makabaila wenye mashamba
Matrekta yanafukuta na vumbi kutimuliwa!
Zungumza juu ya vijiji wakakuonyesha kidole
"Pilipili usiyoila yakuwashiani!"
Basi kama were hujui, uliza wanaojua
Ukweli watakwambia.

3. Lakini Darubini la Serikali ni kubwa sana
Tena lina nguvu sana na lina sumaku.
Linawavuta wakapimwa
Chote walichokwisha kula kitaonekana.
Rafiki, kama wewe hujui, basi uliza
Wanaojua. Ukweli watakwambia.

4. Hata dawa ya kutapisha Serikali inayo
Mabepari na Makabaila wametapishwa hadharani
Wakaona na aibu mbele ya wake zao.
Wananchi tuliwazomea tena tukacheka sana.
Ndugu, kama wewe hujui, basi usinyamaze.
Uliza wanaojua. Ukweli watakwambia.

### 5. Maombolezo ya Mtu Maskini

1. Panya wa uhitaji aniguguna tumboni,
Na kunikeketa kama msumeno.
Simba wa ubepari anaipachika makucha
Na kunitia mashimo mifukoni,
nami nabakia kutangatanga
Na kupepesuka kama utete tufanini.

2. Tanuu ya jua imeikaanga ardhi yangu,
Jabali la udongo limelibutisha jembe langu,
Na matiti ya uwingu wenye ubahili
Yameninyima maziwa ya kuinyweisha ardhi yangu-
Ardhi ya riziki, riziki ya maisha.

3. Radi ya maradhi imeuangukia mti wa nasaba yangu,
Na kuung'oa hadi mizizini,
Mishale ya upofu imenifuma macho yangu
na barafu ya umri imegandia kichwani pangu;
Sina kimbilio, sina tegemeo
Sina hisi yoyote ya faraja upeoni!

4. Shuburi ya ufakiri umeizimua sukari yangu ya maisha,
Na miiba ya dhuluma imeitoboa mikono yangu
nisiweze kujikimu:
Maradhi yamezidi dawa
Na funza wa shutuma amenitekenya nyayo zangu
nisiweze kusonga mbele.

5. Nimekuwa mtumwa katika dunia huru
Fakiri katika jumuiya tajiri;
Nachungwa na kuswagwaswaga
Kama sarakasi katika uzi!

Kwa nini? Najiuliza.
Kwa nini nasumbuka hivi, kwa nini nateseka hivi?
Natangatanga, nadidimia, nageuka kiguu na njia?
Sijui.
Labda nilikufa kabla ya kuzaliwa,
na sasa naishi baada ya kufa.

Katika enzi zisizokuwa zangu,
  Katika nchi isiyokuwa yangu!

Labada siishi ila nipo tu
Kama kitu tu, kama kijiwe tu, kama kijiti tu!
  Labda naipo siku ya wokovu abadan!

6. Lakini hilo si kweli, najua:
Siku ya wokovu ipo,
Siku ya kukombolewa inakuja!
Itafika!
Itafika siku, siku hiyo isiyo kifani:
Dunia itapinduka
mambo yatasawazika
Mtu atakuwa mtu
Heshima itatang'aa,
Miungu ya ukabaila itakufa
Na mwanadamu atakuwa huru,
Makanisa ya udhalimu yatabomoka
  Na misahafu ya ubepari itafutika.

6. Enzi Za Mapambano

1. Enzi hizi za mapambano
Nukta hizi zidundazo kwa haraka
kama pumzi ya mgonjwa anayekata roho
Au kama moyo wa kibarua mbele ya meneja;
Enzi hizi za jua lielekealo machweo daima
Ndugu, hizi ni enzi za mapambano!

2. Mapambano gengeni
Mchicha umepanda bei na kauzu wana mchanga
Nyama huliwa na mwinyi na changu huliwa na wazungu!
Na'mnunia ngoa' ni unga mtupu
Mapambano mabarabarani
Mavolvo yanafanya fujo mitaani
Na marenja yanabomoa njia zetu za udongo!

3. Mapambano mahotelini
katika mbuga za wanyama, katika mitaa ya kati mchana
Na mitaa ya pembezoni usiku
Manywele wametanda kama wimbi la sotoka
Wanakuja na dola katika dola inayowaabudu
Na kuleta kanuni mpya ya kuishi kwa watu wasio na maisha

4. Mapambano vilabuni
Bia hazinunuliki, kangara imezuiwa Manzese
Safari ni ya watalii na ulaka una mabibo ndani
Chibuku ni uji wa jioni
Kabwela kafumaniwa na gongo Manzese Jumapili
Mgambo! Magongo hayatoshi!
Bunduki zinaridima! Makabwela wanalala ndani ya gongo lao!

Muhanga wa Soweto!

5. Ndugu ujuaye na wewe usiyejua
Siku zimepanda bei
Na kila dakika ni mpwito wa mapambano!
Mampambano kitandani
Kabwela agomea shilingi tano
Katika mtaa wa 'Paris' Temeke
Mwanayamala A, Mwanayamala B
Magomeni Mapipa, Magomeni Makuti
Ubaguzi umekwisha, mitaa ya Wahaya sasa ni ya wote
Dhiki ya mapambano haina kabila!

6. Mapambano kanisani
Kasisi ataka zaka gwanda limechakaa
Mbao hazina watu ila wazee na watoto
Sanamu ya Maria imekusanya vumbi
Msalaba wa yesu umepata kutu
Kengele ya Jumapili ni mwito wa mapambano!

7. Mapambano ya suhleni
Vijana wamegoma kula ugali una wadudu
Amri amri amri zimeshamiri
Vyuo vimekuwa seminari na hali mapenzi hayana
  nidhamu
Chuo Kikuu kinachua na wazee ni watoto!

8. mapambano viwandani, kibwanyenye chafungiwa chooni...
Mapambano katika UDA, shilingi ndani, mia mlangoni...
Mapambano mipakani... Mtukula...

9. Ndugu ujuaye na wewe usiyejua
Shida zimepanda bei
Maisha yananunuliwa na mauti pia,
Hivyo ni vibaya lakini ni vizuri:
Ni mwito wa mapambano!

## MASUALA MENGINE YA KIJAMII

### 1. Kisu Mkononi

1. Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
Siwezi, kama gurudumu nitajiviringisha.
Mtelemko mkali huu.
Lina na wapi mwisho sijui:

2. Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya dhambi.
Kisu, maisha kafiri haya
Kama kutazama nyuma au mbele
Ni kufa moyo mzima!

3. Sasa kama Simba-Mtu shauri nimekuta.
Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili.
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa,
Kila mpigo wa moyo wangu
Huu mpigo muziki wa maisha.

## 2. <u>Hadija</u>

1. Hadija
Umekata mti mtima
  Umeangukia nyumba yako.
Umeziba mto hasira
  Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
  Watoto kuwakimbia.
Mbuzi kumkimbia chui
  Alijigeuza panya
Akalia kuliwa na paka
  Mchawi kutaka sana kutisha
Alijigeuza simba
  Akalia na risasi kichwani

2. Jongoo kutaka sana kukimbia
  Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka.

3. Hadija wapi sasa utakwenda
  Bwanako kumpa sumu?
Hadija umemshika nyoka kwa mkia.
Hadija umepita nyuma ya punda.

## 3. Karibu Ndani

1. Washairi wa mapokeo, sasa wacheza lalasalama
Katika mionzi hafifu, ya jua machweoni
Na mahadhi yagaagaa, juu ya bahari ya utenzi
Yameshindwa chini kuzama, kwenye kina cha urazini
Nao wahenga vibandani, nje tena hawatoki
Hakuna tena ngoma, ya kugeeana kani
Na ushairi umehama, umerudi upeponi
Lakini majani makavu, sasa hayatingishiki
Nayo madirisha ya nyumba, imara yamefungwa
Waliomo ndani wahofu, hasira ya mizimu.

2. Muda si mrefu, patakuwa kiza totoro
na wanyama wa usiku, watazitawala taswira
Kwa kuwa njia naikumbuka, msitu nitauingia
Kwenye kiza cha karne, pasipo vichochoro mkato
Nikiwa na nanga yangu, nyimbo mpya tatongoa
Tatumia silika ya uzawa, kuupata mwelekeo
Maana ushanga wa shingoni, bado sijautupa.

Na hiki kibanda gani, ghafla mbele yangu!
Ni kibanda msonge, mlango wake mmoja
Mlango wenyewe u wazi, na ndani moto wawaka.
Hodi Hodi wenyewe, ni mimi Kichwamaji
natafuta zangu njuga, na lile vazi la kindu
Ingawa sina ubuyu, naja kukesha nanyi.

II

4. Ni kibanda kuukuu, kuanguka kimekaribia
Mhimili wake ni mmoja, umeanza kukatika
Nao mchwa walialia, paa si paa tena
Karibu na huu mhimili, katikati ya kibanda
Kuna kigoda kikubwa, ngozi ya chui pambole
Mbele yake pana moto, vijinga vyake mifupa.

5. Ukutani pametundikwa, ala nyingi za muziki
Humo ndani ya kibanda, pamekaa vizee kimya
Vichwa vyao vimeinama, chini kifikra vyatazama
Karibu na huo mhimili, ajuza ainua kichwa
Naye mbwa ghafla, ainuka akbiweka
meno mdomoni hana, lakini povu malfura
Vizee vingine vyastuka, vichwa vyao vyainua
macho yao makali, yatua usoni pangu
Mbwa abweka tena, kama kwamba kushambulia
We Mavina! Lala chini! ajuza amuasa
Akinitazama kwa makini, kimya anichunguza.

6. Karibu ndani asema, hapa hujawa mgeni
Tumekuwa tukikusubiri, ingawa umefika mapema
Umo ndani ya duara, ukinaswa nasika
Ulipo umezingirwa, kumbukumbu zilokufinyanga
Hapa ulisafisha zako fizi, kwenye titi la mama
Na huyu ndiye mbwa, aliyekulamba kidevu
Na hizi ndizo nyuso, zilizopima hatua zako
Ulipoingia na kutoka, ndani na nje ya ua
Juu ya hili paa, palitupwa meno yako
Tunashukuru umefika, pe' kitovi cha utambulisho
Ingia sasa ngomani, ufnge fundo la kitali.

7. Hiyo ala ulonayo, tenzi zake twazikumbuka
Sifa zako zimetufikia, na huo wenu mgogoro
Nyimbo za wanamapokeo, ni nzuri si utani
Zina mahadhi na mdundo, pia zatia hamasa
Lakini zilitulaza, usingizi mapema mno
Ikawa kama kwamba, Mungu alitusahau
Lakini nyimbo zako, zimezindua taaluma
Mlango sasa u wazi, wajao wafuate nyayo.

8. Sasa tazama ukutani, masalia ya wako utu
Changua ala moja, ukae juu ya kigoda
Tuna hamu ya kucheza, tupate kukoga karne.

## 4. Hatima ya Kila Mwali

1. Ama sihofu kamwe kuondolewa
Kabla ya kofia ya pili kuvaa,
Mimi ni mwanamwali, nilichumbiwa
Siku ile mama aliponizaa.

2. Mimi ni mwali na hivyo ninajua
hatimangu asilia kuolewa;
Kuacha ndugu na wote 'naojua
Hata ng'ambo ya pili kuchukuliwa.

3. Huko ng'ambo ya pili ninaambiwa
Nyanya zangu ndiko walikoolewa,
Nami kwenda huko ningefurahia
Japo kiza totoro kimepajaa.

4. Kimila, jioni jua likivia
Mchumba huja mkewe kuchukua,
hapo mwali mashua huabiria
Na harudi tena akisha twaliwa.

5. Kwa hiyo ninakaa nikitambuwa
Jioni taja mumengu kunitwaa;
Ninajirembua, ninajikwatua-
Kwa harusi yangu ninajiandaa.

## 5. Wimbo Uliosahaulika

1. Nitauimba wimbo wa kale uliosahaulika,
Nitauimba wimbo wa jandoni;
na nitacheza manyanga kwa mchagisho wake.

2. Nitajitakasa na najisi hii inayonuka:
Matope yanayochubua ngozi yangu,
Mitishamba ya kigeni inayoukwajua mwili wangu,
Dondandugu linaloitafuna roho yangu,
  Ukoma unaoihusuru nafasi yangu.

3. Nitaukata mnyororo huu wa utumwa
Unaoning'iniza talasimu za kigeni shingoni pangu,
Nitakataa kuzainiwa na uwongo wao
Na kutetemeshwa na mizimu nisiyoijua,
Sitaziingia kumbi zao
  Sitashiriki katika ufasiki wa ngoma zao.

4. Nitajifunga 'kishenshe' kiunoni pangu
Nitajifunga lubega kwa fundo la jadi;
Nitachukua ngao na mkuki wangu
Kutetea hadhi ya mababu zangu;
Nitajikatia njia katika safu zao
  Hadi ng'ambo ya pili, penye Mbuyu wa mahoka wangu.

5. Nitatambaa kwa tumbo langu
Kuuendea Mbuyu uniitao
Na nitasujudu kwa moyo wa toba
Chini ya ngao ya mikono yake
  Iliyonyooshwa kunikumbatia.

6. Nitamsihi wakili wa Mahoka na Mizimu
Azilete Ngoma zake zote
Na Simbi zake takatifu
na Mikia ya Nyani wasio na doa
Na Tunguri zake za ajabu
Zilizojaa damu ya baraka ieuayo;
Naye atacheza
na kufanya miujiza yote ya kale
Mbele ya Moto uchangamshao

Chini ya ule Mbuyu;
Na pamoja naye
Nitaicheza Ngoma Kuu ya zamani
  Na kufarijika.

7. Nitawasihi wahenga wa ukoo wangu
Kuteuwa Beberu mweupe mwenye ndevu
Ambaye sufu yake i kama theluji
Ambaye pembe zake zi kama meno ya ndovu,
Wamlete penye madhabahu yaliyosahaulika
Penya shina la Mbuyu,
Wamtoe kafara kwa niaba yangu
Ili niapte kuokolewa
Ili nipate kutakaswa
Na kutuzi hili, masalia
  Ya ustaarabu uliokufa.

6. Habari Mpya

1. Siku moja tukiwa kanisani
Kasisi katamka toka altarini:
"Dunia mja mzito wa maovu!
Yafaa kuchomwa moto! Kwani wokovu
Waupatao ni haba! Wengi wetu
Hatuukumbati fuadini katu:
Hatumhitaji Mungu, hatutaki wokofu!
Tunabwata siku hizi kuwa hakuna Mungu Mtukuka
Eti kesha kufa! Lakini majuto mjukuu
  Tutajuata kwa ujinga huu!"

2. Kanisa likazima pumzi.
Kisha kijana mmoja pandikizi
Kasimama na ksuema (na sauti yake ilisikika
ng'ambo):
"Dini ni mja mzito wa uongo na maovu!
Ushirikina ulotia wengi makovu!

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Gofu la taasisi linalojikongoja
Fikira na maendeleo ya mtu kufuja-
Yafaa kuchomwa moto! Kwani uwongo huu
Umeangamiza wengi! Wanaukumbata kwa kiruu
Unawapofusha, unawapumbaza, unawalemaza!
Wokofu wa mtu hautoki mbinguni!
Wokofu wa mtu ni hapa duniani!
Vitisho vya Jahanam sikuze si hizi,
Siku hizi za zinduko na mapinduzi!
Nimesema! Majuto mjukuu humkuta
  Mwongo ukweli asiyekamata!"

3. Kanisa likazima pumzi kwa kimako kikuu.
Kasisi, macho matumbwi, kawayawaya
Chini kadondoka. Pumzi kote twii.
Katekista akenda kumnyanyua, kakuta mkavu.
Kiwewe, kiherehere, hangaiko.
  Kanisa likashiwa mashaka.

4. Kuzima pumzi, kanisani kukazidi.
Pakatanda wasiwasi baridi.
"Amekufa!" Katekista kagwaya; woga wakavuvumka
Kukimbilia nje, wakihofu jicho la kifo.
Mashujaa wakenda pale. Vilio vya wanawake na
  watoto
    Vikaanza kupahinikiza pale.

5. Radi ikanguruma, umeme ukafyatuka,
na mvua ikanyesha.
habari mpya zilikuwa
Zimetangazwa kanisani.
  Ziliweza kusikika hata ng'ambo.